ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae

30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA NANE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 16 Januari, 2013

Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi

WIMBO WA TAIFA

DUA

Mhe. Spika *(Pandu Ameir Kificho)* alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kukukaribisheni katika Mkutano wetu huu, Mkutano wa Kumi wa Baraza la Nane la Wawakilishi hapa Zanzibar Unaokutana kuanzia leo hii tarehe 16/01/2013.

Pili nikupongezeni na kukupeni hongera na heri ya Mwaka Mpya ya mwaka 2013 ambao kwa mwaka huu wa 2013 huu ni Mkutano wetu wa kwanza na ni Kikao cha kwanza kinachoanza leo. Kwahivyo karibuni sana na Mwenyezi Mungu awajaalie nyote mafanikio mema.

Waheshimiwa Wajumbe Taarifa ya Spika ya leo ni kama ifuatavyo:-

Katika Mkutano wa Tisa wa Baraza la Nane la Wawakilishi ulioanza tarehe 10 Oktoba, 2012 hadi tarehe 24 Oktoba 2012 Baraza lilipitisha Miswada mitano ya Sheria kama ifuatavyo:-

- Mswada wa Kwanza ni Mswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi Nam. 7 ya Mwaka 2005 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

- Mswada wa Pili ni Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi ya Biashara na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

- Mswada wa Tatu ni Mswada wa Sheria wa Kuanzishwa kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na mali Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

- Mswada wa Nne ni Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na Kuanzisha Baraza la Maafisa wa Afya ya Jamii na Mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

- Mswada wa Tano ni Mswada wa Sheria kuhusiana na hifadhi na usimamizi wa vihatarishi vya afya ya jamii na afya ya mazingira na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 90 (3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2012 naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Naomba kuwasilisha taarifa hiyo kwenu.

Nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuipokea taarifa hiyo kwa moyo mkunjufu.

Taarifa ya pili ndogo leo hii kama kawaida yetu chombo chetu hichi huwa kinatembelewa na wageni mbali mbali. Leo tunae mgeni mmoja ambaye ni ndugu zetu, marafiki zetu wa Norway. Mgeni wa leo aliyefika ni ndugu yetu bibi Elizabeth huyu ni Afisa kutoka Ubalozi wa Norway ambaye anafanya kazi nasi na ubalozi wake kwa karibu sana kwa shughuli mbali mbali.

Madam Elizabeth you are most well come. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha kutufikisha mwaka 2013, kwa misingi hiyo naomba nitoe heri za mwaka mpya kwa wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi wote wa Zanzibar na kuutakia mwaka huu kheri, mafanikio na amani kubwa sana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani, nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 25 Oktoba 2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada ama Sheria kwa marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997 na Mambo yanayohusiana na hayo, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuamka salama na kukutana tena katika Baraza letu hili tukufu kwa kipindi hichi cha mwaka 2013, namuomba Mwenyezi Mungu atuongozee na atupe mafanikio yaliyo mema.

Pili nakushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Mswada huu katika Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha

hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria na Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997 na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 31

Sababu za Kutokuunda Tume za Uchunguzi Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mhe. Spika, na nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuingia kwenye mwaka mpya wa 2013. Pia nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi ya mwanzo kwa *back bencher* kwa mwaka huu kwa kuanza kuuliza swali langu.

Ndani ya macho ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla suala la kushuhudia mateso, vipigo, ukamataji na hata mauaji, vitendo vinavyofanywa na Jeshi la Polisi sio vigeni. Yamewahi kutokezea mauaji ya raia wasio na hatia mwaka 2001 na hata mwaka 2012 pale Chama cha Chadema kilipojaribu kufanya maandamano na mikutano ya hadhara mkoani Morogoro na Iringa na kupelekea malalamiko kwa Jeshi la Polisi hatua ambayo imepelekea SMT kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuunda Tume ya Uchunguzi ya Kuchunguza sababu ya tukio la kifo cha Mwandishi wa Habari Mkoani Iringa.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea SMT kuunda Tume ya Uchunguzi kwa kifo kilichotokea Iringa na ikakataa kuunda Tume mwaka 2001 yalipotokea mauaji makubwa Zanzibar.

(b) Katika vurugu zilizotokea hivi karibuni ambazo zilihusishwa na Jumuiya ya Mihadhara ya Kiislamu na Polisi kwa upande mwingine ambapo nyumba za Ibada (Misikiti na Makanisa) ziliathirika, viongozi wa Jumuiya ya Mihadhara ya Kiislamu walitoa wito wa kuundwa kwa Tume ya Kuchunguza kadhia hii mara kadhaa, lakini SMZ haikuchukua hatua Je ni kwa sababu gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, naomba kumjibu Mheshimiwa ndugu yangu mpenzi, swali lake Nam. 31 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliunda Tume ya Uchunguzi kwa kifo cha Mwandishi wa Habari Marehemu Daudi Mwangosi kilichotokea huko Iringa. Pia ikumbukwe kwamba serikali iliunda Tume kwa ajili ya kuchunguza kadhia iliotokea Zanzibar mwaka 2001 hapo Januari 26 na 27. Tume ambayo iliongozwa na Bregedia Jenerali Mstaafu Hashim Mbita. Nia ya Tume hiyo ilikuwa ni kujua kadhia

nzima iliotokea na kutafuta njia ya kuzuia vitendo kama hivyo visitokee tena katika nchi yetu.

(b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa za Jeshi la Polisi naomba ieleweke kwamba vurugu zilizotokea hazikufanywa na pande mbili kwa maana ya wafanya vurugu kwa upande mmoja na Polisi kwa upande mwengine. Polisi ilifanya kazi zao kwa mujibu wa Sheria kwa nia ya kutuliza vurugu hizo na hatimae kufanikiwa kurejesha hali ya amani katika nchi yetu. Kwa hiyo, katika hali kama hii hakukuwa na haja ya kuunda Tume ya Uchunguzi wakati Jeshi la Polisi linatekeleza wajibu wake Kisheria. Kilichofanyika ni upelelezi wa kesi zinazowahusu watuhumiwa wa vurugu hizo na baadhi yao wamekamatwa na mashauri yao yanaendelea Mahkamani huku wengine wakiendelea kutafutwa na wakipatikana watafikishwa katika mikono ya Sheria na Sheria itachukua mkondo wake.

Mhe. Spika, naomba nitoe wito kwa wananchi kufuata sheria za nchi na kukataa vitendo vyovyote vile vinavyosababisha fujo na kuvuruga amani ya nchi yetu. Kwani vitendo hivyo licha ya kuathiri uchumi wa nchi huathiri sana hali ya maisha ya watu wetu ya kila siku. Hivyo Serikali haitomvumilia yeyote yule atakayevunja Sheria za nchi na kusababisha hali ya amani na utulivu kutoweka.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na kwa sababu ameonesha kwamba Ofisi yake ina kumbukumbu muhimu za zamani kwanza naomba nimpongeze kwa hilo. Lakini naomba anijubu swali dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kutokana na kwamba hivi karibuni viongozi wetu wa kidini wamekuwa wakipata majeraha, yalianza Sheikh Soraga kujeruhiwa na hivi karibuni Padri akajeruhiwa. Hatuoni kwamba kuna umuhimu wa polisi kuunda Tume kwa wale wanaowajeruhi viongozi wetu wa kidini ili kuweka imani kwa Wazanzibari ambao wote kwa pande mbili Waislamu na Wakristo hawapendi matendo haya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hija kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa sababu kazi ya uchunguzi inaendelea na jeshi la polisi wameanza kupata vielelezo vinavyosaidia katika kufikia mwisho wa hatua ya uchunguzi huo. Kwa hivyo ni vyema kwa sasa tukaliachia jeshi la polisi kufanya uchunguzi huu na baadae kupata taarifa rasmi juu ya yaliyotokea.

Ni kweli yaliyotokea yanatia hofu na wasi wasi kwa wananchi. Lakini nataka niwahakikishie wananchi wote wa Zanzibar kwamba vikosi vya ulinzi na usalama vitaendelea kufanya wajibu wake kuhakikisha kwamba wale wote wanaofanya vitendo viovu hasa vya hujuma, wanachukuliwa hatua zifaazo kwa kufuata mkondo wa sheria.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwanza nijipongeze kwa kufika mwaka 2013. Naomba kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri, pamoja na majibu yako mazuri Mhe. Waziri huoni kwamba sasa iko haja ya kuwachukua askari wetu kuwapeleka nchi za nje ili wakapate taaluma zaidi ya uchunguzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, siku zote kujifunza zaidi ni jambo la busara na ni jambo la maana sana. Hatua zinachukuliwa pale ambapo uwezo wa nchi unaruhusu kuwaendeleza zaidi kimafunzo askari wetu. Hatua hizo zinafanyika.

Ushauri wa Mhe. Mshimba tunaupokea na kwa sasa tutaendelea kuvitumia vyuo vyetu vya ndani pamoja na vya nje ya nchi, ili kuliimarisha jeshi letu liweze kuwa na uwezo mkubwa sana katika kufanya shughuli za uchunguzi ili uchunguzi ufanyike kwa haraka na ulio na uwadilifu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwanza nataka nimuunge mkono kwamba nchi hii inasheria na tunapaswa kuzifuata.

Mhe. Spika, mimi niliwahi kuwa polisi na nilipokuwa nafanya mafunzo ya polisi nilisomeshwa somo moja linaitwa *Criminal Procedure Act.* Katika somo hilo unaelekezwa mle ukitaka ku – *arrest* kama kosa limetokea basi unakwenda kwa yule unaetaka kumu-*arrest* baada ya uchunguzi unamsomea kifungu cha sheria. Bwana mimi ni Askari Polisi mwenye namba kadha kadha kadhaa, tunakutuhumu umefanya kosa kadhaa kwa mujibu wa sheria na kwa hivyo mpaka sasa hivi uko chini ya ulinzi. Lakini bahati mbaya sana askari wetu wamekuwa hawaifuati sheria na wanaweza wakaingia tu wakakuta kundi la watu wamekaa tu, wakaanza kuwatandika virungu bila ya kujua chochote na hatimaye hawamchukui hata mtu mmoja.

Swali lipo hapa, Mhe. Waziri haoni kwamba askari wetu kufanya hivi, wasifuate sheria na mafunzo waliyoyapata wakati wanasomeshwa, huku ni kuvunja sheria ya nchi na ni kulidhalilisha sana jeshi la polisi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuwa huyu ni maulana kujibu kwake ni lazima uwe na tahadhari kubwa sana.

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba sheria na taratibu za nchi zinapaswa kufuatwa na watu wote, wakiwemo jeshi la Polisi, vikosi vya SMZ na kila muhusika katika nchi hii. Kwa hivyo ni wajibu wa kila mmoja kufuata sheria. Pale sheria inapovunjwa hayupo aliyejuu ya sheria zinapaswa hatua za sheria kuchukuliwa dhidi yake. Kwa hivyo si askari wala raia, atakaevunja sheria atakaevumiliwa aendelee kuvunja sheria ni lazima ifate mkondo wake.
Nakubaliana kuna wakati jeshi letu linalofanya shughuli hizi pengine kwa dharura wanazo taratibu zao. Lakini sheria ni lazima zifuate mkondo wake. Nashukuru sana Mhe. Spika.

Nam. 12

Marekebisho ya Kumi ya Katiba

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:

Katika marekebisho ya Katiba kipindi kilichopita, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa pamoja walipitisha kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais wote kwa pamoja watakuwa ndio Washauri Wakuu wa Rais.

Katika Katiba ya Zanzibar ya 1984 Toleo la 2010 Kifungu 39(5) na (7) ukurasa wa 28 maelezo hayakubainisha ipasavyo. Nahisi kunahitaji marekebisho.

(a) Je, maelezo haya yamejitokeza kimakosa.

(b) Kama ni kimakosa, marekebisho ya Katiba huwa yanakuwaje.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru wewe, lakini zaidi naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuukaribisha mwaka mpya. Naomba niwatakieni kheri Wajumbe wote na Wafanyakazi wote wa Baraza katika mwaka huu wa 2013.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 sura ya nne, sehemu ya pili, kifungu cha 39(1) kinaeleza kuwepo kwa Makamo wawili wa Rais, kifungu hicho kinasomeka ifuatavyo:-

Kifungu cha 39(1) kutakuwa na Makamo wawili wa Rais ambao watajulikana kama Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais.

Kifungu cha 39(5) kinaeleza kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais atakuwa ni Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na atafanya kazi zote atakazopangiwa na Rais.

Kifungu cha 39(7) cha Katiba kinaeleza pia kwamba Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ni Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na pia atakuwa ndiye Kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

Hivyo, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeweka wazi kuwa Makamo wa Rais watakuwa Washauri Wakuu wa Rais kwa mujibu wa vifungu hivyo vya Katiba na hakuna makosa yoyote yale. Ila ijulikane tu kifungu 3(7) kinampa uwezo Makamo wa Rais mbali na kuwa ni Mshauri Mkuu wa Rais, basi pia ndiye atakayekuwa Kiongozi wa Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

(b) Kifungu cha 80 cha Katiba kinaeleza utaratibu wa kubadilisha kifungu chochote cha Katiba.

Ili kifungu cha Katiba kiweze kubadilishwa, mswada wa kubadilisha Katiba unatakiwa kuungwa mkono kwa mara ya kwanza na mara ya pili katika kusomwa kwa kura si chini ya theluthi mbili ya kura zote za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kama kinavyoelezea katika kifungu cha 80 (2).

Utaratibu wa kubadilisha Katiba unatofautiana kwani kuna vifungu vya Katiba ambavyo vinahitaji kupigiwa kura ya maoni ya wananchi na baadhi ya vifungu kuwa havihitaji kura hiyo. Kwa mfano, (80) (a) cha Katiba kinatoa maelekezo ya vile vifungu ambavyo kubadilishwa kwake ni lazima kuwe na kura ya maoni na ambavyo si lazima kuwa na kura ya maoni.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu yake mazuri ambayo yamegusa Katiba moja kwa moja.

Mhe. Spika, swali langu lilikua linatokana na kazi tuliyoifanya ya kubadilisha katiba kabla ya kura ya maoni na tulipitisha kwa pamoja kuwa Waheshimiwa hawa wawili yaani Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais wote wawe ni washauri wakuu wa Rais. Na imeandikwa hivyo na Katiba lakini katika hali ambayo mimi kwa ufahamu wangu inaonesha kuwa kuna mmoja kapewa uwezo zaidi na kuna mmoja kapunguziwa kama ifuatavyo:

Tukiangalia kifungu cha 39(5) ukurasa wa 28 kinasomeka hivi:-

> "Makamo wa Kwanza wa Rais ni Mshauri Mkuu wa Rais" na halafu kaendelea na mambo mengine

Kifungu cha 39 (7) ukurasa wa 28 kinasema:-

> "Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ndiye Mshauri Mkuu wa Rais.

Sasa ikiwa Makamo wa Kwanza wa Rais atakuwa ni Mshauri Mkuu wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ndiye Mshauri Mkuu wa Rais. Uhalisia unaonesha kuwa huyu Makamo wa Kwanza si mshauri tena.

Kwa hivyo Mheshimiwa kama tulivyokuwa tumepitisha kuwa hawa wawe na nguvu sawa za kumsaidia Mhe. Rais katika ushauri hii **'**ni' ndio inayotofautisha malengo yetu. Ama wote iandikwe ndiye au wote litumike neno **'**ni' au maelezo mengine yoyote ambayo yanatuonesha kuwa kweli hawa ni washauri wa Rais. Kwa hivyo kutokana na kuwa sikuridhika na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa maneno haya mawili ya kutumiwa **'ni'** na **'ndiye'** atanieleza vipi kisheria mpaka nione kuwa ile dhima ya kuwa wote ni washauri wakuu wa Rais imepatikana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, sote ni Waswahili na Kiswahili chetu ni *rich* katika lugha. Sasa ukisema kitu kwamba kalamu hii ni na ukisema kalamu hii itakuwa *all most*

lugha ni sawa sawa. Kwa hivyo unavyosema Makamo wa Kwanza wa Rais ni Mshauri Mkuu na Makamo wa Pili wa Rais ndiye Mshauri Mkuu, mimi nahisi kwamba hakuna tofauti yoyote ile. Yote ni sawa sawa kama ndiye mshauri mkuu kama ni mshauri mkuu ni utumiaji wa lugha tu katika uandishi.

Ni kweli labda niseme tu katika uandishi labda pengine tungeandika zote ama tukitumia iwe **ni** au zote iwe **ndiye**. Lakini zote zina maana tofauti, kwa maelezo hayo mara nyengine *In shaa Allah* tutakapofanya marekebisho mambo kama haya ya kutumia neno moja kwa maana mbili tutaweza kulirekebisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba na mimi nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuushuhudia mwaka huu mpya wa 2013 na nitumie fursa hii kukutakia wewe Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wa Zanzibar kheri ya mwaka mpya, inshaallah mwaka mpya uwe wa kheri, barka, neema na kuzidisha masikilizano katika nchi yetu pamoja na amani iliyopo.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kuhusiana na suala hili kama ifuatavyo:

Swali ukilitazama na maelezo ya Mjumbe linaonekana kwamba hata baadhi yetu Wajumbe bado uelewa wetu katika masuala ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na marekebisho tuliyoyafanya inawezekana ukawa unatofautiana. Mara nyingi katika Baraza hili Mhe. Spika, Wajumbe na hasa nataka kumpa heshima maalum mjumbe Mhe. Asha Bakari Makame amekuwa akikumbusha mara kwa mara kwamba kuna haja ya serikali sasa kufanya kazi ya kutoa elimu kuanzia kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusiana na mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hasa ukizingatia kwamba Baraza hili Mhe. Spika, liliunda Kamati ambayo ilikwenda kufanya ziara nje ya nchi kujifunza juu ya mifumo mengine ya kufanya kazi. Sasa mara nyingi serikali imeahidi kwamba itatoa mafunzo hayo lakini mpaka hii leo tunakaribia nusu ya kipindi cha Umoja wa Kitaifa mafunzo hayo hayatolewi. Kwa nini serikali haitekelezi ahadi yake ile ya kutoa mafunzo. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba, na Sheria: Mhe. Spika, swali lililoulizwa lilikuwa swali la Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais si swali la Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo hili ni swali lilioko nje ya swali hili. Nakubali kwamba ni swali muhimu na ningelimuomba Mhe. Mjumbe alilete swali hilo ili tuweze kumjibu hasa utaratibu ambao tunataka kuufanya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nilikuwa naomba utusaidie tu Mhe. Spika, muongozo kwamba je anayekataa swali ni anayeulizwa au ni Mhe. Spika, akiwa katika kiti kinachoongoza Baraza. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ninafikiri Mhe. Waziri alikuwa anamkumbusha Spika, kwamba hilo swali liko nje ya mstari na mimi nakubali hivyo kwamba liko nje ya swali mama. Hivyo nimuombe basi Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili afanye utaratibu kuuliza swali la msingi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri kutokana na hali ambayo inayojitokeza hivi sasa iko haja hasa Mheshimiwa Wajumbe wako wote ukatupa semina ikaeleweka hasa hii katiba kutokana na shughuli zilizotajwa marais wetu wawili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi ninaamini sana kwamba kuna haja ya Wajumbe wetu kuwaelimisha kwenye Katiba. Swali hili nitalipeleka Mhe. Spika, kama atakuwa na *funds* za kutosha, sisi Wizara yetu iko tayari kutoa elimu hiyo kwa Wawakilishi wako.

Mhe. Spika: Ninakushukuru Mheshimiwa.

Nam. 36

Ukosefu wa *Pathologist*

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nichukue fursa hii kwamba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha asubuhi hii kufika hapa nikiwa katika hali ya uzima. Pia nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutukutanisha sote katika mwaka huu wa 2013 tumuombe Mwenyezi Mungu atupe khatima njema. Baada ya hapo ninamuomba Mhe. Waziri anijibu swali langu namba 36.

Kwa kuwa baadhi ya kesi zinahitaji daktari mwenye fani ya *pathologist*, na kwa kuwa Pemba nzima haina bingwa au mtaalamu huyu jambo ambalo hupelekea baadhi ya kesi kukosa ushahidi wa kitaalamu na hushindwa kuthibitishwa kosa Mahkamani.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako inaliangaliaje suala la kupatiwa mtaalamu huyo, pamoja na vifaa vya kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kheri ya mwaka mpya kwako na kheri ya mwaka mpya kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa fursa hii tena kuwajibu Wawakilishi na kwa kuanzia naomba kumjibu Mhe. Shadya Mohammed Suleiman swali lake nambari 16, Mjumbe wa Wanawake Kusini Pemba CCM swali lake kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, *Pathologist* ni wataalamu ambao wapo wachache ulimwenguni na huwa wanakuwepo kwenye hospitali za rufaa.

Wataalamu hao katika jumla ya kazi zao, moja wapo ni kutoa ushahidi kwa kesi za jinai zenye utata.

Kazi hiyo anaweza akaifanya mtaalamu mmoja peke yake, lakini pia anaweza kutafuta ushauri kwa mtaalamu wa aina hiyo wakafanya kazi pamoja ili kujiridhisha kwamba anatoa ushahidi ulio sahihi.

Kwa hiyo akihitaji msaada huo anaweza kuwasiliana na mtaalamu mwenziwe popote pale alipo.

Mhe. Spika, kwa kuwa hospitali ya Rufaa kwa Zanzibar ni Mnazi Mmoja kwa hiyo hapo ndipo anapostahiki kuwepo.
Ikiwa Pemba kuna kesi yenye kuhitaji uamuzi wa mtaalamu huyo kuna njia mbili za kufanya:-

1. Wafanyakazi wa huko wawasiliane na daktari mtaalamu wa hospitali ya Mnazi Mmoja na atatoa maelekezo au watamwita kama kuna ulazima wa yeye kwenda.

2. Kama kinachochunguzwa kinahitaji maabara basi itachukuliwa sampuli na kutumwa Mnazi Mmoja kwa uchunguzi na atapelekewa jibu au atakwenda kutoa ushahidi akihitajika.

Lakini kwa suala la kutoa ushahidi kwa mambo ya kawaida mtaalam wa afya wa ngazi yoyote anaruhusika na ana mamlaka ya kutoa ushahidi Mahakamani kwa kesi nyengine zote zinazoendeshwa na si lazima *Pathologist.*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa hai, wazima katika mwaka huu wa 2013 huu si ujanja wetu wala nguvu zetu wala uwezo wetu, kwa hii neema kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na tunatakiwa tuseme alhamdulillahi. Wangapi sasa hivi wanakata roho, wengine wanazaliwa, wengine wanavua. Baada ya hapo naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa kazi nzito ya muda mfupi aliyoifanya katika jimbo lake, sisi sote ni mashahidi bila ya kujali itikadi ya chama ameweka usafiri hivi sasa Darajani pale kuhudumia basi kwa fedha zake, kwa gharama chungunzima na sisi tunaomba tuige mfano wake yeye Mheshimiwa.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa mshangao mkubwa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi aliloulizwa alisema hospitali ya Mnazimmoja imeshafika hospitali ya rufaa, serikali imekuwa na kilio hicho kwa muda mrefu je atueleze hospitali hiyo imeshakuwa hospitali ya rufaa.

Pili, ni wataalam wangapi aliowataja hapo hospitali ya Mnazimmoja waliokuwepo, mimi ninajua hospitali ya Mnazimmoja mpaka hivi sasa haijafika hospitali ya rufaa hebu atueleze.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sijafahamu swali.

Mhe. Spika: Rudia swali bila ya maelezo marefu ya mwanzo rudia swali moja kwa moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, alipokuwa akijibu swali Mhe. Naibu Waziri alitaja hospitali ya Mnazimmoja kuwa hospitali ya rufaa, nataka kumuuliza tayari imeshafika hospitali ya rufaa hiyo ili wananchi wapate kuelewa hospitali ya Mnazimmoja sasa hivi ni hospitali ya rufaa.

Pili alipokuwa akijibu hawa wataalamu Pemba hawapo aweze kutwambia ni wataalamu wangapi aliokuwa nao katika hospitali hii ya Mnazimmoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, anasema nilipokuwa nikijibu swali langu nilisema kwamba Mnazimmoja ni hospitali ya rufaa imefikia wapi? Ninachoweza kujibu kwamba katika maelekezo tuliyopewa na ilani ya uchaguzi wa CCM mwaka 2010 ni kwamba hospitali ya Mnazimmoja iwe hospitali ya rufaa. Na katika marekebisho ya kuifanya hospitali ya rufaa kuna wataalamu ambao wanatakiwa kuwepo akiwemo mmoja kwamba ni *Pathologist*. Kwa hivyo kwa maandalizi hayo ninaweza nikasema kwamba tunaelekea kuwa katika hospitali ya rufaa. Lakini sio tukisema hospitali ya rufaa inakuwa kama vile kipeto wa kipeto hapana. Kuna mambo yanatakiwa kufanywa, *process* zifanywe tufikie huko. Tunaelekea kuwa hospitali ya rufaa kwa sababu tumeshaitangaza kwamba Mnazimmoja itakuwa hospitali ya rufaa.

Swali la Pemba, Pemba ni nchi moja Zanzibar, kwa hivyo hospitali ya rufaa iliopo ni moja tu mengine ambayo yanastahiki kuwepo Pemba yatakuwepo kwa utaratibu wetu kama Wizara ya Afya inavyoyapanga. Tuna *stage* zetu na tuna taratibu zetu za Wizara, kama anataka nichukue muda aje ofisini kwangu nitamfahamisha ipasavyo ili afahamu kwa sababu hapa ninaweza nikachukua muda mrefu wala haitostahiki. Njoo ofisini tuzungumze nitakufahamisha kimoja baada ya chengine baadae utafahamu na hutoniuliza maswali ambayo kwa kweli yatakuwa hayaendani na masuala haya.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza swali kama hivi ifuatavyo.

Katika swali la msingi lililoulizwa limezungumzia kukosekana kwa mtaalamu huyu wa *Pathologist* ambapo imepelekea kesi kukosa ushahidi wa kitaalamu na kushindwa kuthibitishwa mahakamani. Nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri je, swali hili ni kweli linatokea Kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama ulivyosema swali limeulizwa hivyo, lakini sisi katika Wizara hatujawahi kupata malalamiko hayo kwa hivyo siwezi kusema kuwa ni kweli au si kweli.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri huoni tabu kuiita ile hospitali ya rufaa wakati hivi sasa hata ile dawa ya ganzi ya operesheni haipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sioni tabu na nitaendelea kuiita hospitali ya rufaa kwa sababu tunaelekea kuifanya hospitali ya rufaa na hicho unachosema kimekosekana si kweli, kipo njoo nitakuonesha.

Nam. 1

Ujenzi wa Barabara Msitu wa Ngezi

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam.18

Vituo vya Kununulia Karafuu

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Katika ununuzi wa karafuu msimu uliopita, wizara ililazimika kutumia vituo vya muda ambavyo pia viliuza karafuu nyingi kwa Wizara.

a) Je, Wizara imejipangia vipi kuongeza vituo vipya vya kudumu katika msimu unaofuata.

b) Wizara imeweka mpango gani wa kuviimarisha vituo vikongwe ili vibakie katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, na mimi kama walivyotangulia wenzangu kwa ruhusa yako naomba niwatakie Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wewe Mhe. Spika, kila la kheri katika mwaka huu mpya wa 2013.

Sasa kwa ruhusa yako Mhe. Spika, napenda nimjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe swali lake nambari 18 lenye vifungu (a), na (b) linalohusiana na uimarishaji wa vituo vya kununulia karafuu kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa sasa serikali inavyo vituo 36; vituo hivyo hufunguliwa kulingana na hali ya uzalishaji wa karafuu katika msimu husika. Lakini serikali Mhe. Spika, haitosita kuongeza vituo vipya ikiwa kutakuwa kuna haja ya kufanya hivyo ili kuwarahisishia wakulima wa karafuu kuuza karafuu zao.

(b) Mhe. Spika, kwa upande wa kuviimarisha vituo vya kununulia karafuu ili vibakie katika hali nzuri, Wizara kupitia serikali baada ya kufanya tathmini ya vituo hivyo imeandaa mkakati maalum wa kuviimarisha vituo vitano kwa mwaka. Na katika kipindi hiki cha fedha cha mwaka 2012/2013 serikali imeviimarisha vituo vitano vifuatavyo:-

Kituo cha Mkanyageni
Kituo cha Raha
Kituo cha Mzambarao Takau
Kituo cha Kinyasini na
Kituo cha Chonga.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri yanayotoka kwa Mhe. Naibu Waziri na hasa kuona kituo cha Mzambarauni ni kimoja katika vituo vitakavyofanyiwa matengenezo. Mhe. Spika, katika msimu wa karafuu uliopita Shirika lilijitahidi sana kuongeza vituo ili kuondoa usumbufu kwa wananchi katika ununuzi wa karafuu, ikabidi vituo vyengine viwe ni vya muda vya kuazima majengo ya watu.

Mhe. Spika, lakini kabla ya karafuu kumalizika kutokana na hali shirika ilivyoona iliahidi kwa baadhi ya vituo walivyoazima watajenga vituo vya kudumu ikiwa ni kijiji cha Chanjaani katika Jimbo la Mtambwe na kijiji cha Bwagamoyo ambapo ilibidi tutoe Kituo chetu cha Afya tunachojenga, sehemu hizi mbili watajenga vituo kutokana na hali nzuri ya manunuzi waliyoiona na mpaka leo hapajafanywa lolote. Je, haoni msimu huu ujao ambao utakuwa ni mkubwa wananchi kufuatilia vituo vya mbali pengine na kusababisha ukosefu wa karafuu zetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, wakati nikijibu swali la msingi nimesema kwamba serikali haitosita kuongeza vituo pale itapoona ipo haja ya kufanya hivyo. Naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wanaouliza maswali yao Mhe. Spika, wawe makini kwenye kusikiliza majibu.

Mpaka sasa hivi katika manunuzi ya karafuu katika kijiji cha Mtambwe bado wizara kupitia serikali hatujaona haja ya kuongeza lakini tumeona iko haja ya kuimarisha vituo vilivyokuwepo na hiyo ndiyo kazi tuliyoifanya katika kipindi hicho cha mwaka wa fedha Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Biashara.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu la msingi la Mhe. Waziri alivitaja vituo ambavyo vimefanyiwa matengenezo je vituo hivyo viko maeneo gani. Pili ni gharama gani zilizotumika kufanyia matengenezo vituo hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, katika kuvifanyia matengenezo vituo, Wizara imezingatia ku-*cover* maeneo yote ya Pemba na katika kutekeleza hilo kituo cha Mkanyageni kinatoka Wilaya ya Mkoani, Kituo cha Chonga kinatoka Wilaya ya Chake Chake. Wilaya ya Wete kwa kuwa ndiko kunakotoka karafuu nyingi tumefanyia marekebisha vituo viwili ambavyo ni kituo cha Mzambarau Takau lakini Micheweni Mhe. Spika, ndipo kwenye kituo cha Kinyasini kwa ajili ya kununulia karafuu.

Gharama zilizotumika katika matengenezo ya vituo vitano hivi Mhe. Spika, ni milioni mia mbili na mbili laki tano ishirini na saba na mia tatu na thamanini.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali ina azma nzuri ya kuwaondoshea usumbufu wananchi wake katika kijiji cha Ngomeni linapatikana zao la karafuu kwa wingi, na kwa kuonekana hilo Serikali ya Mkoa iliamua kuwatengenezea barabara. Je serikali ina mpango gani wa kuwatengenezea njia yao hiyo ili wananchi hao wafaidike na kituo chao pale ili waondokane na usumbufu wa kufuata kituo maeneo ya mbali. Serikali ina mpango gani wa kuwahudumia kituo chao kile ili kiendelee kuwepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa hali halisi barabara nyingi za ndani kisiwani Pemba haziridhishi na hili Wizara tumeliona na mimi binafsi nimekwenda kutembelea vituo hivi tumeona hali halisi ya barabara zilivyo na tumekuwa tukiwasiliana na Wizara husika kwa kuzitengeneza njia hizi ili kuwapunguzia masafa au kuwarahisishia wakulima wa karafuu katika kupeleka karafuu vituoni. Na muelekeo ni kwamba Mhe. Spika, inaonesha kwamba suala hili limepokelewa vizuri basi zitafanyiwa matengenezo kwa kadri ya fedha zitakavyoruhusu.

Nam. 42

Vyanzo vya maji kwa wakulima wadogo wadogo

Mhe. Ussi Jecha Simai - Aliuliza:-

Wakulima wadogo wadogo wa vijiji vya Chaani, Gamba na Moga ni wakulima wanaotegemea mvua kwa ajili ya mazao yao. Kutokana na kukosa vyanzo vya maji ya uhakika mara nyingi mazao yao hasa yale ya mboga mboga hukauka kwa jua.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wakulima vyanzo mbadala vya maji kwa ajili ya mazao yao.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Spika**,** napenda kuchukua fursa hii kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake namba 42 kama ifuatavyo:- Uwezo wa vianzio vya maji katika maeneo mengi yaliyotajwa umepungua kutokana na kazi tofauti zinazofanywa na Binaadamu katika maeneo hayo ambapo husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na uoto wa asili hasa ukataji mkubwa wa miti kwa ajili ya kujipatia nishati ya kuni pamoja na matumizi ya ardhi.

Mhe. Spika**,** Wizara inapenda kutoa ushauri ufuatao:-

- Jamii ielimishwe juu ya changamoto zilizopo na hivyo kila mmoja ashiriki kuzuia uharibifu wa mazingira;

- Maeneo ya vyanzo vya maji yote yapandwe miti na yaendelezwe. Hata hivyo vyanzo mbadala vya maji ni kuchimba visima vidogo na vikubwa katika kupata maji ya kumwagilia. Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kutekeleza mpango wa Umwagiliaji Maji imeandaa mpango wa kuendeleza maeneo ya kilimo yawe ya umwagiliaji maji na hivi sasa inaandaa programu na miradi midogo midogo kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri yenye kuleta ufanisi. Mhe. Naibu Waziri hivi karibuni katika mabonde yangu mawili kati ya Pangeni na Kilombero walitembelewa na wataalamu kutoka Marekani, lengo ni kuchimba visima ili watu walime mpunga wa kumwagilia maji.

Je, Mhe. Naibu Waziri hatua hiyo imefikia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kweli ilitembelwa na wafadhili hao, kwa kuwa hivi sasa kuna mradi wa *Exim Bank* mradi ambao wizara tayari imeshapata mfadhili na hivi sasa maombi ya ujenzi huo wa miundombinu ya umwagiliaji maji tayari imeshafunguliwa. Wizara inasubiri ripoti ya utekelezaji ripoti ya fedha kutoka kwa wakandarasi waliopitishwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mwisho wa mwaka 2012 mvua imenyesha vizuri na zenye rutba ya kupanda mazao. Je, Mhe. Naibu Waziri utawahamasishaje wananchi ili wazitumie mvua hizi na pia kuwapatia wataalamu na kuwapatia mbegu zilizo bora ili kuendeleza kilimo chao hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ni kweli suala hili la uhamasishaji wizara yangu inalifanya vizuri na pia uhamasishaji huu nadhani Mhe. Mwakilishi tuwe pamoja katika kuwahamasisha wananchi katika shughuli hizi za kupanda kilimo hichi.

Mhe. Spika, wananchi ni watu ambao wizara yangu inafanya kazi ya kuhamasisha juu ya vilimo vya kutumia mvua, lakini hata hivyo nawaomba Wawakilishi kupitia majimbo yetu na sisi tushiriki katika kuhamasisha wakulima wetu. Kwa sababu wizara inachukua sehemu moja ya kuhamasisha na sisi wawakilishi tuna sehemu nyengine kama ni wawakilishi wa wananchi kufanya kazi hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niongezee majibu ya nyongeza. Mhe. Spika, hivi sasa serikali imeweka utaratibu maalum ili kuwahamasisha wakulima wetu kushiriki zaidi katika shughuli za kilimo ikiwemo kutoa ruzuku kwa mbegu, dawa na hata kusaidia katika vifaa mbali mbali vya kilimo. Pia imeanzisha mpango maalum wa mashamba darasa ili kuwaelimisha wakulima katika maeneo yao kwa nia ya kuhamasisha kuwawezesha wakulima kutoa kilimo kilicho bora na chenye tija katika nchi yetu. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 51

Msaada wa Serikali kwa Wanafunzi

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwasaidia wanafunzi wa Zanzibar ili kuwawezesha kumudu gharama za masomo kwa njia ya mkopo, lakini hata hivyo kiasi hicho kinalalamikiwa kuwa ni kidogo sana.

(a) Wanafunzi hao wa elimu ya juu wanapaswa kulipwa kiasi gani na wanapatiwa mikopo ya kiasi gani kwa mwaka kwa kila mwanafunzi.

(b) Je, serikali haioni kuwa kutoa kiasi hicho kidogo cha fedha hailengi kuwasaidia kwa dhati vijana hao wa wakwezi na wakulima.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza niungane na wenzangu kukutakia wewe kheri za mwaka mpya pamoja na Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu Mwenyezi Mungu atujaalie mwaka huu uwe wa kheri na baraka katika nchi yetu na atuzidishie imani na mapenzi ya kweli.

Mhe. Spika, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ina majukumu na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Zanzibar wanaochaguliwa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu vya ndani na nje ya nchi. Idadi ya wanafunzi wanaomba mikopo inaongezeka kila mwaka kutokana na wanafunzi wengi kufaulu masomo yao na kupata sifa za kuwawezesha kujiunga na masomo mbali mbali. Kutokana na wingi wa wanafunzi wanaoomba mikopo na kulingana na bajeti ya mikopo tuliyonayo kiwango cha fedha ya mikopo kinachaotolewa hakitoshi mahitaji yote kwa wanafunzi.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi ilitengewa fedha ya bajeti ya Shilingi Billioni 4 na idadi ya maombi ya mikopo ilikuwa ni 1,850 ambapo ni wanafunzi 209 tu ndio waliopatiwa mikopo sawa na asilimia 11.3 ya maombi yote. Katika mwaka 2012/2013, Bodi imetengewa bajeti ya Shilingi Billioni 8 na maombi ya mikopo yalikuwa ni 3,020 na waliopatiwa mikopo hiyo ni wanafunzi 800 tu ndio waliopatiwa sawa na asilimia 26.5 ya maombi yote.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Kiwango cha mikopo kinachotolewa kwa mwanafunzi kinatofautiana kutokana na gharama za ada kutofautiana baina ya chuo kimoja na chengine na baina ya somo moja na jengine. Mara nyingi gharama za ada ya masomo ya sanaa ni za chini ukilinganisha na masomo ya sayansi, ufundi na udaktari. Kwa wanafunzi wanaosoma vyuo vya Tanzania Bara Bodi ya Mikopo inagharamia malipo ya ada malazi na gharama za kufanya utafiti. Kwa vyuo vya Zanzibar wanafunzi wanaolipiwa gharama za ada na utafiti na kiasi cha shilingi 250,000 kwa kugharamia malazi au usafiri.

Mhe. Spika, fedha za malazi kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya Zanzibar zimeanza kutolewa kuanzia mwaka huu kwa lengo la kuwahamasisha wanafunzi wengi zaidi kusoma vyuo vya ndani kwa nia ya kupunguza gharama hasa kwa masomo yanayopatikana hapa hapa nchini. Kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya nje ya nchi, Bodi ya Mikopo inawalipia gharama za ada, malazi, chakula na usafiri. Kwa wastani ya mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya Zanzibar ni Shilingi 2, 000,000/= kwa mwaka, kwa wanaosoma Tanzania Bara ni Shilingi 3, 000,000/= kwa mwaka na wanaosoma nje ya nchi katika nchi za China na Malaysia ni Shilingi 12, 000,000/= kwa mwaka.

(b) Serikali inatambua kuwa kiwango cha fedha cha mkopo kinachotolewa hakitoshelezi mahitaji kwa mwanafunzi, mzazi au mlezi wana wajibu wa kugharimia mahitaji mengine

kwa watoto wao. Kwa kufanya hivyo Bodi inaweza kuwalipia waombaji wengi zaidi kwa mwaka. Pindipo kama Bodi ya Mikopo itagharamia kwa wanafunzi wote mahitaji yote, ni dhahiri kwamba wanafunzi watakaopata mikopo watakuwa ni wachache sana. Hata hivyo, Bodi inakusuidia kufanyia mapitio viwango vya fedha za mkopo zinavyotolewa kwa kadiri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Omar Ali shehe: Mhe. Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kiwango kinachotolewa kwa wanafunzi wetu kutoka Bodi ya Mikopo ni kidogo sana kitu kinachopelekea wengine kupata na wengine wasipate. Vile vile suala linalopelekea hali kugaiwa matabaka katika nchi yetu, kwamba kuna wengine wanaosoma na wengine wasioweza kusoma kitu ambacho ni kinyume kabisa na malengo ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Mapinduzi yetu yalikuwa na lengo la kuwaweka wananchi wote katika hali ya usawa. Sasa kwa utaratibu huu na tabia hii serikali ina mpango gani m-badala utakaowafanya wanafunzi hawa ama wapate wote au wakose wote ili kuona kwamba wananchi wetu wote wanakuwa katika hali ya usawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama ambavyo nimezungumza kwenye jibu mama kuwa mahitaji ya waombaji ni mengi, lakini uwezo wa bodi kuwasomesha watoto ni kidogo. Kwa mfano, nilisema ndani ya mwaka 2011/2012 bodi ilitengewa shilingi bilioni nne wakati Mheshimiwa waombaji 1,850 tulihitaji shilingi bilioni 13 na zaidi ili tuweze kuwasomesha wanafunzi wote.

Lakini vile vile nikazungumza kwamba kwa mwaka huu tulitengewa shilingi bilioni nane na Mhe. Mwakilishi ni shahidi walipitisha katika bajeti hapa, wanafunzi ambao waliomba ni 3,020. Kwa hivyo, uwezo wetu wa bodi ni wanafunzi 800 tu kuweza kuwasomesha kwa hicho kiwango ambacho nilisema.

Mhe. Mjumbe serikali haina nia ya kuweka matabaka kwa wanafunzi, lakini tatizo linalotukwaza ni uwezo wa bodi, lakini kama alivyouliza kuwa bodi ina mpango gani wa kuweza kusaidia ili wanafunzi wengi wapate kusoma. Bodi inao mpango, kazi moja ya bodi ambayo tumeipa ni kutafuta vianzio mbali mbali ndani ya nchi na nje ya nchi ili kuhakikisha tunapata fedha zaidi za kuweza kuwasomesha watoto wetu ili yale malengo makuu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba kila mtoto wa Kizanzibari asome basi aweze kusoma.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ni hivi majuzi kuna taarifa kwamba wanafunzi katika kile Chuo cha KIU pale Dar es Salaam wanaotoka Zanzibar walizuiliwa kuingia madarasani kwa kutokulipiwa ada, sijui taarifa hizi ni kweli, kama ni kweli serikali imechukua hatua gani kwa tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli lakini kwa taarifa yake na kwa taarifa ya Baraza kuwa tayari wanafunzi hao wamelipiwa na sababu iliyopelekea wanafunzi hao wakafika kuzuiliwa kwanza bodi iliona ni bora tuwahudumie wale wanafunzi

ambao wako nje ya nchi ambapo kule hawana baba, mama, shangazi kwa kile ambacho Wizara ya Fedha imetutilia katika mfuko wetu.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri enzi za utawala wa Mhe. Abeid Amani Karume aliondoa usumbufu huu kutokana na kuwa wananchi wote wana haki sawa hasa ya kielimu. Sasa naomba kuuliza, kwa kuwa Mhe. Karume alifanya jitihada zake zote na akaitangaza elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi kuendelea. Je, wizara yako au serikali kwa ujumla ni sababu zipi zilizopelekea kuwalazimisha wananchi wachangie ili wapate elimu ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama Mheshimiwa alivyozungumza kuwa nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kutoa elimu bure kwa wote na Mheshimiwa ndivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inavyofanya inatoa elimu bure kwa wote. Hiki ambacho kinatakiwa kutolewa ni mchango sio kama ni malipo ya elimu ambacho hakifikii hata 0.5. Nakushukuru sana.

Nam. 10

Ahadi ya Serikali ya Kusambaza Maji

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Katika kipindi cha Bajeti cha mwaka 2011/2012, serikali iliahidi kusambaza maji katika vijiji tofauti Zanzibar vikiwemo vijiji vya Mtambwe Kaskazini Pemba.

(a) Ni sababu zipi zilizofanya ahadi hiyo isitekelezeke kwa vijiji vya Mtambwe Kaskazini.

(b) Zile sehemu nyengine ambazo hazikutajwa zimewekewa utaratibu gani wa uhakika usiokuwa wa kubahatisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu a na b kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli serikali iliahidi kusambaza maji katika vijiji vya Mtambwe Kaskazini katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Sababu kubwa ya kutokutekelezwa ahadi hiyo ni kutokana na wingi wa maeneo ambayo yalihitaji kupelekewa huduma hiyo katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ikilinganishwa na ukubwa wa bajeti.

(b) Mhe. Spika, vijiji vya Mtambwe, Kaskazini kama vile Chanjaani, Kiapaka, Kidundo Uchawi, Chekea, Mtambwe ambavyo havijafanikiwa kupata huduma hiyo ya maji ya bomba Mamlaka ya Maji inajiandaa kuviingiza vijiji hivyo katika bajeti ya mwaka huu wa fedha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu ahadi ya serikali kwa kupitia bajeti yake sio ya mwaka 2011/2012 tu, lakini hata mwaka 2010/2011 kitabu cha bajeti kilieleza hivyo hivyo. Kwa vile bajeti mbili zimepita na bado hatujafanyiwa lolote katika vijiji hivi vya Mtambwe Kaskazini na kutokana na shida ilivyo tayari wananchi kwa kutafuta mbinu wanazoweza wenyewe wamefanikiwa kupeleka maji katika kijiji cha Kiapaka na vile vile cha Mtambwe Mkuu.

Je, kwa vile wananchi wameshajitahidi hivyo, wizara hasa kwa maana ya wizara itawaisaidia vipi kuona kwamba vijiji hivyo vilivyobaki vitatu katika Mtambwe Kaskazini ikiwa ni Kidundo, Chekea na Kiapaka navyo vitapatiwa maji kulingana na juhudi ya wananchi waliokwishachukua kabla tena kwa haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza niwashukuru wananchi wa vijiji hivyo kwamba wako tayari kushirikiana na wizara yangu hususan katika kuliondoa suala hili la tatizo la maji. Kama wameshaanza kujiandaa kutafuta vifaa na mambo mengineyo basi nawaahidi kwamba wizara yangu itashirikiana nao na tutahakikisha tutaliondoa tatizo hilo katika vijiji hivyo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa vijiji vya Mtambwe kama vile Mpakanjia, Nyali na Uondwe na kadhalika huwa kunakuwa na mkusanyiko mkubwa wa kambi za kuchuma karafuu zao ambalo ni muhimu sana katika kupanua bajeti ya serikali ya nchi hii. Je, kuendelea kuviachia vijiji hivyo kukosa maji na hatimaye wachumaji karafuu kushindwa kwenda kupiga kambi zao pale kwa ajili ya kuliokoa zao la taifa si kuzoroteshwa uchumi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naamini kwamba yeye ni shahidi kuona serikali nini inafanya katika juhudi za kuliondoa tatizo hili la maji. Ni kweli kuna baadhi ya vijiji kama hivyo alivyovizungumza kwamba havijafikia huduma hiyo, lakini lengo la serikali vijiji vyote vya Zanzibar kuvipelekea huduma hiyo ya maji safi na salama. Kwa hivyo, vijiji hivyo ambavyo vina wachumaji wengi wa karafuu tutavipelekea huduma hiyo.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika bajeti ya mwaka 2011/2012 iliahidi kuchimba kisima katika kijiji changu cha Kinyasini pale katika Jimbo la Chaani. Lakini vile vile katika mwaka 2013 pia iliahidi suala hili, je, Mhe. Naibu Waziri wananchi wangu wa kijiji cha Bandamaji waendelee kuchimbiwa kisima katika kipindi hiki kinachomalizikia bajeti hii au serikali ama wizara yako bado iko mbioni na wananchi waendelee kusubiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji bado ina mpango wa kuchimba kisima katika eneo lake Mhe. Mwakilishi, nimhakikishie tu kwamba kisima hicho si muda mrefu wizara yangu itaelekea huko kupitia Mamlaka ya Maji kwa ajili ya kukishughulikia kisima hicho. Kwa sababu lengo ni kuhakikisha kusambaza maji katika vijiji vyote vya Unguja na Pemba.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa 2012

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nismhukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha tena kutukutanisha hapa leo katika Mkutano wetu huu wa Kumi wa Baraza la Wawakilishi tukiwa katika hali ya uzima, afya na furaha.

Mhe. Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya Mwaka 1997.

Mhe. Spika, kadhalika napenda niwashukuru viongozi wetu wakuu wa kitaifa akiwemo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa miongozo na busara zao zilizotusaidia kuhakikisha tunakamilisha rasimu hii kwa maslahi ya nchi yetu.

Aidha Mhe. Spika, naomba niishukuru Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa namna ambavyo wametupa ushauri na mapendekezo yao na ambavyo walivyokubaliana na serikali kwa mujibu wa mapendekezo yetu tulivyowasilisha kwao.

Mhe. Spika, kwa sababu hiyo basi, naomba uniruhusu niwataje Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu hii.

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mjumbe
5.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mohammed Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Ussi Jecha Simai	Mjumbe
8.	Ndugu Ramadhan Khamis Masoud	Katibu
9.	Ndugu Rahma Kombo Mgeni	Katibu

Mhe. Spika, baada ya kushukuru Kamati naomba uniruhusu kushukuru Baraza letu tukufu kwa namna mbali mbali walivyosaidia katika kuhakikisha kukamilisha Mswada huu wa Sheria.
Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako sasa naomba nifanye marekebisho madogo kupitia mswada wenyewe. Katika ukurasa wa 313 ile tarakimu inayosomeka “2012” zilizopo katika kifungu cha kwanza cha mstari wa pili zisomeke “2013” na yale maneno yaliyosema “asilimia 25” yaliyopo katika kifungu cha 5(2) (a) yasomeke “asilimia 20”. Na yale maneno yanayosomeka “asilimia 25” yaliyopo katika kifungu cha 5(2) (c) yasomeke “asilimia 30”.

Mhe. Spika, baada ya marekebisho hayo kwa ruhusa yako naomba niwasilishe kwa muhutasari mswada wenyewe.

Utangulizi:
Mhe. Spika, Sheria ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa ilipitishwa rasmi mwaka 1997. Madhumuni makubwa ya sheria hiyo ni kuiwezesha serikali kutimiza wajibu wake wa msingi wa kuimarisha demokrasia na utawala bora nchini. Kutokana na nafasi ya vyama vya siasa kama nguzo kuu ya demokrasia nchini na uwakilishi pia kama taasisi muhimu katika sera na mwelekeo wa taifa, takriban nchi nyingi zenye demokrasia ya vyama vingi hivyo serikali inatoa ruzuku kwa vyama vya siasa vilivyotimiza masharti ili kuvisaidia kuendesha shughuli zake ambazo zilikubalika kutumika kwa ruzuku hiyo na kwa mujibu wa sheria hiyo. Vyama vilivyopata kiti cha Rais, viti vya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani hupatiwa ruzuku hiyo.

Mhe. Spika, tokea kupitishwa kwa sheria ya rukuzu kwa vyama vya siasa Nam. 6 ya mwaka 1997, utekelezaji wake umeshindikana kutokana na sababu kuu mbili zifuatazo.

a) Kifungu cha 3(1) cha sheria kinaeleza kuwa ruzuku inayotolewa na serikali isipungue asilimia moja ya bajeti ya kawaida (re-current budget) ya kila mwaka. Kiwango hicho cha ruzuku ni kikubwa sana hasa ikizingatiwa changamoto za kiuchumi, kijamii na kisiasa ambazo serikali inapaswa kukabiliana nazo. Kutokana na hali hiyo Mhe. Spika, ilishindikana kuweza kutekeleza sheria hii.
b) Mgawanyo wa ruzuku hiyo kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria hiyo, mgawanyo wa ruzuku upo kama ifuatavyo hapo awali. Asilimia 50 ya ruzuku kwa chama kitakachopata kiti cha Rais, asilimia 30 kwa mujibu wa uwiano wa viti vya majimbo ya Uwakilishi na asilimia 20 kwa mujibu wa viti vya Wadi.

Mhe. Spika, mgao huu umekuwa ukilalamikiwa kuwa hauzingatii mustakabali wa vyama vya kisiasa na kiuendeshaji na kulazimisha ushindani mkubwa sana na mvutano katika kiti cha uchaguzi wa kiti cha Urais. Hivyo marekebisho yanahitajika ili kuiwezesha sheria hii kutekelezeka kwa manufaa yaliyokusudiwa.

Madhumuni ya Waraka huu:
Mhe. Spika, madhumuni ya sheria hii ni kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria Nam. 6 ya 1997 ili kuondoa kasoro iliopo katika sheria hiyo. Kasoro za msingi za sheria hiyo ni kama zilivyoelezwa katika utangulizi wa maelezo yangu.

Katika kuandaa mapendekezo yaliomo kwenye waraka huu serikali imechukua hatua za kushauriana na wadau wa sheria na kamati husika wamechangia kwa kina katika mapendekezo yaliyowasilishwa na serikali.

Mhe. Spika, mapendekezo ni kama yafuatavyo:-

Baada ya maelezo ni juu ya upungufu wa sheria iliopo ya vyama ya ruzuku kwa vyama vya kisiasa na baada ya kupitiwa na Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa na majadiliano na wadau, serikali inapendekeza kama ifuatavyo:-

a) Kuifanyia marekebisho sheria ya ruzuku ya vyama vya siasa Nam. 6 ya 1997.
b) Kifungu cha 3 cha sheria kinachoeleza kuwa kima cha ruzuku kitakachotolewa na serikali kirekebishwe kwa kueka kima cha ruzuku kisichozidi asilimia moja ya bajeti ya kawaida ya kila mwaka ya serikali.
c) Kifungu cha 5 cha sheria kifanyiwe kirekebishwe kwa kuweka mgawanyo mpya wa ruzuku kama ifuatavyo:-

    1. Asilimia 20 ya ruzuku iende kwa chama kilichoshinda kiti cha Urais
    2. Asilimia 50 ya ruzuku itagaiwa kwa uwiano wa viti vya majimbo vya Uwakilishi
    3. Asilimia 30 ya ruzuku itagaiwa kwa uwiano wa viti vya Udiwani katika Wadi.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Baraza la Wawakilishi katika mkutano wake wa tarehe 8 Januari, 2013 ilipata fursa ya kuyajadili kwa kina mapendekezo haya na hatimaye kuyaridhia.

Ninamshukuru Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na busara zao na kuona umuhimu wa kuwepo kwa sheria hii na hatimaye kuridhia mapendekezo hayo.

Hitimisho:
Mhe. Spika, kama inavyoeleweka kwamba nchi yetu ipo katika kutekeleza juhudi kubwa za kupanua misingi ya demokrasia na utawala bora, hivyo ninaomba kusisitiza kuwa marekebisho ya sheria hii yatasaidia sana kuifanya sheria ya ruzuku kwa vyama vya siasa ya 1997 iweze kutekekelezeka kwa ufanisi zaidi na hatimaye kuvisaidia vyama husika kupata msaada utakaowezesha kuendesha shughuli zao kama inavyotakiwa.

Aidha, naomba kupokea ushauri wa Kamati yetu ya Kudumu kuhusu maoni ya vyama vya siasa ili tuweze kuyafanyia kazi kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe waipokee rasimu hii ya mabadiliko ya sheria na kuijadili na hatimaye kuipitisha. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe wangu walisahau kidogo kama tuje kuhusu kuungwa mkono lakini Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko akakumbuka, ameunga mkono na wengine wakamfuata.

Kwa hivyo hoja hii sasa ijadiliwe.

Mhe. Mwajuma Faki Mdachi (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa mwaka huu wa 2013 kuwa wa mwanzo kutoa maoni ya Kamati za Kudumu za Baraza.

Mhe. Spika, naomba nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu za Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya sheria ya ruzuku kwa vyama siasa Nam. 6 1997 na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kukutana tena asubuhi ya leo katika Baraza letu tukufu ili kujadili masuala muhimu kwa ajili ya mustakabali mzima wa maendeleo ya watu wetu na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, vile vile nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niwasilishe maoni ya Kamati za Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa sheria ya marekebisho ya sheria ya ruzuku kwa vyama vya siasa Nam. 6 ya 1997 na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba niipongeze serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutuwasilishia mbele ya Kamati ya Baraza lako tukufu mswada huu muhimu kwa ajili ya kuimarisha sheria ya ruzuku ya vyama vya siasa ya mwaka 1997, hususan katika vifungu vilivyokusudiwa kufanyiwa marekebisho hayo.

Mhe. Spika, aidha kwa niaba ya kamati naomba niwashukuru wadau wote walioshiriki kutoa maoni na michango yao kwa mswada huu. Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano makubwa waliyonipa katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu na ninaomba niwataje wajumbe hao kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mjumbe
5. Mhe. Mohamed Haji Khalid	-	Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohamed Ali	-	Mjumbe
7. Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9. Ndg. Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu

Mhe. Spika, kamati yetu ilipokutana na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika kuujadili mswada husika pamoja na mambo mengine kwa pamoja ilikubaliana na ofisi hiyo katika kuufanyia marekebisho mswada huo. Miongoni mwa marekebisho hayo ni yale yanayokihusu kifungu cha 5 (2) (a) (b) na (c).

Marekebisho yaliyopitishwa katika kikao baina ya Kamati na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni yafuatavyo.

1. Maneno asilimia 25 kwa kifungu cha (a) yamerekebishwa na kusomeka asilimia 20.
2. Maneno asilimia 25 katika Kifungu cha (c) nayo yamefanyiwa marekebisho na kusomeka asilimia 30.

Mhe. Spika, kamati kwa ujumla inafarijishwa na marekebisho hayo na zaidi kutokana na sababu zilizotolewa na serikali, na mfano mzuri suala la kuongeza asilimia 30 badala ya 25 katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kumeelezwa kuwa ni kuimarisha serikali za mitaa, kamati yetu inaamini kuwa ongezeko hilo pia huenda likavihamasisha vyama mbali mbali vya siasa kuweka wagombea wengi katika uchaguzi wa Udiwani.

Mhe. Spika, sambamba na ongezeko hilo kamati yetu inaikumbusha serikali kuwasilisha hapa Barazani ule mswada unaozungumzwa siku zote, yaani Mswada wa Sheria ya ya Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa iwe sheria ambayo itayoziimarisha vyema serikali hizo.

Mhe. Spika, ujumla kamati yetu iliujadili mswada husika na kuupitisha pamoja na marekebisho yake ambayo nimekwisha yainisha hapo juu.

Mhe. Spika, kabla ya kukutana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ilikutana na wadau hapa ofisi ya Baraza la Wawakilishi ili kupata maoni juu ya mswada huu wa sheria ya marekebisho ya sheria ya ruzuku kwa vyama siasa Nam. 6 ya 1997.

Mhe. Spika, wadau hao waliuchangia mswada huu na kushauri yafuatayo:-

1. Kuwepo na asilimia maalum ya ruzuku kwa vyama vya siasa vinavyoshiriki chaguzi mbali mbali ndani ya nchi hata kama kura za wananchi hazikutosheleza kuviwezesha vyama hivyo kushinda chaguzi hizo. Jambo la msingi ni kuzingatia namna gani vyama hivyo vinaweza kupata kura kwa asilimia nzuri yenye kuridhisha.
2. Vyama vya siasa vipewe ruzuku kwa ajili ya kuimarisha demokrasia, ushindani wa kisiasa pamoja na uhai wa vyama hivyo.
3. Vyama vya siasa ambavyo havina viti vya uwakilishi na udiwani viungane ili viweze kuongeza nguvu za kushindana na kujipatia ushindani katika chaguzi mbali mbali.
4. Vyama vya siasa vinaipongeza Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuweka utaratibu wa kuwashirikisha wadau mbali mbali katika kuchangia miswada ikiwemo Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam.6 ya 1997.

Mhe. Spika, kamati yetu inayathamini na kuyaheshimu maoni haya, hivyo basi kamati inashauri serikali kuyapokea na kuyazingatia na kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha maoni haya ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo kabisa baada ya mchango wa mwenyekiti kuuchangia mswada huu ambao kwa kweli ni mfupi sana, lakini ni mswada muhimu sana katika ujenzi wa demokrasia wa nchi yetu.

Mhe. Spika, nataka nianze moja kwa moja kwenye madhumuni na sababu. Tumeelezwa hapa kwamba marekebisho ya sheria hii yanatokana na sababu mbili kuu.

Moja ikiwa kiwango kile cha ruzuku serikali inashindwa kukitekeleza na kwa hivyo ikafanya mabadiliko kutoka yale maelezo yanayosema si chini ya asilimia moja ya mapato ya serikali na sasa yamekuwa si zaidi ya asilimia moja.

Mhe. Spika, ukiyazingatia maneno hayo utaona yanakaribiana lakini yana tofauti kubwa sana. Maana ukisema si chini ya asilimia moja basi maana yake inaweza ikapanda juu mpaka ikawa asilimia mbili, tatu kadri hali itakavyowezekana. Ukiangalia kwa msingi huo ni kweli kama serikali ingeshindwa kutoa lakini pia ukisema si zaidi ya asilimia moja Mhe. Spika, hii lugha ukiitizama kwa undani kidogo inatisha.

Inatisha kwa sababu inategemea sasa nia njema ya serikali. Wanaweza wakenda mpaka asilimia moja hiyo itakuwa nzuri lakini si zaidi ya asilimia moja wapo huru kwenda mpaka asilimia ziro nukta tano.

Sasa hofu yangu mimi, ninaamini serikali itakuwa na nia njema lakini hofu yangu serikali siku itakayokosa nia njema wanaweza wakavigawia vyama vya siasa shilingi milioni tano, kwa sababu haiwafungi hii sentesi. Sasa nilikuwa nafikiri tuangalie uzoefu unavyotwambia serikali inakusanya mapato kiasi gain kwa mwaka, halafu tukaweka figure basi tukaitaja hasa kama ni milioni mia sita, milioni mia ngapi zitatolewa kwa vyama vya siasa. Lakini tukiweka hivi ni nzuri kwa siku nyengine lakini siku nyengine inaweza ikawa mbaya.

Nadhani *practice* zaidi itakayoleta uzoefu lakini nilikuwa ninahisi siku mbele tuje tuangalie kitu kama hicho. Nilikuwa ninajaribu hapa kumuuliza Waziri wa Fedha anipe alau uzoefu wa mwaka jana walikusanya kiasi gain ili nipate *proposal* figure gain iweze kutumika lakini bahati mbaya naye haikuwa tayari sana.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nilitaka niligusie kidogo ni hii asilimia ilikuwa 25 lakini hivi sasa ni asilimia 20 kwa mujibu wa mapendekezo ya kamati. Mhe. Spika, ukiangalia *concept* ya huu mkondo wa ruzuku umegawika makundi mawili. Kundi la kwanza vyama vilivyoeka mgombea Urais lakini kundi la pili ni vyama vilivyoshinda viti vya majimbo na viti vya Madiwani, wodi zile.

Sasa tatizo katika hii formula ya mgao iliyoekwa kwenye viti kama vya Uwakilishi au Udiwani. Maana yake imeelezwa hapa kama asilimia 50 itakwenda kwa vyama vya siasa kwa misingi ya uwiano wa idadi ya majimbo walioshinda katika Baraza.

Kifungu cha (c) kinaeleza asilimia 25 sasa ni 30 kwa mujibu wa marekebisho, vinakwenda kwa vyama vya siasa kwa msingi wa uwiano wa idadi ya wodi walizoshinda katika chaguzi za serikali za mitaa.

Sasa hii mimi sina tatizo nayo kwa sababu ipo direct lakini nipo hapa kwenye kifungu cha (a) ambacho kinataja asilimia 20 kwa chama kilichoshinda kiti cha Urais. Sasa Mhe. Spika, hapa pana upendeleo kidogo, kwa sababu walioingia katika mbio za Urais ni wengi au ni vyama vingi,

kama vile ambavyo walivyoingia katika mbio za viti vya udiwani na uwakilishi ni vyama vingi, lakini kule tumeteremsha asilimia kwa mujibu wa idadi ya viti, lakini hapa tumetoa kwa chama kimoja tu kilichoshinda.

Sasa mimi nilikuwa ninadhani, ilikuwa formula hii iliyoteremka huku chini basi na hii ya mbio za Urais ingekuwa vile vile, kwamba nayo tungeangalia kwa mujibu wa kura walizopata wagombea Urais, nayo hii ikagaiwa vile vile lakini akipewa mtu mmoja na wengine waachiwa, mimi ninadhani si sahihi sana.

Lakini pia nilikuwa ninataka niongeze jambo hapa sijui ile sheria yenyewe hasa bahati ilipokuwa inatungwa mimi nilikuwa sikuwepo na sijaipata kwa kweli, lakini sijui kama ipo hivyo au vipi. Lakini nilikuwa ninahisi hii kwanza izingatie vyama vyote vilivyoshiriki katika uchaguzi wa Urais. Lakini basi paekwe mpaka au paekwe masharti pengine ndivyo ilivyo katika sheria sina uhakika uzuri, lakini *at least* kile chama ambacho kimeweza kupata alau asilimia kumi ya *total voters* na vile ambavyo havikupata asilimia kumi basi hivyo katika ruzuku Mhe. Spika, ni afadhali visiwemo kwa sababu vinatuongezea mzigo tu.

Mhe. Spika, hata kama watakaonisikiliza kama ninabinya demokrasia lakini unaweza ukashangaa masharti ya kuwa na chama cha siasa au chama cha siasa cha kukubalika kuwa *registered* yalielezwa wazi na yakasemwa kwamba lazima chama hicho kipate udhamini wa watu mia mbili kutoka kwa kila mkoa.

Sasa unaweza ukashangaa kwamba chama kinapata wadhamini mia mbili katika kila mkoa, mimi nilikuwa ninadhani hao ni wanachama wa chama hicho na taaban kwa sababu ni wanachama wangeweza kukipigia kura chama hicho siku za uchaguza.

Lakini tunapofika pahala chama tunapoingia kwenye uchaguzi tukatoka na kura arobaini, sasa mimi ninakujiuliza jee chama hicho hivyo kweli kimesajiliwa kihalali, maana yake kama ni arobaini hata wale wadhamini wake hakijapata. Sasa ukichukua fedha za wananchi ukiwapa hawa mimi ninadhani sijui kama itakuwa ni sahihi tena. Kwa hivyo nilikuwa ninasema hii ruzuku ya asilimia 20 ni vyema kwa mapendekezo yangu ikaangaliwa kwa kura watakazopata wagombea Urais na ikagaiwa hivyo, lakini *at least* chama kile ambacho kitapata angalau asilimia kumi ndio kiwemo katika hizo sifa za kupata hii ruzuku, walio chini ya hapo mimi ninadhani wangetusamehe wakajikaza kwanza wakafika hapo.

Mhe. Spika, mswada huu ni mfupi sana na hauna mambo mengi ya kusema ni hayo mawili tu.

Baada ya kusema hayo mimi ninadhani Mhe. Waziri atakuwa kanisikia vizuri na atayazingatia na naomba niwape fursa wenzangu waweze waliyonayo.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa asubuhi ya leo nikawa ni mtu wa pili kuchangia suala la mswada kuhusu ruzuku za vyama.

Mhe. Spika, ni kweli ipo haja ya kuleta mabadiliko ya aina hiyo ili kuweza kuvipa nguvu ili kuweza kuvisaidia vyama vyetu ambavyo tunavyopambana navyo. Lakini Mhe. Spika, pamoja na hayo tukifika kuleta miswada kama hii kwenye Baraza, hii ni dhahiri ni kuonesha Mhe. Spika, kukwa tayari uchumi tunao na ndio maana tukaweza kuleta sheria hizi ili kuweza kuanza kuwagaia wenzetu wenye vyama.

Lakini pamoja na hayo Mhe. Spika, ningeomba sana serikali ili kuweza kuangalia kwa uangalifu kabisa, mimi nimeona mswada kuja ingali ni mapema sana, hili tukitaka tusitake ni hivyo. Mutakuwa ni mashahidi Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kuwa mswada huu una mantiki ya watu kuongezwa fedha, wakati leo bado wafanyakazi wetu bado wanaendelea na mshahara mdogo, kuwa leo mutaukubali na kuunga mkono, mimi nitakuwa ni mtu mmoja wa maajabu makubwa sana.

Kwa sababu tukipitisha huu ina maana tayari tunatoa fedha, mishahara leo bado ingali midogo sana ya wafanyakazi wetu. Kwa hivyo mimi ninaomba sana jamani Wajumbe wenzangu tukaangalia hili suala, hii ruzuku ambayo inayotaka kupelekwa huku tukawapelekea wale ambao ndio walengwa, ndio wenye vyama wenyewe, hebu tugeuke hizi sentensi tuziangalie kwa sababu wale ndio wenye vyama waliokuwapo kule wafanyakazi ndio wenye vyama.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ningeomba sana mswada huu tukauulekeza huko. Hali ni ngumu Mhe. Spika, hili tukitaka tusitake ni lazima tuliseme hali ni ngumu tuseme ukweli, wafanyakazi wetu wanapata mshahara mdogo sana. Hali kila siku kukicha mambo yanazidi kuwa makubwa. Hata ufanisi tunaukosa, wataalamu tunawakosa na hiyo mimi ningeomba sana Mhe. Spika, hili suala tuliangalie kwa mantiki makubwa sana.

Lakini Mhe. Spika, pamoja na kuendelea na kifungu hicho mimi naona asilimia hii 25 ibaki pale pale kwa Mhe. Rais kwenye kifungu cha (b) asilimia 50 iwe pale pale. Lakini katika kifungu cha (c) basi tuweke hiyo asilimia 20 kwa mtizamo wangu mimi.

Hayo yote Mhe. Spika, tena tusiongeze mambo mengine humu kwa sababu kila tukiongeza au kupunguza ni uzuri zaidi kuliko tukaongeza. Mimi naomba sentensi hii ibaki vile vile Mhe. Spika, kwa mtizamo wangu mimi, tukiibadilisha sentensi hii itakuwa na mantiki nyengine, kwa sababu wanasheria wanasema kuwa neno moja lina tafsiri ya zaidi ya kumi.

Sasa mimi Mhe. Spika, naogopa kubadilisha neno hili nikalitafsiri nyengine. Kwa maana hiyo nasema tubakie na hiyo hiyo asilimia ambayo itaweza huko nyuma tumeshaizoea na watu wetu wanajua hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, tukiingia ukurasa wa 314, sababu nimeziona hapa zimeshatolewa na ndio maana nikasema kifungu hiki nikianzia na masuala haya, kwa sababu mimi naomba kidogo kwa ruhusa yako kwa mujibu wa Kanuni inavyoniruhusu nikisome kidogo ndio nitakapoona raha.

Mhe. Spika, kifungu kinasema kuwa sababu ya kwanza ni uwezo wa serikali kwa mujibu wa sheria hiyo serikali inatakiwa itoe ruzuku kwa vyama vya siasa isiyopungua asilimia moja ya bajeti ya kawaida ya kila mwaka, ukizingatia na hali ya uchumi, ukusanyaji wa mapato na matatizo ya msingi ambayo serikali inapaswa kukabiliana nayo katika kila mwaka wa fedha

imekuwa vigumu sana kwa serikali kutenga kima hicho cha fedha kama ruzuku inavyoeleza. Ndio pale mwanzo nikasema na nikawataka Wajumbe wenzangu wanikubalie kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, uchumi huu tayari kila siku kukicha tunaambiwa tuna makusanyo asilimia kubwa sana tena tumepindukia. Mimi niwashukuru sana serikali tena nawashukuru sana wale ambao ni wahusika zaidi wakusanyaji wanaoziba mianya ya watu sasa hivi wasiibe, niwashukuru sana. Kwanza niwashukuru watu wa *ZRB* wanafanya kazi vizuri sana kwa kutukusanyia mapato mengi sana. Hata leo tunathubutu tunataka kuwagaia vyama, hili moja ni makusanyo makubwa ya vianzio vyetu.

Lakini vile vile serikali, jamani hata tuwe na mpango wa kuongeza vianzio ili na hawa watu wa vyama tuje kuwaongezea ruzuku nyingi, lakini ikiwa vianzio vyenyewe viko pale pale tu, vile vile vitano basi tutakuwa tuko pale pale tunazunguka tu na hatimaye ndio maana tunasema kwamba wafanyakazi wetu tunawakosesha mishahara. Vianzio vinakuwa kidogo, bandari bado ni finyu, tuongeze bandari ili tupate makusanyo mengi sana.

Mhe. Spika, hapa mimi nimeona kuwa sasa serikali inataka kuleta muelekeo mzuri kwa kuwasaidia vyema ili tuweze kupata kushindana nao. Lakini sheria hii sisi ndio tunatunga sheria haimlengi mtu, inawezekana mimi nikawa Rais pengine nikaja nikafaidika na ruzuku hii. Ndio kwa sababu sheria haikumtaja mtu hii. Kwa hivyo, tusione tabu kuweka asilimia 25 mpaka asilimia 50 kwa Rais. Ni kweli Mhe. Spika, kwa sababu kuna leo na kesho. Sasa mimi ni nani mtajua nyinyi, inawezekana kwa Mungu hakuna dogo bwana hata siku moja. Mimi ninaweza nikawa Rais na wewe ukawa Makamo wangu, ndio ilivyo Mheshimiwa.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuliona hili na kufikiria kuwa sasa tunataka kuleta *challenge* ya kuvifanya vyama vyetu viwe katika ushindani kuwa na hali ya kifedha. Mhe. Spika, kama ulivyosema mswada wake ni mdogo sana na vifungu vyake vidogo. Sasa sitaki niendeleze nikavitoa utamu. Nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutuletea mswada huu. Kwa hayo machache Mhe. Spika, nasema naunga mkono kwa asilimia 65 na baadae akinijibu vizuri, basi nitammalizia na zilizobakia. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutia tia nyalio katika marekebisho haya yaliyoletwa mbele yetu. Lakini kabla ya hapo Mhe. Spika, kwanza naomba uniruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na hatimaye kutupa uwezo na nguvu za kutoka katika maeneo yetu mpaka katika jengo hili tukufu. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Nadhani Mhe. Spika, nitakuwa mchache wa shukrani kama sitotumia fursa hii kukushukuru wewe vile vile kwa kunipatia fursa ya kuweza kutoa mawazo yangu hapa leo. Hii ni ihsani kubwa uliyonifanyia na kwa vyovyote vile nakushukuru sana.

Mhe. Spika, naomba nimalizie shukrani zangu kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Sherehe na Mapambo ya Taifa Balozi Seif Ali Iddi. Yeye, ofisi yake pamoja na Kamati nzima ya Sherehe na Mapambo kuweza kufanikisha vizuri sana sherehe ya Mapinduzi iliyofanyika juzi.

Kwa kweli mmejitahidi sana na mnastahiki sifa, lakini katika hili Mheshimiwa naomba uniruhusu kidogo nitie tanbihi ndogo.

Mhe. Spika, fedha zinazotumika katika matayarisho mbali mbali ya sherehe zetu za nchi, zinatokana na fedha za walipa kodi wa nchi hii. Kwa hivyo, kila mwananchi ameguswa na sherehe ile na kila mmoja anastahiki apate furaha moyoni mwake siku ile ya sherehe, kwa fedha zake zimetumika katika kuhudumia sherehe ile.

Sasa tanbihi yangu Mheshimiwa naomba tu jambo moja, kwa sababu Mwenyekiti yupo hapa, basi nimpe tanbihi kwamba tujitahidi sana mwaka ujao kuangalia rangi nyengine. Katika zile sare ambazo tulivaa siku ile nyingi zilikuwa ni za rangi ya manjano ambazo ni sare ya chama kimoja cha siasa. Kwa kweli hatukufanyiwa haki walipa kodi wa nchi hii, naomba mara hii muangalie vizuri sana katika kutayarisha sherehe. Lakini pamoja na hayo nakupongeza sana wewe na Kamati yako kwa kuweza kufanikisha hili.

Baada ya dibaji hiyo fupi Mhe. Spika, naomba sasa niende katika hoja iliopo mbele yetu. Mhe. Spika, kama kuna kitu cha kusifiwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ni kuleta marekebisho haya. Kwa hivyo, nampongeza sana Waziri kwa kutuletea marekebisho haya, kwa kweli amefanya kazi nzuri tu, kutokana na sababu zifuatazo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, historia ya vyama vya siasa, inaonesha kwamba vyama hivi havikuja tu hivi hivi, hapana; kwamba tulikaa tu sisi tukaanzisha vyama hivi, la hasha! Vyama hivi vilikuja baada ya serikali kuunda tume ya kupita kuuliza wananchi kutoa maoni, na hatimaye kwa nia safi sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ikaamua kuanzisha mfumo huu wa vyama vingi. Hii kwa kweli ni nia nzuri, na wala serikali haikuleta tu vyama kwamba tuwe wengi katika kukimbilia mbio za kuingia Ikulu, la hasha! Lakini ilikuwa ni katika kupanua demokrasia ya nchi pamoja na utawala bora.

Mhe. Spika, kuanzisha vyama ni hoja moja, lakini vile vile kuviwezesha vyama kufanya kazi zake kwa kweli ni hoja nyengine nzito. Mwaka 1992 hapa vyama vilianzishwa kwa kupitia sheria nambari 5 ya Jamhuri ya Muungano, na tukatakiwa kuanzisha vyama. Mimi na wenzangu kina Mzee Mloo, James Mapalala na kina Mabere Marando, tukaanzisha vyama vya siasa, tulipoanzisha vyama vya siasa Mhe. Spika, tulipata kazi kubwa sana, tukahangaika nchi nzima tukaambiwa lazima tupate wanachama 200 katika Mikoa 10 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati natakiwa nipate wanachama 200, *I can't afford even to have a day meal* na mimi nikataka kuanzisha chama cha siasa Mheshimiwa.

Sasa ilikuwa ni tatizo wakati chama cha CCM tayari kipo kinaleta mageuzi, mimi nataka kuanzisha sasa chama na tumesharuhusiwa na serikali kuanzisha. Tukawa tunapata shida sana mimi na wenzangu, wenzangu kina Ndimara Sebabwage, kina Mabere Marando, kina Mzee Mloo marehemu bwana Ali Haji Pandu, tulipata shida sana Mhe. Spika. Nimeamua kutoa historia ndogo katika hili kwa sababu ruzuku ya serikali iliopo iende mbele zaidi, kwa sababu unapopata usajili wa muda basi unatakiwa urande nchi nzima, na kule kuranda nchi nzima kuna gharama kubwa tu, mpaka upate ule usajili wa kudumu basi unatumia pesa nyingi sana. Lakini katika ruzuku hatukuona, lakini naamini mswada huu ni mabadiliko makubwa sana yamefanywa na serikali, na mabadiliko ni *process*, naamini kuna siku na hapo mtapaona kwamba vile vyama

vikihitaji kupata usajili huwa vinahitaji fedha na fedha huwa hawana, sasa serikali itafanyaje ili kuvisaidia hivi vyama katika kupata ule usajili.

Hii ni nukta moja ambayo nadhani kwa hapo mbele Mhe. Waziri atuangalie sana, usajili wa chama ni mgumu, ukitaka kuyatimiza masharti na ukiwa huna fedha ni ngumu na fedha hizi jamani ni za walipa kodi wote mpaka hao wanaotaka kuanzisha hivi vyama na wao tuwaangalie. Kwa hivyo, huwezi kupata ruzuku hii kwa mujibu wa sheria hii mpaka chama ukianzishe, hata ukakianzisha hicho chama na kukipata ni kazi. Sasa tutavisaidiaje hivi vyama ambavyo vinawania sasa usajili, hilo ni moja Mhe. Spika.

Mhe. Spika, jambo la pili ni hii nukta ya asilimia 25 ya nafasi ya chama kilichogombania urais. Mhe. Spika, hapa nashukuru pamewekwa chama, kwa sababu kuna siku pengine kutakuja kuwa na mgombea binafsi tuje tuzimimine pesa hizi kwa atakayeshinda urais kupitia *private candidate.* Lakini nashukuru kwamba hapa tumeweka chama.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono hili, lakini naomba niishauri serikali tu kwamba *for the long run*, basi tutakuwa tuko *bias* sana, kuchukua asilimia 25 ya fedha za walipa kodi, tukakimiminia chama kimoja tu cha siasa au mgombea mmoja tu wa siasa. Mimi nadhani tungekwenda kwa uwiano wa *number of vote*, kwa vile wale wanaokwenda kwenye *presidential race.* Tukaweka tu sio kwamba mtu kagombania tu hivi tumpe, pengine tungetenga asilimia fulani, pengine kwa chama kitakachogombania urais akipata kuanzia asilimia 10 basi aweze kupata na yeye chochote, ili mwaka wa mwakani ajitayarishe tena kuja kugombea tena urais. Lakini kinyume na hivyo, itakuwa siku zote tunagombania sisi tu na CCM urais na hao wengine hawana uwezo. Hilo ni jengine Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tatizo jengine ambalo katika mswada huu ambalo naliona, ni *auditing* ya *public fund.* Hizi fedha ni fedha za walipa kodi wa nchi, fedha za ruzuku ya chama ukizipeleka kwenye chama. Kuna vyama vyengine mimi nakumbuka tulipoanzisha vyama, kuna vyama vyengine sitaki nivitaje, lakini kuna chama kimoja alikuwa Mwenyekiti na mkewe alikuwa ni Katibu Mkuu wa hicho chama, yaani mume ni Mwenyekiti wa chama na mke wake ni Katibu Mkuu wa chama. Sasa tukiangalia vyama kama hivi tutakuja kuvipa fedha hizi je, hawatozitumia kwa kuwasomeshea watoto wao fedha hizi. Kwa hivyo, nadhani kuwe na utaratibu maalum wa kuzi-*audit* hizi fedha kwa sababu ya kukimbia hayo.

Mhe. Spika, mimi nakumbuka kuna chama kimoja sitaki nikitaje, lakini rafiki yangu mmoja alikuwa ni Mwenyekiti, na Katibu Mkuu ni mke wake na Naibu Katibu Mkuu ni mtoto wake wa mwanzo, ni tatizo kubwa Mheshimiwa hili. Sasa unachukua fedha unazipeleka kwenye familia tu hivi. Kwa hivyo, tuandae utaratibu sisi tunaotaka kupitisha haya marekebisho, kwamba sijui utaratibu ukoje, lakini lazima *PAC* waweze kwenda katika vyama vya siasa, kwa sababu sisi kazi yetu sio kupitisha tu hizi bajeti, lakini ni kusimamia matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi, ikiwemo hii ruzuku.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nadhani kwamba utaratibu wa kuzikagua fedha hizi, serikali iwe ina *great role* kwa kupitia ma-*auditor* wake, lakini vile vile na hiki chombo kiwe na haki ya kupita kwenye vyama vya siasa kuzi-*audit* hizi pesa, isiwe kwamba zinatumika kwa matumizi mengine tu, hapana, zitumike kwa mambo muhimu, kwa sababu vyama vya siasa vina kazi nzito.

Vyama vya siasa kazi yake sio kugombania udiwani, uwakilishi na urais tu, lakini vile vile vina-*role* ya ku-*stabilize* hii amani na utulivu katika nchi. Sasa wazitumie pesa hizo kwa kutoa *civic education* na mambo mengine, sio kwa kwenda zao Dodoma kule na kwengineko, lakini watumie katika mambo haya.

Mhe. Spika, mimi nilipoviangalia vipengele vyote vitatu vya ruzuku hii kwa hapa Zanzibar, basi mimi nashukuru kwamba chama chanagu kimeguswa sana na ruzuku hii, nampongeza sana Waziri. Lakini tujue tu kwamba vyama hivi viwili vya CUF na CCM havifiki hata asilimia 30 ya *total vote*s za nchi. Kwa hivyo, na hizi pesa zinatoka kwa wananchi wote, hivyo baadae huko mbele tuandae utaratibu utakaoweka mazingira ya hawa walipa kodi wengine na wao vyama vyao kuweza kunufaika angalau kidogo katika hizi pesa.

Kwa sababu Mhe. Spika, moja kati yetu ni kuangalia *interest* ya vyama vyetu, kuangalia *national interest* ya nchi, kuangalia maslahi ya jimbo, lakini vile vile na *national interest* nayo inatakiwa tuiweke mbele kuwatetea wananchi, hata ikiwa sio wanachama wa vyama vyetu. Kwa hivyo, nadhani serikali baadae waone ni utaratibu gani kila mmoja ataguswa na hizi pesa zinazotoka katika jasho lao.

Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa sababu huu mswada hayo marekebisho yenyewe ni madogo sana. Napenda tena nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta mabadiliko haya na mimi nasema amechelewa sana kuleta mabadiliko haya kuviwezesha vyama vya siasa. Nadhani katika hili Mhe. Spika, kwa sababu mswada huu ulikuwepo tangu mwaka 1997 inasikitisha sana na sababu alizozitoa sio za msingi za kwamba sheria hii haikutekelezwa. Hizi sababu zote mbili Mhe. Spika, sio za msingi, bajeti ya nchi kwamba hairuhusu, sio sababu ya msingi na kwamba eti mgawanyo wa ruzuku utaleta mvutano katika mambo ya vyama, sio sababu za msingi alipotuomba Mhe. Waziri.

Sasa mimi naomba tu kwamba utakapopita mswada huu Mhe. Spika, na Rais akishasaini, basi tuangalie uwezekano japo wa kulipa *arrears,* kuanzia ile sheria kongwe iliposainiwa hadi hapa atakapo saini Rais, kwa sababu hizi sababu alizozitoa Waziri hazina msingi na vyama ni haki yao kupata hii zuruku. Kwa hivyo, mimi naomba serikali lazima ibebe mzigo wa kuweza kulipa *arrears,* kuanzia *August 1997 up to date* ili wavitendee haki vyama vya siasa kwa sababu fedha hizi zinatoka katika mfuko wao.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu mno, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Spika, na mimi sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake, kutujaalia kuwa tuko hali ya uzima na afya nzuri na bahati njema ikawa katika Baraza zima la Wawakilishi hakuna upungufu wa aina yoyote, si neema ndogo ya Allah na pia nimtakie rehma Mtume wetu Muhammad (SAW).

Mhe. Spika, na mimi sina budi kusema kwamba ninashukuru leo tarehe 16/01/2013, nikawa nimeingiza maneno machache katika *hansard* kwa suala zima la mswada huu wa sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ya nambari 6 ya mwaka 1997 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, marekebisho yaliopo hapa ni madogo lakini ni mazito, kwa hivyo ni vyema Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tukawa wazi kabisa na kutoa maoni yetu, ili kuondosha utata ambao serikali ilishindwa kutekeleza sheria hii kwa muda wa miaka iliyopita.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 kwenye Sehemu ya Pili ya marekebisho, serikali inasema itatoa si zaidi ya asilimia 1 ya bajeti ya kila mwaka. Nikubaliane na wale waliochangia kwamba kuwa na kitu sio zaidi, lakini ikakosekana neno isiyopungua, kwa hivyo bado itakuwa yale mashaka waliyoiona serikali kwamba haiwezi kutekelezeka hili basi tungeomba pia "isiyopungua" neno hili liingizwe katika mswada huu. Kwa hivyo, hilo ni ombi langu moja.

Lakini ukija katika suala zima la ugawaji wa hizi asilimia, mimi nakubaliana moja kwa moja na maoni ya Kamati pamoja na maoni ya Waziri aliyoyawasilisha mbele yetu asubuhi hii. Lakini Mhe. Spika, ili kuvifanya vyama vya siasa viweze kukurupuka na kuja juu, basi ni vyema katika asilimia hizi, vile vyama vitakavyoshiriki katika chaguzi zetu, basi asilimia hizi zisibakie katika vyama vyenye kushinda tu.

Mhe. Abdalla hapa alitoa wazo kwamba chama kisipungue asilimia 10 katika uchaguzi ule. Mimi naungana naye kwamba chama chochote cha siasa kitakachoshiriki basi kitakapofikia asilimia 10 ya kura, basi ruzuku hii vyama hivi navyo viweze kujaaliwa ruzuku hii ili waweze kupiga hatua. Lakini kama vitaangaliwa vyama vyenye kushinda tu Mhe. Spika, basi Zanzibar itakuwa vyama vyetu vya siasa haviwezi kukua na kupiga hatua mbele.

Kwa hivyo, Mhe. Saleh Nassor hapa alisema kwamba; na ni kweli kuwa ruzuku hizi zinatoka ndani ya migongo ya wananchi wa Zanzibar, akiwa ni CUF, CCM au akiwa ni chama chengine chochote au pia akiwa hana chama lakini anachangia tu siku hizi. Kwa hivyo, ni kila mwananchi anahusika. Hivyo na vile vyama vitashiriki katika chaguzi, iwapo chama hakikushinda, lakini kuweko asilimia fulani ya kuweza kupata ruzuku hizi.

Mhe. Spika, niseme kwamba kwenye madhumuni huku Waziri ameeleza kwa kupitia kwa wanasheria kwamba sheria hii ilishindwa kutekelezeka. Sasa suala kama hili kwa muda wa miaka iliyopita tukaletewa leo kuwa tupitishe katika mabadiliko haya. Kwanza Mhe. Spika, naomba kwamba kauli iliyoandikwa katika sheria hii kwa kweli ni aibu kubwa kuwa mwaka 1997 ilipofikishwa kwenye Baraza hili, sheria hii ikapitishwa na hadi kufikia leo mwaka 2013 imeshindwa kutekelezeka, ndio tunaifanyia marekebisho. Kwa kweli inaonesha udhaifu mkubwa kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na ni aibu kwa serikali, kwa sababu moja ninaloliona ni kwamba tunapotunga sheria na sheria zile tusiziweke wazi ili Wajumbe wa Baraza wakaweza kuchangia vizuri, basi hatima yake ni matatizo kama haya yanaanza kujitokeza na mengine yatajitokeza zaidi.

Mhe. Spika, mimi ningewaomba sana wanasheria wetu wanapojaribu kuweka sheria, basi waache mibano, wasiweke mibano ili sheria iweze kupitishwa na Baraza, na Wawakilishi wetu waweze kuifahamu vya kutosha. Mwakilishi anapoifahamu sheria na akaweza kutoa michango yake, basi anaifanyia urahisi wizara ile yenye kuleta sheria ile. Lakini ikiwa sheria zetu tumezibana, Mwakilishi anapotoa michango yake hafahamu anachangia nini, kwa kweli hatima

yake ni kama haya yaliyotufika hapa kwamba sheria ina miaka imeshindwa kutekelezwa kwa sababu ya ugumu na hali halisi ya maisha na ruzuku inayopatikana serikalini.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, jambo kama hili ningeinasihi sana serikali tusiwe na tabia kama hiyo. Pia niseme kwamba wakati sheria imepitishwa muda mrefu na Rais kaitia saini, basi ni vyema, mimi sisemi kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor kwamba tokea mwaka 1997 vyama hivi viweze kupewe *arrears*. Lakini serikali ione kwamba ni muda mrefu wamevikosesha vyama vya siasa ruzuku. Kwa hivyo, ni vyema kuanzia mwaka 2000 basi waweze vyama hivi kupewa ruzuku zao ambazo ni muda mrefu hawajapewa, kulikoni inavyoeleza hii sheria kwamba itakapotiwa saini iweze kutekelezwa. Hivi itakuwa hatukuvitendea haki vyama vyetu vya siasa. Kwa hivyo, ni vyema kuanzia mwaka wa 2000 basi angalau vyama hivi wapewe *arrears* zao ili na wao waweze kunyanyuka na kuweza kuendesha siasa vizuri hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kutokana na hali mswada wenyewe ulivyo, mimi nimetoa mchango wangu huo na naunga mkono mswada huu, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu mfupi juu ya mswada huu uliopo mbele yetu. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi hii kusimama mbele ya Baraza hili kutoa mawazo yangu. Pia niwatakie wenzangu wote baraka za mwaka mpya, tuendelee kwenye mwaka huu kwa amani na upendo.

Mhe. Spika, kadhalika nikushukuru wewe kwa umahiri wako wa kutuongoza katika hali nzuri kabisa. Pia niipongeze Wizara hii ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuletea mswada huu wa marekebisho ya sheria nambari 6 ya mwaka 1997, inayohusu ruzuku kwa vyama vya siasa.

Mhe. Spika, Zanzibar kabla ya Mapinduzi haya ya mwaka 1964, tulikuwa na mfumo huu wa vyama vingi vya kisiasa. Wakati huo mimi sijui ni vipi vyama hivi vilikuwa vinaendeshwa, kuwa vilikuwa na ruzuku kutoka serikalini au vilikuwa ni michango ya wanachama wenyewe kuweza kuongoza chama chao. Lakini nilikuwa nikiona kwa baadhi ya wakati kwenye mikutano mbali mbali ya vyama, ilikuwa viongozi wanafika na vijikapu, kama vile watu wanavyopita Misikitini hivi sasa kuomba michango ya watu, basi kuna watu wanatoa pesa mbili pesa nne na wengi humu pesa mbili hawaijui lakini Mhe. Abubakar Khamis Bakary anaijua, lakini wengi hawaijui. Kwa hivyo michango ya aina hiyo ilikuwa ikitolewa, ili wanachama wa chama fulani kuweza kukiimarisha chama chao.

Mhe. Spika, michango ya aina hii ndiyo iliyojenga Makao Makuu ya pale Kisiwandui na wakati huo ilikuwa Makao Makuu ya Afro Shirazi na leo ni CCM. Michango mbali mbali na michango ya aina hii ndiyo iliyoweza kufikisha hicho chama katika hatua hiyo mpaka ikaweza kufanya mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya mapinduzi, chama kilichofanya Mapinduzi cha Afro Shirazi kilipiga marufuku huu mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa nchini. Kwa hivyo, tukaendelea na mfumo wa chama kimoja na kila mtu akawa ni Afro Shirazi au akabakia kuwa hana chama chochote, lakini kisiasa ikawa kila mtu ni Afro Shirazi. Hatimaye kwa kuwa dunia sio inazunguka tu ki-

geography kupata usiku na mchana, pia inazunguka katika mabadiliko mbali mbali. Sasa kutokana na mabadiliko ya kidunia huu mfumo umejirejea tena wa vyama vingi vya kisiasa.

Mhe. Spika, baada ya mapinduzi takriban kila mtu alikuwa Afro Shirazi na mfumo uliporejeshwa watu walitoka huku na kuasisi vyama vyengine, ambavyo navyo kwa hatua ya awali vilianzishwa katika mfumo ule ule uliokuwepo kabla ya mapinduzi, kwamba wanachama husika kuchangia chama chao ili kiweze kustawi.

Sasa kwa kuwa dunia ina mabadiliko na sisi Zanzibar au Tanzania ni kisiwa, tunakwenda labda na dunia ilivyo. Kwa hiyo, inawezekana ikawa duniani na wala sina hakika kwamba serikali zinatoa ruzuku kwa vyama, na kama hivyo ndivyo basi na sisi tumeiga, kama sivyo sisi tumeona kuna umuhimu wa kuvisaidia vyama vyetu, ili viweze kuendeleza kazi zake za kisiasa.
Kwa hivyo, hii naipongeza afisi husika kwa kuliona suala hili la kuweza kuvinyanyua na kuviendeleza vyama vya kisiasa.

Mhe. Spika, Tanzania tunavyo takribani vyama 14 hadi 20 ambavyo vimepata usajili wa kudumu na kwa kuwa vina usajili basi vinaruhusiwa kufanya siasa ndani ya Tanzania ikiwemo Zanzibar.

Lakini sheria yoyote inayotungwa lazima ikaekewa mipaka yake. Kwa mfano kwa hapa Zanzibar kwa hivi sasa ruzuku hii pindipo mswada huu ukiwa sheria vitakavyonufaika ni vyama ambavyo hivi sasa vina Wajumbe katika Baraza hili ni vyama viwili, ambapo ni Chama cha Mapinduzi na Chama cha Wananchi CUF. Kwa hivyo, hawa sheria itawasukuma kufanya shughuli zao za kisiasa pindipo mswada huu ukipita kuwa sheria.

Mhe. Spika, pendekezo la mswada huu ni kuwa hii ruzuku haitazidi asilimia moja ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya kila mwaka, inaweza ikapungua sijui mpaka *zero point* ngapi, lakini haiwezi ikawa zaidi ya moja. Kwa maana hiyo, hapa kuna siri ndogo iliyojificha na wala hatujui huku chini itakuja mpaka *zero point* ngapi, lakini haitazidi asilimia moja. Kwa kweli kwa vyovyote serikali inayo nia baada ya marekebisho haya kutoa hiyo ruzuku.

Mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati inayotokana na serikali kwanza nitakuwa mtu wa ajabu kama sikuyaunga mkono haya mapendekezo ambayo mimi mwenyewe nilishiriki kuyafanya. Kwa hivyo, nikubaliane kuwa twende katika asilimia 20, 50 na 30 kama tulivyopendekeza, yaani pale kwenye urais 20, uwakilishi 50 na serikali za mitaa kwa sisi tunaita udiwani ni asilimia 30. Sasa wale ambao wanashiriki katika resi hizi na ikawa kwa bahati mbaya hawakufanikiwa kupata chochote ama urais, uwakilishi au udiwani, basi natoa wito wakaze buti waongeze kuhubiri siasa, ili wakubalike na wao waweze kuingia katika kupata hizi ruzuku, kwa sasa ruzuku zitawanufaisha au itavinufaisha vyama viwili ambavyo vina uwakilishi.

Kutokana na hali hiyo, hadi hapo ambapo mswada huu ukipita basi hapo baadaye inaweza kufanyiwa marekebisho kuviwezesha vyama ambavyo kama vitafanikiwa asilimia fulani ya kura hata kama havikushinda basi viweze kupata ruzuku.

Mhe. Spika, fedha hizi kama walivyosema wengi zinatokana na kodi za wananchi wetu na kila mtu anao mtazamo wake. Kwa mfano, mimi nadhani wapiga kura walio wengi wanazidi asilimia 30 kama tutafanya mahesabu ya kura alizoshinda urais wa CCM ambaye ndiye Rais wa nchi hivi

sasa na kura alizopata Mhe. Makamo wa Kwanza tukazijumlisha na tukazifanyia asilimia ya *total votes* zote, basi hizi nadhani zinazidi asilimia 80, yaani alizopata Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Kwanza tukizijumlisha na tukatizama ni wapiga kura wangapi walioshiriki katika chaguzi hizi, basi bado hii asilimia yao itakuwa ni kubwa kuliko vile vyama vyengine vyote.

`Lakini kwa mtazamo wangu mimi nadhani kama ni sahihi ni sawa na kama si sahihi nitakuja kufanya marekebisho huko baadaye. Kwa maana hiyo, lakini nahisi kuwa kwenda hapa itakuwa imekwenda kwa *voters* wengi zaidi kuliko vile ambavyo pengine wengine tunayo mawazo kwa wapiga kura sisi wachache tu ambao tutanufaika na wengi hawatanufaika tukichukulia wapiga kura na wala si wazanzibari wote tukichukulia wapiga kura.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo haya mafupi tena machache niseme mimi naunga mkono hoja au mswada huu na ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii kuendelea kuturuzuku neema zake, ikiwemo neema ya uhai na uzima tukamudu kusimama hapa kufanya kazi zilizotuleta hapa, ambapo ni kazi ya kusimamia masuala yanayohusu wananchi wa Zanzibar.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache katika mswada huu, na tatu Mhe. Spika naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na serikali kwa jumla kwa kuleta mswada huu na kuona haja ya kufanya marekebisho katika sheria hii Nam. 6 ya mwaka 1997 inayohusu ruzuku kwa vyama vya siasa. *(Makofi)*

Kwa hali ya kawaida Mhe. Spika, tungetegemea tusiwe na mjadala tena pengine ungetuhoji tu na kupitisha mswada huu, kwa sababu mswada wenyewe hata huo wa asili si mkubwa na haya marekebisho yake ndio kabisa yamegusa vifungu zaidi viwili.

Lakini nimeshawishika Mhe. Spika na mimi kusema machache hasa baada ya kusikiliza mjadala unavyokwenda nadhani kuweka kumbukumbu vizuri, vile vile nadhani hata kwa wananchi ambao tunaowawakilisha hapa wanaotusikiliza kupitia vyombo vya habari basi na wao waweze kulielewa.

Mhe. Spika, swali la kwanza kabisa la kujiuliza ni kwamba nini msingi wa serikali kuvipa ruzuku vyama vya siasa katika nchi mbali mbali duniani. Kwa kweli dhana hii Mhe. Spika imekuja katika nchi tofauti ili kuepusha uwezekano wa vyama vya siasa ambapo sote tunajua kwamba ni taasisi muhimu sana katika nchi, kwa sababu ndizo zinazokwenda kwa wananchi kuomba ridhaa ya kuongoza nchi.

Kwa hivyo, ilikuwa ni dhana ya kuvipa ruzuku imelenga kuvinusuru kuja kugeuka wakala wa wanaovifadhili. Mhe. Spika, kuna usemi maarufu unaosema kwamba *anayekufadhili ni bwana wako*. (*Makofi)*

Sasa kwa khofu hiyo ilionekana kwamba ikiwa vyama vya siasa havipewi ruzuku ya kujiendesha kutokana na fedha za wananchi wa nchi husika, basi upo uwezekano kwa sababu vinahitaji gharama za kujiendesha vikatafuta vyanzo vyengine vya fedha na hao wanaovipa vyanzo vya fedha wakavitumilia vyama vya siasa kwa maslahi yao na huo ndio msingi wa vyama kupewa ruzuku kutokana na fedha za walipa kodi.

Maana yake nini Mhe. Spika, kwamba madamu vinaendeshwa kwa fedha za walipa kodi, basi bwana wake watakuwa ni walipa kodi ambao ni wananchi wa nchi ile, kwa hivyo vitawatumikia wananchi wa nchi husika. Kwa hivyo, hiyo ndiyo dhana yenyewe Mhe. Spika.

Dhana hiyo haiwezi tu ikawa imefungua milango kwa yeyote mwenye kuanzisha chama akasema apewe fedha za walipa kodi. Waheshimiwa Wawakilishi hapa wametoa uzoefu wao wengine katika usajili wa vyama vya siasa sote kwa namna moja au nyengine tulishiriki huko nyuma, kweli ni kazi ngumu.

Lakini Mhe. Spika kusajili na kufanikiwa kuupata usajili wa chama cha siasa haiwezekani ikawa yenyewe ndio sifa ya kupewa ruzuku, kwa sababu binadamu tuko watu wa khulka tofauti. Kwa mfano, kuna watu wanaweza kuanzisha chama cha siasa kwa sababu tu ya kuamini kwamba kuna maslahi kama haya kwani kuna ruzuku ataipata. Sasa msingi wake ni kwamba unatokana na matokeo ya uchaguzi ni nini.

Mhe. Spika, kwenda katika uchaguzi katika vipindi tofauti kwenye nchi yoyote ile ni utaratibu uliojengwa, ili kuipa uhalali serikali kwamba imepata ridhaa ya inaowaongoza, na kwa nchi kama zetu ambazo bado hazijaruhusu mgombea binafsi, basi bado vyama vya siasa ndivyo vinavyotumika kutupatia wagombea na msingi wake ni kwamba hivi navyo vipate ridhaa ya wananchi.

Sasa ruzuku inapofungamanishwa na kura au ridhaa ya wapiga kura inalenga kuhalalisha kwamba wewe unapewa ruzuku kwa sababu wewe wananchi wamekukubali. Kutokana na hali hiyo ndio maana ni utaratibu wa kawaida wa nchi nyingi sana nadhani ni chache zilizobakia zenye mfumo tofauti kwamba uwiano wa kura au wa viti katika nafasi za kuchaguliwa ndio unaotumika katika nchi mbali mbali kutoa ruzuku kwa vyama vya siasa, ambavyo vimepata uwakilishi katika chombo kinachohusika.

Mhe. Spika, sote humu tunajua kwamba dhana ya kuwa na bunge na kwa maana hiyo nakusudia hata Baraza la Wawakilishi ni bunge kwa maana ni chombo cha kutunga sheria.

Dhana ya kuwa na bunge katika historia ya nchi ya Uingereza ambako ndiko dhana hii ilikojitokeza hasa, ilianzia na wananchi hasa walipa kodi na wakati huo wakiitwa *barons* wale waliokuwa mabepari wakilipa kodi, walipodai uwakilishi kwamba haiwezekani tukalipa kodi halafu ikawa mfalme ndiye mwenye maamuzi ya kila kitu katika kuendesha nchi. Kwa hiyo lazima tuwe na chombo ambacho sisi walipa kodi tunawakilishwa, ili sisi tuibane serikali katika uendeshaji wa hizo kodi zetu ndio msingi mzima wa kuanzishwa mabunge tangu Uingereza mpaka huku kwetu.

Sasa ndipo ulipokuja ule usemi kwamba walipoanzisha wao waliposema '*No taxation without representation*', kwamba kusiwepo na kulipa kodi ikiwa hakuna uwakilishi.

Kwa hivyo, naeleza yote haya Mhe. Spika kwa sababu nataka kujenga hoja kwamba kwa chombo hichi leo kuletewa sheria hii ni pahala pale, lakini zaidi kwamba sheria hii imeweka utaratibu kwa haya marekebisho yanayofanyika kuwe na fungu la fedha katika bajeti ya serikali ambalo halitazidi asilimia moja ya bajeti hiyo, ambalo litakuwa ni ruzuku kwa vyama vya siasa.

Kwa maana hiyo, ile kwamba chombo hichi ndicho kitakachoamua Mhe. Spika, kwamba Baraza la Wawakilishi katika kupitisha bajeti ya nchi au ya serikali kwa kila mwaka ndio itaamua kiasi gani, almuradi isizidi asilimia moja ikiwa marekebisho haya tutayapitisha ni pahala pake, kwa sababu chombo hichi ndicho kinachowasimamia wananchi kwenye hizo kodi katika nchi yetu. Mhe. Spika, naipongeza serikali kwa kuona umuhimu wa marekebisho haya na kuzingatia vigezo ambavyo kidogo kidogo vinatupeleka kule ambako dunia inaangalia katika kutoa ruzuku.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya kwanza nataka nisifu hii hatua ya kufanya marekebisho katika kifungu cha tatu cha sheria mama inayorekebishwa. Kwa kweli kifungu hichi ukikisoma kilivyo kabla ya marekebisho haya ambayo hatujayapitisha au kama kilivyo kama hivi sasa, kilikuwa kikisomeka kwamba serikali itatenga si chini ya asilimia moja, maana yake ianze asilimia moja kwenda zaidi.

Sasa hii kwa nchi masikini kama yetu Mhe. Spika mimi nataka nikubaliane kabisa kwamba ilikuwa sio tu kuwatendea haki walipa kodi, lakini na utekelezaji wake unakuwa mgumu hasa ukilinganisha mapato, haidhuru kuwa Mhe. Mjumbe mmoja alizungumzia kwamba mapato yanaongezeka, sawa na kama yanaongezeka basi kwanza yaende kuwahudumia wananchi katika huduma muhimu.

Kwa hivyo, nasema haya marekebisho aliyoleta Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwamba sasa turekebishe tuseme hapana isizidi asilimia moja mimi nayapongeza sana, kwa sababu inaweka uhalisia wa mambo kwa nchi masikini kama yetu.

Lakini nani wataamua ni sisi Baraza la Wawakilishi ndio tunaopitisha bajeti, kwa hiyo bado wananchi ambao ndio wenye kulipa kodi watakuwa wanaamua kupitia Wawakilishi wao katika chombo hichi na hilo nalipongeza sana Mhe. Spika.

Jambo jengine Mhe. Spika, pia napongeza kwamba sheria ile namna ilivyokuwa pale mwanzo na sote tunakumbuka ilipitishwa katika zama ambazo tulikuwa na mivutano mikubwa sana, yaani ungeweza kuita ilikuwa ni *arbitrary* kidogo. Lakini hatimaye chini ya mfumo huu mpya wa mashirikiano tulioujenga serikali imeona kuna haja ya kuwa na marekebisho. Vile vile tunakumbuka kwanza uliletwa hapa kama ni sehemu *miscellaneous amendment* na serikali ikaona mantiki na busara kuondosha, ili ikafanyiwe marekebisho zaidi na hatimaye umeletwa hivi.

Mhe. Spika, mimi zaidi nataka pamoja na kuipongeza serikali kwa kuja na fomula hii, pia niipongeze na Kamati nayo kwamba Kamati ya Kudumu ya Baraza lako Mhe. Spika ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeona bado ina haja ya kufanyiwa

marekebisho, ili kama ulivyosema fomula inayowekwa au vigezo vilivyowekwa viwe vinakwenda sambamba na jinsi nchi za wenzetu duniani zinavyokwenda na bado hatujafika, lakini mabadiliko ni hatua, na hapa ilipopendekezwa pia ni hatua kubwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika nimefurahi na marekebisho ya kamati lakini nataka niipongeze serikali pamoja na Mhe. Waziri kwamba katika kuwasilisha mswada huu ameshatamka pale kwamba yeye kwa niaba ya serikali bila ya shaka ameyapokea na ameyakubali mapendekezo ya Kamati na hata alipowasilisha hapa alisema anayaunga mkono.

Sasa nikisema hivyo si kama sizielewi hisia kama alizozizungumza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chonga na wengine waliosema kwamba tuzingatie uwiano wa kura za Rais hasa kwenye kifungu hichi kimoja na katika nchi za wenzetu ndivyo ambavyo ingekuwa. Lakini ninachowaomba wenzangu kama nilivyosema kwamba hapa ilipofikishwa pia ni hatua kwa nchi kama yetu kwa huko tulikotoka.

Mhe. Spika, mimi nataka kuwaomba Wawakilishi wenzangu wote kwamba wale wanaosema twende hivi na vile, basi sote tuache tofauti na hii hatua iliyofikiwa pia si ndogo tuukubali mswada huu, ili tuweze kuupitisha na kuunga mkono.

Jambo la mwisho kabisa Mhe. Spika kuna kitu amekizungumzia Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Wawi Mhe. Saleh Nassor Juma nataka nikiunge mkono, kwamba ametoa pendekezo kuwa kuna haja pengine siku za mbele serikali itakapofanya marekebisho, lakini hata sasa kwa sababu hizi ni fedha za walipa kodi na hata kama sheria haisemi hivyo.

Kwa kweli kuna haja katika kujenga dhana ya utawala bora kwamba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali awe anakagua matumizi ya fedha hizi ambazo ni za walipa kodi na wala halina wasi wasi.

Suala hili Mhe. Spika tutakuwa tunakwenda sambamba na hata hiyo sheria mama kwa maana kwamba mpaka hivi sasa vyama vya siasa ni suala la muungano na vinaandikishwa katika Jamhuri ya Muungano. Sasa hata katika Jamhuri ya Muungano tunakumbuka kwamba yamefanywa marekebisho katika ile sheria Nam. 5 ya vyama vya siasa mwaka 1992, ambapo sasa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kukagua matumizi ya fedha zile za ruzuku kwa vyama vya siasa.

Sasa kama hiyo inafanyika kwa fedha ambazo zinatoka kwenye Hazina ya Jamhuri ya Muungano kwa ngazi ya taifa, basi naamini pia na kwa ngazi ya taifa la Zanzibar katika hii ruzuku kwamba inatolewa hapa, basi ni sahihi kabisa hata kama sheria haitamki hivyo kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, kwa sababu kwa *mandate* yake aliyonayo hahitaji hata kutamkiwa ndani ya sheria, almuradi kwamba hizo ni fedha za walipa kodi, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anayo haki ya kuzikagua.

Kwa hivyo, nadhani katika kujenga misingi ya uwazi, uwatala bora pia kuona kwamba fedha hizi hazitatumika kwenda kufanyia shughuli nje zilizokusudiwa za maslahi ya umma katika kuwatumikia walipa kodi ambao wanatumikiwa na vyama hivi basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu aweze kupitia hesabu hizi na kujiridhisha kwamba zimetumika ipasavyo.

Baada ya kusema maelezo haya Mhe. Spika na kama walivyosema wenzangu kwamba mswada huu si mkubwa maelezo yake, maoni pamoja na madhumuni yake yanafahamika kirahisi na Mhe. Waziri ameeleza kwa ufasaha hapa na Kamati pia imekuja kufafanua pamoja na kuongezea ufafanuzi kwa ufasaha.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe walionipa heshima na ridhaa ya kuja hapa, lakini naamini kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar kwa jumla niseme naunga mkono mswada huu na naomba tuupitishe kwa sauti moja. Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na kuweza kujadili mambo yetu kwa maslahi ya umma. Vile vile nikupongeze wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi fupi ambayo nataka kutoa mchango wangu kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri kwenye mswada wake huu ambao ametusomea hivi punde. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ujumla mswada tumeuelewa na kwa kweli Mhe. Waziri anajitahidi kufanya wajibu wake, na inaonekana wazi kwamba amedhamiria kupanua demokrasia na kutoa usawa katika mashindano ya kisiasa.

Lakini Mhe. Spika, ni vyema tukatambua kwamba nchi hii si ya CCM na CUF peke yao ni nchi ambayo imeruhusiwa demokrasia ya vyama vingi na kwa msingi huo kuna haja ya siku za mbele kutambua uwepo wa vyama vyengine kwa ajili ya kupata fursa sawa katika mbio hizi za kugombania uongozi wa kisiasa.

Kwa hivyo, pamoja na hatua ya kutoka huko tunakotoka ambao ilikuwa ni asilimia hamsini kwa ngapi na leo Mhe. Waziri ametuletea asilimia 20. Kwa kweli mimi nasema ni hatua kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni hatua nzuri. Lakini kwa busara hizi Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Waziri afikirie kuwapa fursa wenzetu ambao si CCM wala CUF kuingia kwenye ushindani katika mbio hizi za urais.

Kwa nini Mhe. Spika nikasema hivyo, nasema hivyo kwa sababu tumeshuhudia mara kadhaa vyama vyetu vya kisiasa vyengine vimeshindwa hata kuweka mawakala katika kugombania nafasi hizi za urais na uwakilishi. Kwa maana hiyo, ni jambo la busara sana Mhe. Spika, katika msimamo huu wa utawala bora na umakini wa Mhe. Waziri kuzingatia suala zima la kuwapatia fursa wenzetu katika siku za mbele hasa katika nafasi hizi za juu za urais.

Mhe. Spika, huo ulikuwa ni ushauri wangu. Lakini hoja yangu ya msingi kwenye mswada huu ile ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliyomalizia ambayo alianza kuizungumza Mhe. Saleh Nassor Juma kuhusu suala zima la ukaguzi wa fedha ambazo watapatiwa wanasiasa.

Mhe. Spika, fedha hizi ni fedha ambazo Baraza la Wawakilishi wataidhinisha na kwa msingi huo ni fedha za umma ambazo zinatokana na michango pamoja na kodi za wananchi wetu.
Kwa hivyo, sheria ya mwaka 1997 kwa habati mbaya sijaipitia sijui kama kimo kifungu hicho, lakini kama hamna kifungu hicho basi Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi mazima aongeze kifungu kipya ambacho kitamuwezesha *CAG* kukagua fedha hizi, kwa nini,

kwa sababu fedha hizi ni za wananchi na imeidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, kwa hiyo lazima Baraza la Wawakilishi lipate kwenda kukagua matumizi yake na wala hatuwezi kufika huko kwa maana ya *PAC* bila ya kukaguliwa na *CAG*.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana tena kwa heshima kubwa na busara za Mhe. Waziri kwamba akubali kuongeza kifungu maalum cha mswada huu, ili *CAG* apate nafasi ya kwenda kukagua fedha hizi na hatimaye *PAC* iende moja kwa moja kutupa taarifa za matumizi ya fedha hizi na wananchi wa Zanzibar wapate taarifa zake.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika tukisema kwamba tuache wazi wazi tu na *CAG* tumuachie kwa sababu ni mtu makini pengine atakwenda sheria haitasema hivyo na wala hatapata fursa ya kwenda kukagua fedha.

.

Mhe. Spika, lazima nimuombe Mhe. Waziri tuongeze kifungu kipya kwa ajili ya kumuwezesha CAG kukagua ili na hatimaye PAC iende kujiridhisha kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi na wananchi, matumizi halisi ya fedha hizi za umma.

Baada ya hapo Mhe. Spika, Mhe. Waziri naamini atanikubalia tuongeze kifungu hicho na kwa msingi huo nitaunga mkono Mswada huu mia kwa mia. Nakushukuru sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi nikaweza kutoa mchango wangu katika suala zima ambalo linatukabili mbele yetu juu ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kuishukuru wizara ambayo imejitahidi pamoja na Waziri ambaye ameweka kitu hichi ambacho ni muhimu kwa ajili ya maslahi yetu sote na kwa maslahi ya wananchi. Namshukuru waziri amejitahidi katika kuweka mambo wazi kabisa ili tujue nini la kufanya baadaye. Lakini hata hivyo nachukua nafasi hii kuishukuru kamati ambayo iliyokaa kitako ikapitia hii sheria na ikaweza kutoa maoni yake.

Mhe. Spika, sheria hii si ya leo, sheria hii ni kongwe, ni ya zamani sana, tangu mwaka 1997. Niishukuru wizara kwa kusema kweli. Hili ni jambo la msingi maana watu wengi si rahisi kusema kweli. Lakini wizara kipindi chote hicho kuanzia mwaka 1997 serikali ilishindwa kuweza kulitekeleza suala hili kama linavyotakiwa. Wametoa sababu kwa nini wakasema hivyo. Wametoa sababu kwamba kutokana na hali ya uchumi hili suala limeshindikana. Katika nchi yetu inategemea namna gani uchumi wetu unavyokua. Baadhi ya wakati tunapata uchumi mzuri na baadhi ya wakati uchumi unakuwa mbaya.

Lakini hata hivyo ikaonekana kwamba fedha kuzitoa kwa wakati huo ilikuwa ni ngumu sana kutokana na hali ya uchumi. Kwa hivyo naishukuru wizara kuweza kukiri kwamba wameshindwa kuitekeleza na ni muda mrefu. Lakini kutokana na hii sheria ambayo ni sheria kuu, mkaweza kuleta haya ni marekebisho ambayo yanatokana na sheria kuu kwamba baadhi ya vipengele hapa viweze kuangaliwa kwa vizuri zaidi.

Tunachokizungumzia hapa ni suala zima la ruzuku kwa ajili ya vyama vya siasa. Mimi nataka niseme tu kwamba hiyo ruzuku si kwa vyama vya siasa tu lakini serikali imejikita kutoa ruzuku si kwa vyama vya siasa tu. Kuna sekta mbali mbali serikali inatoa ruzuku kuipa, tunaziona hapa,

tofauti na ile kawaida ya mawizara. Kwa hivyo suala la kutoa ruzuku ni suala ambalo serikali mara nyingi inazisaidia taasisi mbali mbali katika kuendesha mambo yake na kufanya mambo yake kwa njia ya kujitegemea.

Kwa hivyo hapa wizara imeona ni suala muhimu kwamba navyo hivi vyama vya siasa vipate ruzuku ili kuviwezesha hivi vyama vya siasa viweze kujiendesha. Kwa sababu kila mtu anapofanya kazi ikiwa hana mtaji wa kuendeshea chama si rahisi au kuendeshea kitu chochote. Hata wewe ukitaka kufanya biashara ukiwa huna mtaji huwezi kufanyabiashara. Jambo lolote kama huna pesa, huwezi kufanya kitu chochote.

Kwa hivyo, hapa hii ni ruzuku inatolewa, ruzuku ni kitu kidogo tu na sio kitu kikubwa sana. Ni ruzuku ambayo angalau kuweza ku – *motivate* ile *interest* ya vyama kwamba na wao wagaiwe chochote kutoka serikalini. Mimi nafikiri ni jambo zuri kabisa, lakini pia naishukuru Wizara kwa kujikita inasema isizidi kuliko asilimia moja, lakini si chini ya zaidi ya asilimia moja.

Hapa katika Mswada huu imejikita kwenye asilimia moja, ni kuonekana hali ya fedha ambayo serikali ingeweza kupata na kuweza kuwasaidia hivi vyama vya siasa. Kama serikali itakuwa *very serious* itajikita kisawasawa katika mambo yake ya uendeshaji wake na mipango yake mimi nafikiri ikikubali kufanya kitu hicho ijikubalishe kukitoa kile kitu. Hii ruzuku itolewe kihalali katika vyama vile ambavyo vilivyotoa masharti yake.

Katika ruzuku hii bila shaka kumetolewa masharti maalum kwamba kila chama kiweze au kitakachopata kwenye kiti cha Urais kwa asilimia zake. Hapa tumeona kwenye asilimia 25. Halafu tumeona vile vile hapa katika masharti mengine ya majimbo ambayo yaliyoshinda. Hii ni sehemu ya pili, sehemu ya kwanza ni sehemu ya Rais, sehemu ya pili inakwenda kwenye majimbo na sehemu ya tatu imejigawa kwenye wadi za majimbo yale.

Mimi nafikiri inategemea uwiano kama hapa ilivyozungumziwa uwiano wa idadi ya wadi katika jimbo, hilo si jambo baya. Lakini sasa ukitizama kwa pande zote, mimi hapa kidogo nilitaka tufanye uangalifu mkubwa sana, kuanzia kwenye kiti cha urais, tungeingia kwenye majimbo, tunajua hapa tupo katika majimbo mangapi. Majimbo haya yote hapa katika Baraza la Wawakilishi, Chama gani kilichoshinda kutokana na majimbo yale.

Kwa hivyo, utakuta hii ruzuku ime-*stands* kwenye rais aliyeshinda ambaye kwa haraka tunajua nani aliyeshinda katika kiti cha urais, kwa hiyo ile ruzuku inakwenda kwa rais. Wakati wa pili ruzuku ile ile itakwenda kwenye majimbo ambayo tunayo hapa katika Baraza la Wawakilishi. Majimbo yote tunayo hapa na tunajua majimbo gani ambayo yameshinda. Ruzuku ile itakwenda kwenye majimbo yake.

Lakini la tatu vile vile ambalo tunatakiwa tuwe na uangalifu, tuangalie ruzuku ya tatu inakwenda wapi, itakwenda kwenye Wadi ambayo ipo katika majimbo yale. Sasa ukitathmini yote kwa jumla utaikuta ruzuku yote hii imeelemea upande mmoja.

Mimi ningefikiria kidogo hapa tungeangalia namna gani mshindi wa kwanza na mshindi wa pili anavyoweza kupata ruzuku hii na iweze kumsaidia zaidi. Kwa sababu hapa ukitizama wadi hana, majimbo hana, uraisi hana, kwa hivyo ruzuku yake itakuwa ni ndogo sana. Mimi ningefikiri

kuweza ku- *motivate* hivi vyama kwa upande mmoja. Wangefikiria kwa upande wa kile chama ambacho kilichokuwepo chini yake kikaweza nacho kupata ruzuku kubwa zaidi kwa mtazamo mwengine zaidi ya mtizamo huu wa (a) Rais (b) Majimbo (c) Wadi. Utazikuta ruzuku zote zinaingia upande mmoja bila ya kufikiria upande mwengine, kwa sababu ushindi hakuna kwa upande wa pili. Kwa hivyo ruzuku yake itakuwa ni ndogo sana.

Kwa hivyo nafikiria hapa Mhe. Waziri aweze kufikiria zaidi kwenye hilo suala, aka *access* zaidi kwenye utoaji wa asilimia 25, asilimia 50 na asilimia 25 hapa angeweza kufikiria zaidi. Hii imekuja *percentage wise* lakini *percentage* hii yote ikikuswanywa pamoja ni 100%. Utakuta zote hizi asilimia zinaelemea upande mmoja. Kwa upande wa pili asilimia hii itakuwa ni ndogo sana. Kwa hiyo mngeifikiria hapa kidogo Mhe. Waziri si vibaya hivi alivyoileta lakini uki–*put in to consideration* utakuta hii fedha yote ya ruzuku inaelemea upande mmoja bila ya kufikiria upande wa pili.

Mimi nafikiri cha msingi ambacho katika ruzuku hii kama ilivyokwenda si vibaya lakini pia na serikali iwe *serious* katika kuangalia kuzipata kwa wakati wake ambao unaotakiwa.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kwamba fedha hizi zinatokana na kodi za wananchi. Wananchi ndio wanao *struggle* chini ili kuweza kuvisaidia vyama hivi vya siasa. Sasa wananchi na wao wana haki juu ya haya tunayoyazungumza hapa, wananchi wanayasikia yote haya. Lakini tukiangalia fedha hii ambayo itapatikana wanajua kama fedha hii nyingi inakwenda upande mmoja zaidi kuliko upande wa pili. Vile vile cha msingi kuangalia fedha hii iwe na uangalifu na iwe na usimamizi mzuri kwa fedha hizi za serikali ambazo zinatolewa kwenye vyama mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa kuwa waraka huu ni marekebisho tu kutokana na waraka mkuu, haya ni sehemu tu ya marekebisho katika waraka ule mkubwa. Kwa hivyo hauna mazungumzo makubwa sana ya kuendelea kuchambua zaidi ya haya ambayo tunayaeleza, sidhani kama kutakuwa na mengine zaidi. Kwa hivyo Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kuweza kunipatia nafasi angalau na mimi kuweza kutoa mchango wangu katika haya. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru, naunga mkono.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi adhuhuri hii kunipatia fursa ya kuzungumza machache kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Lakini kabla ya yote na mimi ningependa kumuomba Mwenyezi Mungu akaujaalia mwaka huu ambao tumeuanza siku 15 zilizopita ukawa na kheri na baraka kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, tunajadili Mswada ambao upo katika nchi hii miaka karibu 6, 7 iliyopita nyuma. Lakushangaza ni kwamba Mswada huu miaka yote hiyo haujatekelezeka. Moja katika sababu ambazo tuliambiwa humu ni kwamba ilikuwa fedha ni kidogo. Ninachokijua mimi bado fedha hizo ni kidogo hadi hii leo. Kwa sababu nchi ina mahitaji mengi na mengine ni muhimu zaidi.

Juu ya hayo ni kwamba hivi sasa katika nchi hii vyama vya kisiasa vimo katika mfumo wa muungano. Imani yangu kwamba ruzuku inatolewa katika mfumo huo wa muungano. Sasa sijui kulikuwa na sababu gani zilizopelekea kwamba nchi yetu nayo ikajiingiza katika kutoa ruzuku kwa vyama vya siasa jambo ambalo linatekelezwa na Serikali ya Muungano na hasa tukitilia

maanani kwamba keki yetu ni ndogo mno iliyofanya kwamba miaka yote iliyopita suala hili limeshindwa kutekelezeka.

Mhe. Spika, sisi tumo katika mfumo wa vyama vingi hivi sasa. Mfumo huu lengo lake ni kuleta demokrasia na utawala bora. Mpangilio ulioletwa katika ugawaji wa ruzuku hii nina wasi wasi nao kwamba hapo baadae utatufikisha katika yale malengo ya kuleta mfumo wa vyama vingi ukaondoka. Waswahili wanasema na hata sayansi inakubali kwamba ule mti ambao unapata maji kwa wingi basi ndio unaomea zaidi. Kama sisi tutaruhusu kwamba leo kile chama ambacho kitatoa Rais basi kipewe asilimia 20. Mimi nafikiri itakuwa tunakipa nguvu chama hichi na uwezekano wa kwamba kiondoke katika madaraka basi utakuwa mdogo mno. Kwa sababu hichi kitakuwa kina uwezo wa kujiendesha na kujipalilia kwa kila hali kiasi kwamba kuimarika kwake hakutokuwa sambamba na vile vyama vyengine vilivyokuwepo chini. Lile lengo la kwamba sisi tunataka kujenga demokrasia basi litaondoka. Mimi nahisi kwamba kama tuna nia ya kwamba tunataka kuleta demokrasia iliyo ya kweli basi mfumo wa mgawanyo wa ruzuku hii tungeuangalia upya.

Mimi sioni sababu ikiwa Rais yeye anapewa asilimia 20. Ikiwa tulikuwa kweli na imani ya kwamba tunataka kujenga, kweli Makamo wa Rais ambaye ni msaidizi kama tulivyosema hapo katika maswali na majibu asubuhi, basi na yeye asionekane kwamba angalau akawekewa asilimia tano. Kila nikiiangalia sheria hii mimi naifananisha kama na zile *side mirror* za gari kwamba mara nyingi zile ziko mbele ya gari lakini kazi yake kubwa huwa inamsaidia dereva kuangalia yaliyokuwepo nyuma sio yaliyokuwepo mbele. Mfumo uliokuja unaashiria hivyo, hauashirii kwamba tunalengo la kuimarisha demokrasia na utawala bora.

Hivi sasa ninavyojua mimi Mhe. Spika, tumeondokana na ule mfumo wa *Government of opposition* tumeingia katika mfumo ambao sijui tunauita vipi kwa kiingereza lakini ni mfumo wa maridhiyano. Sasa kumpa mmoja keki kiasi kama hichi wengine ukawaona wao labda hawaridhiki. Mimi nafikiri si jambo la busara, tungekuja na mfumo ambao hatutokuwa kama vile wa *side mirror* ikawa tunaangalia nyuma zaidi, tunataka tuangalie yaliyokuwepo mbele zaidi. Mimi naomba hii asilimia 20 iliyowekwa kwa ajili ya chama kimoja tu basi ni choyo. Choyo mara nyingi huwa kinazaa mambo mengi, sasa ili yasije yakazalika haya basi tuangalie upya huu mgawanyo.

Kama sheria hii ilikuwa haitekelezeki miaka hiyo mingi iliyopita nyuma na kutekelezwa kwake kutakuwa na marekebisho, nina wasi wasi kwamba kila tukimaliza uchaguzi basi tutakuwa na marekebisho mengine. Kwa sababu ya kuwa mwanadamu kaumbwa na choyo mara tu utakapomalizika uchaguzi atakaekuja yoyote basi na yeye atasema aaa kwa vile fulani alikuwa yeye anapata asilimia hii kwa nini na mimi nisiunde sababu ya kufanya Mswada huu niurekebishe ili na mimi niongeze zaidi kwa sababu ya kuimarika kwa chama chake.

Lengo mimi nafikiri si kuimarisha chama kama nilivyosema mwanzo. Kwa sababu chama kinaweza kikachukua fedha kikenda kikajenga matawi, ikanunua magari ya kutembelea, lakini lengo ni kuleta demokrasia na utawala katika nchi yetu. Mgawanyo unatuonesha kwamba hili sio lengo, lengo ni kuzipeleka tu pesa lakini sio kujenga hayo. Mimi ningemuomba Waziri akaona haja hiyo kwamba tusiangalie yale mambo kama niliyoyasema tunayoyaona katika *side mirror* ya kuangalia nyuma zaidi, tuangalie ya kujenga zaidi.

Mhe. Spika, ulituusia sana hapa wakati wa kufunga kikao chetu cha bajeti mwaka huu na ukatutaka sote tuwe ni *mas-ul*, kwamba tutawajibika na tutakuwa na dhamana. Sasa haya mimi bado nayakumbuka mpaka leo. Kama alivyosema Mhe. Hija Hassan Hija, pale kwamba lengo sio kuwafaidisha vyama viwili, lengo ni kuwasaidia wananchi katika nchi yao na hasa kuleta utawala bora. Hii fedha itakayotumika inatokana na jambo la kila mwananchi. Wanayo haki na wao wote waliokuwemo katika mchi hii kuitumia fedha hii.

Mhe. Spika, katika matembezi yangu ulimwengu huu mimi nilibahatika kutembelea nchi moja ambayo wenyewe wanajiita ni *Ummu duuniya* wale wa Misri kwa jina jengine tunawaita Egypt. Kwa kukumbuka yale uliyotuwaidh, wakati wa kufunga kikao cha bajeti ikabidi nifanye utafiti kidogo katika vitabu vyangu. Nikakumbuka wakati wa kutembea katika nchi ile niligundua barabara moja wameandika bangoi kubwa naomba uniruhusu niseme vile lile bado walivyoliandika. Mimi ilinipa hisia fulani. Wameandika kwamba:

Mzuri wa mwanzo katika ulimwengu huu na dini yetu ya Uislamu imemtaja pengine na dini nyengine ni Nabii Yusuf, wao wanasema alizaliwa pale Misri lakini pia alikufa pale. Tajiri mkubwa aliyetajwa na vitabu vya dini yetu ni Karun alizaliwa pale na akafa pale hayupo. Mkorofi mkubwa katika ulimwengu ambaye katika vitabu vyote vimemtaja na watu wengi katika ulimwengu wanakwenda kumuangalia ni Firauni, na yeye kazaliwa Misri na kafa pale. Lakini mwisho wameandika kwa lugha yao ya kiarabu katika lile bango *"Ayna hum?"* Wako wapi hao?

Naomba nimalizie hapo Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, name nikushukuru kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia sote tukawa ni wazima wenye afya na tukaweza kushiriki kikao hichi. Lakini zaidi tukaweza kuuona mwaka huu wa 2013, tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu atujaalie afya na uhai ili tuzidi kuiona miaka mengine ijayo mbele yetu. Mwenyezi Mungu aujaalie mwaka wa 2013 uwe ni mwaka wa neema ni mwaka wenye amani na utulivu, kadhalika ni mwaka ambao uwazidishie Wazanzibari Mashirikiano na umoja miongoni mwao pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Mhe. Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia mawili matatu yanayohusiana na Mswada huu ambao ni muhimu. Kwanza niipongeze serikali kwa kuwasilisha Mswada huu kwa wakati huu. Pamoja na kwamba Mswada huu yaliyoletwa ni marekebisho lakini kwa kweli marekebisho haya yamekuja katika wakati ni mwafaka sana kwa vile tukijaaliwa mwaka wa 2015 taifa letu litashuhudia uchaguzi mwengine katika nchi yetu.

Mhe. Spika, umuhimu wa Mswada huu wa kuviruzuku vyama kuna umuhimu mkubwa, hususan kwamba inatakiwa kuandaliwe mazingira kwamba vyama vinapoingia katika ushindani na inapaswa kuwe na ushindani ambao una afya, kuwe na ushindani ambao unaweza kuviwezesha vyama vyote hivi kuweza kuingia kwenye ushindani na hatimaye kile ambacho Wazanzibari watakiunga mkono hatimaye kiweze kukamata hatamu za dola katika mfumo ambao wenyewe wameukubali wa kuwa na serikali ya umoja wa kitaifa.

Mwaka 2013 takriban tunashuhudia tunakuwa tumo kwenye uzoefu zaidi ya takriban zaidi ya miaka 20 tangu tuanzishe mfumo wa vyama vingi. Katika kipindi hiki cha miaka 21 tumeshuhudia kwamba uzoefu unaonesha kwamba kuna vyama ambavyo vimeonesha umakini katika uwanja huu wa kisiasa. Lakini kuna vyama vyengine vimedhihirika kwamba vimekuja kwa lengo au vimeundwa kwa lengo la ubabaishaji na kutafuta ruzuku. Inatosha sasa kwa wanaohusika wafanye kazi ili huu utitiri wa hivi vyama tulivyonavyo na ambavyo vyenginevyo kwa kweli haviko makini katika kufanya siasa. Ni vyema Afisi ya Msajili iweze kufanya kazi na ikiwezekana vyama hivi baadhi yao vipunguzwe ili vibakishwe vyama vichache ambavyo ndivyo vinavyoweza kuingia katika uwanja huu wa siasa na kufanya siasa.

Kuwa na vyama vingi sio tafsiri ya kuwa na demokrasia. Tunaweza tukawa na vyama vichache vyenye sera makini, vyenye viongozi makini na ikaonekana kwamba kuna demokrasia ya hali ya juu katika nchi yetu. Majirani zetu takriban hapa baadhi ya nchi za Kiafrika wana vyama zaidi ya 300 nchi za karibuni tu hapa. Kilichopo ni vita na hakuna chochote kinachoeleweka. Lakini tunashuhudia kama Marekani na nchi nyengine zilizoendelea takriban kuna vyama viwili atu vitatu ambavyo hivyo zinaonesha kuwa na demokrasia ya hali ya juu.

Kwa hivyo katika hili sambamba na kuwasilishwa kwa Mswada huu Mhe. Spika, inanirudisha kuona kuna haja ya kumshauri Msajili wa Vyama aweze kufanya mapitio ya kuwangalia uhai wa vyama hivi na umakini wake ili ikiwezekana baadhi yao ambavyo hivyo vyama vipo kwa maslahi ya kutafuta ruzuku viondoshwe na vibakishwe vyama ambavyo vina lengo la kufanya siasa na kuingia katika serikali.

Mhe. Spika, fedha hizi tunazozizungumza hapa ambazo zitakwenda kama ni ruzuku tukumbuke kwamba zitatokana na kodi ya wananchi. Maana hizi si fedha za vyama wenyewe, hisi si kodi au si ada za wanachama wa vyama hivyo, hapana. Fedha hizi zitachukuliwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ambapo msingi wake ni kodi zinazozotokana na wananchi moja kwa moja, wale wenye vyama na ambao watakuwa hawana vyama. Kama hivyo ndivyo basi ni vyema kwa sababu hizi ni fedha zinazotokana na kodi za wananchi mgao wake ukawa na vigezo vinavyokubalika na vinavyotambulika.

Mhe. Spika, lengo la vyama vyote hivyo lengo lake ni moja tu, ni kufanya siasa na kushiriki kwenye chaguzi hilo ndio lengo tu la vyama vya siasa. Sasa hapa ni lazima tuwe na vigezo na kigezo cha kwanza ni namna chama kinavyoweza kushiriki katika uchaguzi. Kuna vyama vyengine hapo tangu vianzishwe havijawahi kushiriki katika chaguzi, licha ya kwamba tumeshapita katika chaguzi kadhaa si chini ya nne au tano vyama havijathubutu kushiriki katika uchaguzi. Kwa hivyo kuwe na vigezo maalum vinavyokubalika, wenzangu wamezungumza hapa kigezo Chama kusimamisha mgombea Urais, kuna kigezo cha kusimamisha Wabunge na Wawakilishi, kuna vigezo vya kusimamisha madiwani huu ndio uchaguzi hii ndio siasa yenyewe na ndio uchaguzi wenyewe.

Sasa inapofika pahala Chama ndani ya kipindi chote cha miaka 21 tangu kuundwa kwake hakijawahi kushiriki, maana yake tunasema kwamba licha ya kwamba kina ofisi au hakina ofisi kwa sababu vyama vyengine unaweza ukazunguka Unguja nzima ukatafuta ofisi zao usizikute, kwa kweli ofisi ni mkoba wake tu alionao mkononi. Kwa hivyo mgao huu wa ruzuku Mhe. Spika, mimi nashawishika kwamba lazima uwe na vigezo na mimi nikubaliane kwamba kigezo

ambacho ni sahihi ni kile kigezo cha kura kilichopata chama kupitia mgombea wa Urais. Maana yake hapo ndio chama chenyewe kitakachoamua. Maana yake hakutokuja malalamiko baadae kama mgombea Urais kapata asilimia hamsini, mmoja kapata asilimia arubaini na tisa, mmoja kapata asilimia mbili, na huyu aliyepata asilia mbili na yeye apewe japo shilingi mia tano ndio stahiki yake asipuuzwe japo mia tano mpeni mwambie ulichochuma ni hiki ondoka, fanya kazi zaidi ili na wewe upate zaidi.

Kwa hivyo mimi ninadhani Mhe. tungelikwenda kuwa na vigezo vilivyokuwa sahihi na vigezo ambavyo vinavyokubalika. Kuliko huu utaratibu wanaotumia wavuvi maana yake wavuvi mara nyingi wanapokwenda kuvua huwa na ule utaratibu kwamba kwanza kuna pesa zikishapatika, kuna fungu la nyavu zinatengwa pesa hizi ni za nyavu tu, baadae kunakuwa na pesa, chombo, hilo ni fungu la chombo baadae kitakachobakia manahodha tugawane. Kwa hivyo mimi nadhani huu si utaratibu sahihi. Utaratibu sahihi unatokana na wananchi moja kwa moja ni ule utaratibu unaotokana na namna chama kinavyoshiriki na namna chama kilivyoungwa mkono. Na tukizungumzia hivi basi tutapata kwamba wigo wa mgawanyo wa fedha hizi lazima utatanuka, kwa sababu ninakumbuka vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi uliopita ni vingi, na kuna vyama si chini ya saba, ingawa wengine walipata kura mbili wengine walipata kura tatu hiyo ndio hatima ya kazi yao.

Katika hili naomba niseme kwamba kama alivyosema hapa Mhe. Jussa kwamba lengo la ruzuku hizi zinazokuja kama walivyoeleza suala hili kwamba ruzuku zimeletwa ili kuviepusha vyama visije vikanunuliwa na wafadhili katika ule ule mtindo kwamba *anayemlipa kabili ndie anayechagua wimbo*. Lakini kama hili Mheshimiwa halitoshi nalo pia mimi naongezea kwamba pia isije ikapelekea na vyama vyenyewe vikanunuana kwa sababu tunaweza kuviepusha vyama visiweze kununuliwa na wafadhili wa nje lakini ikaja ikapelekea vyama vyetu kununuana wenyewe. Maana yake kama mimi chama changu nina uwezo mkubwa wa kifedha ninaweza nikavinununua vyama vyengine vilivyokuwa havina uwezo wa fedha, kwa hivyo tutakuwa tumehamisha ajenda upande mmoja tumepeleka ajenda upande mwengine. Kwa hivyo na hilo vile vile tulioneshe kwamba tusipovipa vyama vyengine hizi fedha vitapelekea na vyama hivi nao wageuke kuwa ni watumwa wa vyama vyengine vya siasa tulivyonavyo nchini.

Mhe. Spika, kama wenzangu walivyosema kwamba fedha hizi zinatokana na kodi ya wananchi na si fedha zitokanazo na michango ya wanachama; ni kwa msingi ule ule kwamba basi fedha hizi zitahitaji zikaguliwe na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Fedha za Serikali hilo ni kitu muhimu, kwamba leo katika magazeti ya leo kuna chama fulani wakubwa wake wanakamatana shati kwa sababu wakubwa tayari fedha zote za ruzuku wameshakopeshana wao wenyewe. Kwa hivyo hili ni muhimu liwekwe wazi kwamba Mdhibiti atapaswa kwenda kuzikagua fedha hizi lakini sambamba na hilo ambalo litatakiwa liainishwe, Mhe. Spika, napendekeza kwamba kuna kitu lazima kiongezeke na umuhimu wa kuainisha aina ya matumizi ni kitu muhimu sana.

Kwa sababu hata Wawakilishi tulipokuwa na sheria ile ya Mfuko wa Jimbo fedha zile tulipoziidhinisha hapa iliainishwa matumizi, matumizi yale yaliainishwa kwamba Mwakilishi na Kamati yake wanapaswa watumie fedha zile kwa ajili ya jambo fulani fulani. Kwa hivyo na hili Mhe. Spika, lazima tufike pahala aina ya matumizi katika vyama yaainishwe. Kwa sababu siku hizi kuna vyama tofauti na vina malengo tofauti tofauti. Unaweza chama fulani ukakipa fedha,

matokeo yake ikenda ikakodi watu kwa ajili ya jambo fulani. Sasa sidhani kama hayo yatakuwa ni matumizi sahihi ya fedha hizi za wananchi.

Hapa ninachokisisitiza kwamba aina ya matumizi ya fedha hizo kwa vyama yaainishwe wazi, maana yake tukisema Mdhibiti aende akakague, Mdhibiti atakachokwenda kukikagua ni namna ya fedha zilivyotumika kwa sheria ya manunuzi na sheria ya fedha tu, lakini Mdhibiti atakuwa hana uwezo aina ya matumizi yenyewe hata matumizi yale kama yatakuwa ni ya kiharamia, Mdhibiti atakachokifanya yeye kuangalia *procedures* za matumizi ndio sizo. Kwa hivyo hilo Mhe. Spika, naomba nilikazie.

Na mwisho nimuulize Mhe. Waziri kwamba ile sheria ya mwanzo ilipoletwa ilionekana ilishindwa kufanya kazi kwa sababu kama zilivyoainishwa kwamba hali ya makusanyo ya serikali yalikuwa hayaridhishi na ndio maana sheria ile isifanye kazi. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja anawezaje kutuhakikishia kwamba sheria hii itawezaje kutumika je, hali ya mapato ya serikali sasa yapo katika *position* hali ambayo inaweza tukaitoa, maana yake 1% ya matumizi ya kawaida kwa kweli ukiziangalia si pesa nyingi sana, maana hapa hatuko kwenye bajeti yote ya serikali, itakuwa ni bajeti inayohusiana na matumizi ya kazi za kawaida, hivi ndivyo ilivyoainishwa.

Sasa ninamuoma Mhe. Waziri atapokuja anihakikishie kwamba hali ya makusanyo yatawezaje kuifanya bajeti hii ili ile iliyosema kwamba isizidi 1% inaweza ikapungua itawezaje sheria hii hali ya makusanyo yakoje na namna gani sheria hii itavyoweza kufanya kazi katika wakati huu.

Mhe. Spika, ninakushukuru. Ahsante.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena na mimi kunipa fursa ya kusimama ili niweze kuchangia mawili matatu juu ya mswada huu unaohusu marekebisho ya sheria ya ruzuku kwa vyama vya siasa namba 6 ya mwaka 1997 na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, mimi nianze na dhana nzima ya uanzishwaji ya vyama vingi katika Tanzania yetu. Sina budi kuchukua fursa hii kuwashukuru viongozi wetu wakiongozwa na baba yetu kwa wakati ule akiwa Rais Mstaafu Ndugu Ali Hassan Mwinyi ambaye yeye alisimamia mageuzi haya na kuhakikisha kwamba sheria ya vyama vingi itafanya kazi ndani ya Tanzania. Lakini kwa upande wa Zanzibar kwa kipindi kile sheria hii ilikuwa inasimamiwa na Rais Mstaafu awamu ya sita Dr. Salmin Amour Juma.

Katika uongozi ule kwa kipindi kile mwaka 1995 ambapo vyama vingi vilianza kazi miaka miwili baadae 1997 sheria hii namba sita ilipitishwa. Lakini baada ya kupitishwa kwa sheria hii mwezi wa Agosti tuliona kwamba kulikuwa kuna sababu nyingi tu zilizosababisha serikali ishindwe kulipa mafao au fedha hizi ambazo zimetakiwa kulipwa kwa vyama vya siasa ambavyo vilikuwa vinafanya shughuli zake za kisiasa ndani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Lakini kabla sijaendelea mbele sana Mhe. Spika, kuna kitu ambacho wenzangu walionitangulia walianza kukizungumza kwamba tukiangalia kwa kina sheria hii ya vyama vya siasa inasimamiwa na Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Na kule Mhe. Spika, kuna malipo ya

ruzuku ambayo yanatoka, lakini kuna vyama vichache sana ambavyo vina uwakilishi upande wa Zanzibar, navyo pia vinatakiwa kuja kufanyiwa malipo hapa yanayohusiana na masuala haya ya ruzuku. Sasa nataka nipate ufafanuzi na maelekezo kutoka kwa Mhe. Waziri atakapokuja hapa, hivi vyama ambavyo vitakuwa vinafanya shughuli zake na vina uwakilishi hapa Zanzibar vitakuwa vinapata ruzuku mara mbili au vipi? Hili nilitaka nieleweshwe kwanza ili halafu tuweze kuendelea na mambo mengine.

Jengine pamoja na kuheshimu mapendekezo yaliyokuwa yametolewa na Kamati inayosimamia viongozi wakuu wa Serikali katika ukurasa wa 113 hapa pana maelekezo kwamba kuna maneno ambayo yanatakiwa yabadilishwe asilimia 25 ya kifungu cha 5 kifungu kidogo cha 2 (a) yasomeke asilimia 20. Mhe. Spika, mimi sioni sababu ya kubadilisha asilimia 25 tukaelekea kwenye asilimia 20. Lakini pia sioni sababu vile vile katika mgao wa madiwani kutoka asilimia 30 kuja asilimia 25. Ningeliomba kwa mawazo yangu asilimia ambazo zilikuwa zimependekezwa mwanzo basi ziendelee kubakia vile vile pasiwepo na mabadiliko yoyote.

Na vile vile napenda kuchukua fursa hii kuipongeza serikali katika kifungu cha 4 kifungu kidogo cha 1 pale iliposema kwamba serikali itatoa si zaidi ya asilimia 1 hii ni hatua kubwa sana ukilinganisha na pale mwanzo ilivyokuwa serikali inatakiwa itoe ruzuku kwa vyama vya siasa isiyopungua asilimia 1. Kwa hivyo sasa tumeipa nafasi serikali ya kuweza kuamua kama ikiwa asilimia 0.1 asilimia 0.5 asilimia 0.7 zote zile zinazowezekana kwa mujibu wa uwezo wa serikali, serikali iweze kulipa vyama vya siasa na vile vile zoezi hili liweze kufanyika.

Mhe. Spika, mswada huu ni mfupi sana lakini una mambo mengi sana ya kuweza kuchangia ili kuweza kufikia mustakbali ambao unakubalika na unaweza kufahamika na kueleweka na wale wanasiasa na vyama vya siasa ambavyo vinafanya shughuli zao katika nchi zetu. Mhe. Spika, watu waliotangulia vile vile walizungumzia suala zima la kuhakiki fedha ambazo zinatolewa na serikali kwenda katika vyama vya siasa. Mimi hoja hii naiunga mkono hususan ukitilia maanani suala zima la matumizi ya serikali, matumizi yoyote yanayoidhinishwa na serikali Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ana mamlaka na wajibu wa kwenda kuhakiki na kufuatilia masuala ya matumizi yale ya fedha za wananchi.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika kwa vile kuna wengi wanataka kuchangia nasema kwa niaba yangu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia mswada huu ulio mbele yetu. Lakini pia nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kutuletea marekebisho haya ya mswada huu wa ruzuku ya vyama vya siasa kwa wakati muafaka. Pia niipongeze Kamati kwa kazi nzuri na wao waliyoifanya.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu unaanza kwanza kwa kuipongeza serikali kwa kuifanya sheria hii sasa iweze kutekelezeka. Kwa sababu kama tunavyojua ni muda mrefu sheria hii imetungwa lakini ilikuwa na ugumu wa kutekelezeka, lakini kwa sasa serikali imeweza kujipanga na kuweza kuifanya sheria hii itekelezeke ili vyama viweze kupata ruzuku hii na viweze kujiendesha.

Mhe. Spika, kutokana na majukumu mazito ya serikali ndio maana ninaipongeza kwa sababu tunajua serikali ina majukumu mengi tuna mahitaji mengi wananchi tunayahitaji kupitia serikali yetu, lakini pia imeweza kulipa umuhimu suala hili la vyama vya siasa kuweza kuipatia ruzuku.

Mhe. Spika, mimi maoni yangu napenda niungane na mchangiaji ambaye amemalizia kuchangia kwa sababu na mimi ilikuwa tayari maoni yangu yako hivyo na yeye ametangulia kusema kwa hivyo naomba niungane nae kwamba asilimia hii 25 ambayo ililetwa katika marekebisho, basi naungana nae basi marekebisho haya bora yawe hivi hivi kama yalivyo katika kiti cha Rais tuendelee kuwa na asilimia 25 na huku kwengine iendelee hivi hivi ilivyo, isipokuwa tunajua asilimia 30 ya madiwani tutatoa tano tutaileta katika asilimia ishirini ambayo waliitaka wao iwe hivyo lakini mimi kwa mapendekezo yangu naomba iwe asilimia 25.

Mhe. Spika, kama tunavyojua asilimia hii 25 kwa kuiweka katika fungu hili la Rais basi utakuta pia haijawa na ukubwa kama huo unaodhaniwa labda unaweza kuwa ni mkubwa, kwa sababu kama tunavyojua Rais ana majukumu mengi na majukumu yake ni makubwa kutokana yeye na cheo chake, kwa hivyo hii asilimia 25 utaiona sio kubwa. Mimi kwa upande wangu naiona ni ndogo sana sema tunaichukulia kwa kuwa serikali uwezo wake ni mdogo kwa hivyo tunaridhika kwa hapo. Lakini kama serikali itakuwa na uwezo mkubwa basi hata hii asilimia 25 si vibaya ikaongezwa zaidi.

Mhe. Spika, mimi pia napendekeza katika vile vyama ambavyo vitakuwa havina viti, basi kwa kweli visiweze kupata ruzuku hii kwa sababu itakuwa ni kuongeza tu utitiri wa vyama, matokeo yake chama kinasimamishwa lakini katika nchi nzima kinaweza kikapata kura kumi itakuwa haikidhi haja. Kwa maana hiyo mimi nashauri vipatiwe ruzuku vile vyama ambavyo tayari vina uwezo wa kupata viti na kuweza kuvitumia katika mabaraza yetu haya au mabunge yetu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi katika mswada huu mapendekezo yangu yalikuwa ni hayo kwa sababu huu mswada si mkubwa na ni marekebisho tu, kwa hivyo mawazo yangu yapo katika kuitetea hii asilimia 25 ikiwezekana asilimia 25 hii ibaki kama ilivyo na ikiwa serikali itapata uwezo mkubwa zaidi basi iendelee zaidi ya hapo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ninakushukuru Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii nami nikaweza kuchangia mawili matatu katika mswada huu wa marekebisho ya sheria ya ruzuku ya vyama vya siasa Nam. 6 ya mwaka 1997 na mambo mengine yanayohusiana na sheria hii.

Mhe. Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud kwa kuwasilisha marekebisho haya muhimu mbele ya chombo hiki, ili Waheshimiwa Wajumbe wayapitie na waweze kupitisha marekebisho haya ambayo ni marekebisho muhimu katika mswada huu.

Mhe. Spika, mimi baada ya kupokea mswada huu na kuona marekebisho yaliyofanywa ndani ya sheria hii moja kwa moja niliangalia madhumuni ya kufanywa marekebisho hayo, na nimeona kwamba sheria hii ambayo imepitishwa tokea mwezi wa Agosti mwaka 1997 ilishindwa

kutekelezwa kwa mambo mawili makubwa ya msingi ambayo Mhe. Waziri ameona iko haja ya kuyafanyia masahihisho ili sheria hii iweze kutekelezeka.

Mhe. Spika, sheria hii ni muhimu na kama wenzangu waliotangulia kusema kwamba sheria hii ilitungwa kwa madhumuni ya kuviwezesha vyama vya siasa kupata ruzuku na kuweza kuendesha vyama kwa manufaa ya wananchi. Kama tunavyofahamu kwamba mfumo huu wa vyama vingi vya siasa kwetu hapa Zanzibar ni mpya kwa hivyo ni lazima vyama hivi viweze kusaidiwa katika kuendesha shughuli za kisiasa, jambo hili ni muhimu na lingetakiwa liweze kutekelezwa tokea wakati ule. Lakini kwa bahati mbaya halikuweza kutekelezwa na baada ya kuona umuhimu wa jambo hilo, serikali hii ya awamu hii imeona ni vyema ifanye masahihisho na hatimaye tuweze kutekeleza.

Mhe. Spika, fedha hizi zinazotolewa na serikali ni fedha za kodi ya wananchi ambazo zitatoka katika mfuko mkuu wa serikali na zitapitishwa hapa katika chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi. Na fedha hizi sio sadaka kama wengine wanavyofikiria kwamba kila mtu apate hapana. Lengo la fedha hizi ni kuviwezesha vyama kuweza kutimiza majukumu yake kwa lengo la kuleta maendeleo katika nchi. Kwa hivyo nakubaliana na wale waliosema kwamba kuna haja ya kufanyiwa ukaguzi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali zikaguliwe ili yaonekane matumizi yake.

Lakini pia nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe waliosema kwamba hata namna ya kuzitumia basi kuwe na maelekezo ya namna ya kutumika ili wakati unapofanywa ukaguzi basi uwe ukaguzi yakinifu, kwa hivyo mimi nakubaliana pia na suala hilo.

Mhe. Spika, fedha hizi kwa mujibu wa mswada huu wa sheria unaeleza kwamba zitatolewa kwa vile vyama ambavyo vimeshinda katika chaguzi na huu ndio utaratibu ambao unatumika. Kwa sababu jambo hili hatukulianzisha sisi limeanzishwa na wenzetu na wanaendelea nalo na sisi tunaanzisha ili tuweze kuendelea nalo. Na mimi nakubaliana na hoja hii ya msingi ya kupewa vyama vile ambavyo vina uwakilishi ndani ya chombo hiki na hili lina mantiki. Fedha hizi huwezi ukazigawa kwa vyama vyote na utakapofanya hivyo maana yake utaendelea ule utitiri wa vyama, na vyama vinaweza kuanzishwa kwa sababu wanajua kuna ruzuku inayotolewa na serikali na havitoanzishwa kwa sababu ya upinzani wa kisiasa. Kwa hivyo mimi ninaamini utaratibu huu utaviwezesha hivyo vyama vyengine sasa kwenda kwenye ushindani zaidi ili hatimae na wao kuweza kupata ruzuku hii ambayo inatolewa na serikali. Mimi naunga mkono kwamba ruzuku hii bado iendelee kutolewa katika vyama kwa mujibu wa mswada huu wa sheria, vyama hivi ambavyo vina uwakilishi ndani ya chombo hiki.

Lakini katika sheria iliyotungwa mwaka ule 1997 ilizigawa hizi fedha katika vyama kwa utaratibu uliokubalika wakati ule kwamba nafasi ya Urais chama kinachoshinda Urais kipate asilimia 50 ya ruzuku ile. Na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao walioshinda wapate asilimia 50 ya ruzuku ile kama sikosei, ilikuwa asilimia 30 asilimia 50 ilikuwa ya Rais, Waheshimiwa Wawakilishi asilimia 30 na Madiwani ilikuwa asilimia 20 kuifanya yote iwe asilimia mia moja.

Mgao huu ulikuwa unafaa kwa wakati ule lakini serikali katika hatua ya mwanzo walitafakari juu ya namna ya kufanya marekebisho ya mgao huu na katika hatua ya awali ilipunguza kutoka asilimia 50 ya nafasi ya kiti cha Urais kuja asilimia 25, na nafasi ya Wajumbe wa Baraza la

Wawakilishi kuwa asilimia 50 na Madiwani kubakia na asilimia 25 kutoka nafasi ya asilimia 20. Lakini hatimae serikali ikafanya mabadiliko na kufanya asilimia 20 kwa nafasi ya Rais, asilimia 50 kwa nafasi ya Uwakilishi na asilimia 30 kwa nafasi ya Udiwani.

Kupanga ni kuchangua Mhe. Spika, lakini mimi nimevutika zaidi na hili pendekezo la mwanzo bado Mhe. Rais atakayeshinda abakie na asilimia 25 ya fedha za ruzuku na Wawakilishi tubakie na asilimia 50 na Madiwani waendelee kubakia na nafasi ya asilimia 25. Kwa nini Mhe. Spika, ninakubaliana na hoja hii. Nafasi ya Urais sizungumzii hii kwa sababu sasa hivi inashikiliwa na Chama changu cha Mapinduzi la hasha! Pengine kuna siku inaweza kushikiliwa na chama chengine. Lakini ninazungumzia umuhimu wa nafasi hii ya Urais. Kwanza ni nafasi ya eneo zima la nchi nzima na Rais anayechaguliwa katika nchi hii maana yake ndiye anayepata nafasi ya kusimamia kwa udhati utekelezaji wa ilani ya chama chake. Kwa hivyo ana umuhimu wa kuwezeshwa chama chake kina umuhimu wa kuwezeshwa ili aweze kusimamia vyema utekelezaji wa ilani ile ya chama chake. Lazima tukumbuke kwamba chama kinachoshinda ndicho kinachotekeleza ilani ya chama kiliopo.

Kwa hivyo kumuwezesha Rais aliyepo madarakani, kutekeleza ilani ya chama chake inahitaji msukumo wa kweli. Kwa hivyo pamoja na kupunguzwa kutoka asilimia 50 ya sheria ya mwanzo katika busara zilizofanywa mimi Mhe. Spika, bado ninavutika na asilimia 25 iliyopo kutoka hamsini kuja asilimia 25 ili tumuwezeshe Mhe. Rais wa Chama chochote atakayeshinda kuweza kusimamia ilani ya uchaguzi ya chama chake ambayo imeenea katika eneo lote.

Lakini jengine Mhe. Spika, niunge mkono suala la marekebisho haya ya asilimia ya ruzuku ya isiyozidi asilimia moja hili limeangalia zaidi maslahi ya wananchi wetu kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe wengine. Kwa sababu hatuwezi kuitwisha mzigo serikali tukailazimisha serikali kutoa asilimia kubwa zaidi kwa ajili ya kuendesha vyama vya siasa huku fedha hizo au kodi hizo za wananchi zikitegemewa kwa shughuli nyengine za maendeleo kama afya, elimu na mambo mengine. Kwa hivyo mimi ninakubaliana na hoja hii na kiwango hiki kisichozidi asilimia 1 na kwa bahati nzuri bajeti hii tutaipitisha hapa katika zile fedha za matumizi ya kawaida ili ziweze kusaidia vyama hivi vilivyokuwa na Wawakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, sheria iliyopita ilikuwa inazungumzia zaidi ya asilimia moja kwa fedha za jumla maana hata zile fedha zinazoletwa na wahisani kutusaidia katika shughuli za maendeleo hilo jambo kwa kweli wakati ilipotungwa sheria hii halikuzingatiwa vizuri, lakini sasa tumezingatia vizuri kwamba fedha za matumizi ya kawaida za serikali hizo sasa tutazitoa si zaidi ya asilimia moja kwa ajili ya vyama vya siasa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naunga mkono mswada huu wa sheria na niwaombe Wajumbe wenzangu wauchangie, na kwa kuwa mimi ni Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi, niwaombe sana Waheshimiwa wa Chama cha Mapinduzi wachangie mswada huu ili upate baraka za pande zote mbili na hatimae iwe ni sheria ambayo itaweza kutekelezeka kwa manufaa ya vyama vyetu na kwa maslahi ya nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja pale Mhe. Waziri atakapokubaliana na ombi langu la kurejesha asilimia ile aliyoileta mwanzo ya asilimia 25 si kwa

manufaa ya chama changu tu cha Mapinduzi, ni kwa manufaa ya nafasi hii na umuhimu wa nafasi hii katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Nimuombe radhi Mhe. Subeit kwamba hataweza kuchangia kipindi hiki na badala yake tumuombe aje achangie jioni yeye pamoja na Waheshimiwa wenzake nitawaomba wote wafike mapema pamoja na wengine ili kuja kuendelea na mjadala huu. Kwa hivyo jioni tutakuwa na nafasi ya Mhe. Subeit, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Nassor Salim Ali na orodha hii inamalizika kwa Mhe. Fatma Mbarouk Said wote hao niwaombe wafike mapema pamoja na wengine bila shaka ili tuendelee na shughuli zetu za mjadala wa mswada huu muhimu.

Waheshimiwa Wajumbe nimetumwa nitoe taarifa kwa wanachama wa Uwawaza, Umoja wa Wawakilishi Wanawake wa humu ndani kwamba mara baada ya kuakhirisha shughuli zetu hivi punde wao wabaki kwa muda mchache sana kuna mambo wanataka kuambizana. Kwa hivyo niwaombe basi wao wabaki kwa muda mchache.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni kwa kushirikiana nami kwa kuendesha shughuli zetu kwa ufanisi mzuri. Ninaakhirisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7:00 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba kuipongeza serikali kwa dhati kabisa. Nichukue nafasi hii niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona kwamba kuna haja sasa hivi mswada huu kufanyiwa marekebisho ili uanze kutumika.

Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri mtoto wangu Mohammed Aboud ambaye amewasilisha mswada huu kwa utulivu na sisi tutamchangia ili aweze kuuboresha zaidi. Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuipongeza kamati Mhe. Spika, niipongeze kamati ambayo iliangalia kwa kina na yale mapendekezo yao waliyoyapendekeza. Tunaporekebisha sheria ni kwamba hatumtungii mtu sheria ile tunatunga kwa ajili ya taifa letu, hilo naomba.

Kwa sababu huu mswada ni Ruzuku kwa Vyama vya Siasa, niseme tu kwamba vyama vikubwa vya siasa kwa hapa Zanzibar ni CUF na CCM. Kwa hivyo, niwaombe wenzangu kwamba huu mswada hatutungii chama tunatunga kwa mujibu wa taifa hili litapoongozwa na vyama vya siasa. Ni kweli mswada huu toka mwaka 1997, lakini mimi niseme kwa wakati ule kidogo kulikuwa na utashi utashi mana lazima tuseme ukweli. Kwa sababu wakati ule kulikuwa na utashi kwamba kwanza tulikuwa hatufahamiani, zogo, tulikuwa tunaingia kwenye mfumo ambao wa vyama vingi. Lakini pia kulikuwa na utashi wa vyama vingi manaake ukiacha CCM na CUF kulikuwa na utitiri. Sasa tungepitisha wakati ule pamoja na kwamba vyama hivyo visingepata

uwakilishi katika mswada huu, lakini pamoja na hivyo ni vyama navyo vilijisajili kwa sheria serikali ingepata shida kidogo.

Sasa mimi niseme kwamba sasa hivi ni wakati mwafaka kwa mswada huu kufanyiwa marekebisho haya. Tukilinganisha mwaka 1997 na sasa hivi mimi niseme ni wakati mwafaka. Kwa sababu vyama vikubwa kwa upande wa Zanzibar ni CCM na CUF. Kwa hivyo, niseme ni wakati wake lakini nitaiomba serikali, wamesema hapa asilimia mbali mbali mimi namuomba sana Mhe. Waziri, mwaka 1997 na mwaka 2013 ni tofauti, kwa hivyo mimi nikubaliane na serikali si kwamba sikubaliani na kamati kwa sababu kamati nayo ina wajibu wake kutoa mapendekezo, lakini nikubaliane na serikali kuwa kipindi kile na hiki ni tofauti.

Mhe. Spika, naomba nikubaliane na Mhe. Waziri kwamba zile asilimia 25 zibakie vile vile badala ya asilimia ambazo kamati imependekeza. Kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu kipindi hiki tulichonacho tuangalie hali halisi na kama nilivyosema mwanzo kwamba hatuuboreshi mswada huu kwa sababu ya chama au atakayekuwa madarakani tunapanga sheria ambayo itatumika katika nchi, tusiangalie Chama cha CUF, tusiangalie Chama cha Mapinduzi, hii ni sheria ambayo itatumika katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri na nishawishi na mimi wenzangu Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tukubaliane na ile asilimia ambayo ameizungumza mwenyewe Mhe. Waziri katika mswada huu.

Lakini na mimi kwa sababu wenzangu wamechangia sehemu mbali mbali na mimi niseme kwamba, hizi ni fedha za kodi za wananchi. Kwa hivyo, nikubaliane na wale wenzangu waliosema kwamba hizi fedha zikaguliwe, kwa sababu chochote unachopewa miongoni mwa serikali basi kuna taratibu zake na sheria zake. Mimi naomba sana na tutapokagua tuwe na vigezo na tupewe maelekezo kwamba moja, mbili, tatu, nne kila chama au hata nani atatoa hesabu zake kwa mujibu wa utaratibu uliopangwa ili wenyewe wananchi wanaochanga fedha hizi, kwa sababu zinachangwa na wananchi wajue kitu gani na gani kimetumika na vipi fedha hizi zimetumika. Kwa hivyo, niunge mkono wale wenzangu ambao wamechangia katika sheria hii.

Mhe. Spika, na mimi sitakuwa na mengi kwa sababu huu mswada tunauboresha tu baadhi ya sehemu na ni mswada mdogo kidogo, niseme naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuzungumza machache katika kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ya mwaka 1997 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ingawa ni ndogo lakini nzuri anastahiki kupewa pongezi. Sheria hii ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ambayo ilianzishwa mwaka 1997 kuweza kuifanyia marekebisho ambayo yamo katika mswada huu. Mimi Mhe. Spika, kwanza niungane na wenzangu waliotangulia ambao wameunga mkono asilimia 50, 25 na 25; yaani asilimia 25 kwa wale Wajumbe wa Baraza na asilimia 25 nyengine kwa Rais na asilimia 25 kwa Madiwani.

Mhe. Spika, sheria hii au mswada huu ambao umempunguzia Mhe. Rais kutoka asilimia 25 kwenda 20 mimi siungani nao. Kwa sababu Mhe. Spika, katika sheria hii ya mwaka 1997 mwanzo ilimpa Mhe. Rais asilimia 50 na imepunguzwa imekuja asilimia 25 na leo imeletwa iwe asilimia 20. Kwa kweli hapa tunapokwenda sio pazuri, mimi naona ipo haja ya kubakia asilimia 25 na asilimia 25 kwa Madiwani na ile asilimia 50 ni kwa Wajumbe wa Baraza.

Sote tunafahamu Mhe. Spika, umuhimu wa suala hili kwa vyama vyote ambavyo vimo humu Barazani ikiwemo CCM na CUF tunajua umuhimu wake, na sio kwamba tunazumza kuitetea hii asilimia 25 kama Mhe. Salmin Awadh alivyozungumza sio kwamba Chama cha Mapinduzi ndicho kinachoongoza dola na ingawa kitaendelea kuongoza dola, lakini tunachozungumzia ni kwa maslahi ya vyama vyetu vyote. (*Makofi)*

Mhe. Spika, niungane na wengine waliozungumzia kuhusu ruzuku hii kwa vyama vyengine. Mhe. Spika, kuna vyama vyengine naweza kusema vinaishia Nungwi, Chumbe au Mkoani. Sasa vyama hivi ambavyo havijulikani haifai kuonjeshwa, tuangalie vyama hivi ambavyo vina wanachama wengi, vina wapenzi wengi ili kuweza kuimarisha na kuendeleza demokrasia yetu ndani ya vyama vyetu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi niunge mkono tu mswada huu kwa asilimia mia moja na ningemuomba Mhe. Waziri anapokuja basi akubaliane na wajumbe kuendelea kama hivi utaratibu ulivyo mwanzo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kwanza kabisa Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii ya leo kutuwezesha viumbe vyake tukiwa hai na kusimama katika Baraza hili la Wawakilishi na kujadili maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mswada huu uliopo mbele yetu ni mswada muhimu kwa sababu unajadili maslahi ya nchi yetu. Kama wenzangu walivyotangulia niseme mswada huu umekusudia kuweka sawa katika sheria ambayo tulikuwanayo nyuma lakini sheria hii naweza kusema kwamba tangu ilipopitishwa basi haijafanya kazi. Sasa kwanza kabisa niombe kwamba tunapotunga sheria zetu basi tuangalie ile sheria ambayo inatekelezeka kuliko kutunga sheria ikawa haitekelezeki.

Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea sheria hii. Lakini nimuombe kwamba baada ya kuwa sheria hii nyuma ilikuwa ipo lakini sasa tunaifanyia marekebisho ili iweze kutekelezeka ajitahidi sasa tuone kwamba sheria hii inafanya kazi na kila anayestahiki kupewa ile ruzuku basi aweze kupewa. Kwa sababu si hoja kuipitisha sheria hii, lakini sasa hoja ni utekelezaji wa hii sheria.

Mhe. Spika, na mimi napenda niungane na wenzangu kwa kusema kwamba, kama sheria hii ilivyoona kuwa vyama vya siasa vina umuhimu wa kupewa hizi ruzuku ili kujiendeleza kila mmoja anajua kama vyama vya siasa vinastahiki kupata hiyo ruzuku kwa sababu zinataka kutekeleza kazi zake. Kwa maana hiyo ndio maana serikali ikaona kuwa kuna haja ya vyama hivi vya siasa kupewa hizi ruzuku.

Lakini Mhe. Spika, mimi nasema kwamba vyama vya siasa zimegaiwa ruzuku kwa mgao wa Rais, Wawakilishi pamoja na Madiwani. Sasa Mhe. Spika, asilimia hizi 20 ambazo zimewekwa

kwa ajili ya kupewa Rais zinastahiki kupewa lakini mimi nilikuwa nna mapendekezo yangu ya hizi fedha. Mapendekezo yangu kwa sababu wagombea uwakilishi ruzuku kwa ajili ya majimbo ya uwakilishi zinagaiwa kwa uwiano wa viti maalum vitakavyopatikana.

Kwa hivyo, ningependelea kama na hizi fedha ambazo zitatoka kwa ajili ya Rais basi mapendekezo yangu ziangaliwe kwa kura za uwiano wa marais, wale waliogombea urais ziangaliwe zile kura na ziwekwe asilimia ya kura zile zilizopatikana zigaiwe kwa ajili ya kura kuliko kuzichukua tukampa mtu mmoja kama ni Rais tuseme apewe yeye ni sawa chama chake kina sera ya kutekeleza sera au ilani iliyopo ndio inayofuatwa ni sawa, lakini na hawa wagombea wengine waliyogombea wakapata asilimia ikiwa ni kubwa basin a wao wanataka kutekeleza azma za chama chao kwa sababu kunakuwa na ahadi nyingi za chama sasa na wao wanataka kutekeleza.

Kwa hivyo, naomba hizi fedha zigawiwe kwa ajili ya uwiano wa kura, ziangaliwe kura zinazopatikana na ruzuku hii igawiwe kwa uwiano wa kura.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu na wao kama ninavyozungumza kuwa wana umuhimu wa utekelezaji wa kazi zao na ni muhimu sana, halafu hii itatusaidia kwa sababu kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba chama si CUF tu na CCM hapana, kuna CHADEMA, kuna NCCR, kuna Jahazi kwa hivyo na wao wanaweza wakajikaza wakapata kura nyingi, sasa kama wamepata kura nyingi mgombea wao wa urais basi na yeye ana haki ya kuangaliwa na yeye akapata zikamsaidia kukiendeleza chama chake. Kwa hivyo, hizi fedha bora ziangaliwe kwa utaratibu wa kura.

Mhe. Spika, suala hili ni muhimu sana na mimi kidogo nipingane na mwenyekiti wangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliposema kuwa hizi fedha ziangaliwe ziingizwe kwa kuongezewa mishahara wafanyakazi. Hizi hazihusiani na wafanyakazi, kwa sababu hizi serikali imepanga kama ni ruzuku kwa vyama vya siasa na sio huku kwetu tu, hata wenzetu huko Bara na wenzetu wengine basi kwenye vyama wanapewa ruzuku. Chakusikitisha kwetu ni kwamba, hizi fedha tangu sheria ilipopitishwa hakijapata hata chama kimoja fedha hizi. Kwa hivyo, sasa niwaombe nimuombe Mhe. Waziri baada ya kupitishwa sheria hii wameona kama hii asilimia iliyowekwa tunaweza kuitekeleza. Kwa hivyo basi, aweze kusimamia baada tu ya Rais kutia saini iweze kufanya kazi na ruzuku ziwasaidie.

Mhe. Spika, kwa hayo machache ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuuona mwaka 2013.

Mhe. Spika, niwatakie Wajumbe wote heri ya mwaka mpya. Pia nimshukuru Waziri kwa kuwasilisha Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa, Sheria Nam. 6 ya mwaka 1997 na mambo yanayohusiana na hayo.

Kwa kuanzia niseme Mhe. Spika, sheria hii ni muhimu na kwa kuwa Serikali yetu ya Mapinduzi inafuata misingi ya utawala bora ikiwemo demokrasia ya vyama vingi. Mwenyezi Mungu ameweka serikali za wanadamu na mabaraza ya mataifa kama dua yetu ya kila siku ya

kuliombea Baraza hili tukufu la Wawakilishi ambayo ningekuomba Mhe. Spika, ukaridhia angalau kwa dakika kidogo nikainukuu.

Mhe. Spika, dua ya kuliombea Baraza la Wawakilishi inasema, "Mwnyezi Mungu mwingi wa Utukufu muumba mbingu na ardhi, uliyeweka katika dunia serikali za wanadamu na mabaraza ya mataifa ili haki itendeke kwa kufuata sheria kama vile upendavyo wewe, twakuomba kwa unyenyekevu tupe hekima sisi waja wako tuliokusanyika hapa tukiwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi wa Wananchi wa Zanzibar, utuongoze daima katika kujadili mambo yote yatakayoletwa mbele yetu ili tuweze kushinda matatizo yetu kwa manufaa ya ustawi wa nchi hii na watu wake **Amin**".

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa mustakabali huu nasema kwamba hii ni kazi yetu katika Baraza hili tukufu kuwa yale yote ambayo tutayaona yana mustakabali na taifa letu tuyazungumze na tuyajadili humu ili tuifanye kazi hii ambayo ni muhimu.

Kwa kweli Mhe. Spika, nikiendelea ni kwamba hii ni demokrasia ambayo imo katika nchi yetu, kwa vile Zanzibar ni sehemu ya ulimwengu kila baada ya muda kunapatikana mambo mbali mbali na tukiwa kama tunaridhia mikataba ya kimataifa kwa hivyo ni lazima turidhie na yale ambayo yatakuwa hayendi kinyume na taratibu na sheria zetu na silka pamoja na mila zetu.

Kwa hivyo, hivi vyama vingi nitasema kwamba ni maridhiano ya kimataifa ambayo yameleta vyama vingi na kwa sasa ni lazima tutizame namna ya kuviendesha hivyo vyama na kufuata sheria hizi.

Mhe. Spika, nikienda kwenye sheria yenyewe ambapo Mswada huu wa Sheria una sehemu mbili kubwa ambapo sehemu ya kwanza inasema masharti ya awali ambayo yalikuwa na marekebisho na vile vile sehemu ya pili ya marekebisho ya vifungu mbali mbali. Mimi niseme kwamba nimeridhika na mgawanyo huu, lakini vile vile kuna vyama na wao wametimiza ile demokrasia na hapa sijaona kwamba kuna gawio lolote kwa upande wao na kwa sababu wametimiza demokrasia ilikuwa na wao wapate ruzuku hii.

Mhe. Spika, mimi siku zote husema kwamba nina usemi nautumia sana *'Batter late than never'*, bora kuchelewa kuliko kabisa na leo hii nimefarijika sana kusema kwamba tunajadili mswada huu na hapo juu najua yupo msaidizi au tuseme naibu mrajis wa vyama anasikiliza hapa. Kwa hivyo, najua kwamba suala hili na yeye analisikiliza kwa umakini zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme kwamba ni mengi yameshasemwa lakini si vibhaya kurudia vile vile kwamba, pesa hizi kwa sababu ni *public money* kwa hivyo zinahitaji zikaguliwe. Sasa na mimi kama Mjumbe wa Kamati ya PAC na Mwenyekiti wangu asubuhi nimemsikia akisema hivyo na mimi naunga mkono kwamba fedha hizi ni lazima zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, baada ya hayo nisipoiteze muda wako mwingi niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii adhimu na mimi ya kuchangia katika mswada huu ambao uko mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kuwepo hapa kushughulikia shughuli zetu za kila siku.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii adhimu kukutakia wewe heri ya mwaka mpya pamoja na wananchi wote wa Zanzibar. Vile vile naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuletea sheria hii mbele yetu ili tuweze kuijadili na baadae kuweza kuipitisha.

Mhe. Spika, sheria hii ambayo inazungumzia ruzuku kwa vyama vya siasa ni sheria ambayo imekuja wakati mwafaka, lakini lengo lake kubwa ni kupanua wigo wa demokrasia na kuongeza ushindani wa kisiasa.

Mhe. Spika, tunafahamu kwamba asili ya vyama vya siasa haikuanza leo wala jana, imeanza zamani na lengo lake ni kuhakikisha kuwa maendeleo yanapatikana wakati huo vyama vya siasa vilikuwa na lengo la kuleta uhuru na mapinduzi katika taifa la aina yoyote.

Kwa wakati huo Mhe. Spika, kuna mjumbe hapa alisema kulikuwa na vyama vya siasa vingi na baada ya mapinduzi kukawa na chama kimoja cha siasa kwa muda wa miaka 31. Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu nafikiria kwamba hilo lilikuwa ni wazo zuri kwa kipindi chote tulikuwa tunatengeneza umoja, upendo, utulivu na amani katika nchi yetu na kwa hakika tumeupata.

Sasa kwa sababu karne hii inatupeleka kwengine basi ni wajibu kuwa na vyama vya kisiasa vingi, lakini vile vile vyama vya kisiasa tukumbuke kwamba ni chachu ya maendeleo katika taifa la aina yoyote. Hivyo narudia tena kusema kwamba kwa kweli huu ni muda muafaka hivi sasa wa kuhakikisha kwamba vyama hivi vinapewa ruzuku ili kusaidia katika shughuli zake zote za kisiasa na baadae kuingia kwenye ushindani na kupata ushindi kwa lengo la kuleta maendeleo katika taifa letu.

Mhe. Spika, wenzangu wengi waliotangulia kuzungumza wamezungumzia kuhusu suala zima la mgawano wa ruzuku na mimi napenda kusema kuwa nimeridhika na mgawano ambao umependekezwa na Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa sababu nimeona kwamba kutokana na hali ya kisiasa kama alivyotangulia Mhe. Nassor Salim Ali alivyosema huu si mgawano wa chama kimoja na kutokana na hali ya kisiasa tunayokwenda kila mtu mgawano huu utakuja kumgusa wakati wowote. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba sote tuunge mkono na dalili ipo kwa sababu wengi wameshaunga mkono, hivyo dalili ipo na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba mswada huu utapita vizuri.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumziwa ni suala zima la utumiaji wa ruzuku hizi. Mimi naunga mkono kauli za Wajumbe kwamba utumiaji wake basi uwe unachunguzwa namna matumizi yamefanyika na kamati inayohusika na uchunguzaji wa fedha za serikali. Hatutaki leo ruzuku hii iende katika mikono ya watu wachache.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri vyama vyengine ambavyo ni vyama vidogo vidogo kwa kweli zaidi ya vyama viwili vikuu ambacho ni chama changu Chama cha Mapinduzi pamoja na Chama

cha CUF, sioni chama chengine hapa ambacho kitaweza kufaidika na ruzuku hii kwa kipindi hiki sijui hapo baadae.

Lakini kwa kipindi hiki tunachokwenda kwa muda wa miaka 10 mbele hofu yangu ni kwamba sifikirii kwamba ambao watakaofaidika na vyama vyengine, lakini ningeomba sana kwa sababu naamini lengo lao ni moja ni kuleta maendeleo ya Zanzibar sawa sawa na vyama vyengine, inawezekana wengine wapo ambao wana lengo baya lakini wengi tunaamini kwamba na wao wana lengo moja kama vyama vyengine. Sasa basi ningewashawishi kwamba zile nguvu zao waziweke pamoja ili angalau na wao waweze kupata ruzuku hii ambayo itatolewa na serikali.

Mhe. Spika, mimi vile vile ningefurahi zaidi kwamba vyama hivi kuwe na kabla ya usajili wa vyama hivi ambavyo vitakuwa ni vyama vya kisiasa basi kuwe kuna criteria ambazo maalum, ingawa ninajua kuna criteria lakini basi tuzidishe kuweka sheria ambazo zitakazowabana watu wachache kuanzisha vyama vya siasa ili kuondosha ule utitiri wa vyama vya siasa ambavyo baadae wanaweza kudhani watazifaidi ruzuku hizi.

Mhe. Spika, mimi kama wengine leo kwa sababu tu sheria hii ni ndogo lakini nitasema kwamba hii asilimia moja ambayo serikali ina nia ya kuitoa basi isiwe zaidi ya asilimia moja, mimi nafikiri ni sahihi kabisa ibakie kuwa kuwa ni asilimia moja mpaka hapo baadae, lakini kwa sasa iendelee kuwa isizidi zaidi ya asilimia moja.

Lakini vile vile tukumbuke kwamba tusije tukang'ang'ania tukasema asilimia moja ikiwa serikali mapato yake sio mazuri, basi tukubali kwamba inaweza kuwa ni 0.9 au 0.8 lakini isizidi asilimia moja.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache napenda kuwa naunga mkono mswada huu na namtakia kheri na mafanikio Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Dalili inaonesha kwamba tumefikia pahala si pabaya. Kwa maana hiyo tumalizie na Wajumbe hawa wafuatao:
1 Mhe. Hassan Hamad Omar
2. Mhe. Mussa Ali Hassan

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana. Kwanza kabisa Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu Subuhana Wataala aliyetujaalie jioni hii ya leo kuwa katika hali ya uzima na afya njema.

Vile vile nisiwe mwizi wa fadhila nikushukuru na wewe uliyenipa nafasi hii kutoa maoni yangu katika marekebisho ya mswada huu wa sheria wa ruzuku wa vyama vya siasa.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais kutuletea mswada huu wa marekebisho ya sheria ya ruzuku ya vyama vya kisiasa.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba mwanzo wowote ni mgumu kwa sababu sheria hii Nam. 6 ya 1997 huko nyuma haikutekelezeka. Lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu

imerudishwa tena hapa Barazani kwa marekebisho, tunamuomba Mwenyezi Mungu atusaidie ipite salama. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa kweli imani yangu kila aliyeanza na chama cha kisiasa ana malengo, na ana malengo ya kufikia alipokusudia. Kuviwezesha vyama vya kisiasa ndio kuvielewa, maana ni kuvipa uwezo. Kama chama hakina uwezo hakiwezi kufika hatua inayoitaka lakini hapa pamoja na ruzuku hii tuna imani kila chama kinachokusudia malengo mazuri kitafikia muafaka. Hakuna malengo yanayokusudia chama cha kisiasa kwa kukamata hatamu ya dola, hakuna jengine ili kuongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi niseme tu ruzuku hii iliyogaiwa asilimia 50 kwa upande wa viti vya Uwakilishi na asilimia 20 kwa upande wa Urais na asilimia 30 kwa upande wa Madiwani, mimi ninatoa hongera sana. Kwa sababu nilisema mwanzo kama mwanzo ni mgumu, hata tukifikia hatua huko inshaalla mambo yatazidi kuongezeka.

Lakini niseme hata mapendekezo ya kamati hii basi mimi naomba tuyazingatie kwa sababu wamependekeza mambo haya yana unafuu ya kutosha, hata baadae Mwenyezi Mungu akitupa uwezo zaidi, nchi yetu ukiwa na uchumi ulio mzuri tunaweza tukajiongezea, haya ni mambo ya mpito na ndio maana kila siku sheria zinaletwa hapa kufanyiwa marekebisho. Lakini kwa sasa hivi kwa marekebisho haya ya kamati, mimi naomba tuyazingatie vya kutosha.

Mhe. Spika, kwa kweli mengi yamezungumzwa na kama mengi yamezungumzwa kila tutakapopita ni pale pale. Lakini kwa sababu tupo kazini lazima tusimame tufanye kazi ya wananchi.

Jambo ambalo ni kubwa na ambalo limezungumzwa na wengi Mhe. Spika, ni hili baada ya kupewa vyama ruzuku hizi basi ni vyama vikaguliwe matumizi yake yametumika vipi, ili pesa hizi zitumike vizuri. Kwa sababu hizi pesa zinatokana na mifupani ya wananchi wetu, kwa hivyo kuzitumia kwa unavyopenda wewe mwenyewe si jambo la maslahi. Hivyo tunaomba kitengo hiki cha ukaguzi kiwepo ili kuhakikisha kwamba pesa hii imetumika vizuri.

Lakini vile vile mwisho kabisa ningependa kusema hivi ruzuku kwa upande wa viti vya Uwakilishi basi ni vyema kugawiana kwa wingi wa kura wa chama kinachopata. Mhe. Spika, kwa haya machache nasema ahsante sana na naunga mkono mswada huu asilimia mia juu ya mia.

Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Spika, kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria ili tuweze kuushughulikia ipasavyo…

Mhe. Spika: Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wanaopata dharura ya kwenda nje basi wajue muda mfupi baada ya hapa tutapitisha mswada huu na tunahitaji Wajumbe wengi wawemo ndani ya ukumbi.

Kwa hivyo nawaomba wote waliopo nje basi waingie ndani.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Vile vile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha mpaka wakati huu kuweza kuuchangia mswada huu ambao ni mzuri sana kwa sisi wanachama wote wa vyama vya siasa kuweza kupata mgawanyo huu ambao umepangwa, na kwa kweli mswada huu umepangika kiasi ambacho kilichopangwa ni kizuri hasa kwa vile wengi wamechangia suala hili liweze kuendelea kwa asilimia 25.

Kwa kweli hivi sasa mswada huu wakati wake ni mzuri kuweza kuchangiwa na kuhakikisha kwamba yote ambayo yametakiwa yanafuata kwa wakati ili tuweze kupata mchango mzuri katika majimbo yetu, ni asilimia hii iliyoekwa ndio inayoweza kutusaidia katika majimbo na wadi zetu.

Kwa kweli leo sina mengi sana kwa vile mimi ni mtu wa mwisho kuchangia, wengi wameshachangia mswada huu. Upande wangu ninaunga mkono suala hili liweze kuendelea na kupatiwa msaada ya asilimia hii inayotakiwa iweze kuendelea na iweze kushughulikiwa na vyama vyote kama ilivyokubalika, hasa kile chama ambacho kinatoa Rais kukamata dola ni vizuri kikapata ridhaa ya kuweza kupata asilimia hii iliyopangwa ya asilimia 25 na vyama vilivyobaki vikapata kwa mgawanyo uliotakiwa.
Kwa leo sina mengi zaidi naunga mkono asilimia mia kwa mia, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani. Ahsante ninashukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha tena kutufikisha tena jioni hii na kutusaidia kuelekea kukamilisha shughuli yetu hii. Mwenyezi Mungu atuzidishie uhai, atuzishie neema ili mambo yetu yaende vizuri zaidi.

Mhe. Spika, pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maelezo ya ufafanuzi na hatimaye tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakamilishe kazi yetu.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru sana Wajumbe wote wa Baraza hili kwa michango yao mizuri yenye manufaa kwa ajili ya kuimarisha mswada wetu huu ili uwe mzuri uweze kuleta malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, hasa shukurani za pekee ziwaendelee Waheshimiwa waliochangia mswada huu. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niwatambue:-

1. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Saleh Nassor Juma
5. Mhe. Rufai Said Rufai
6. Mhe. Mohamed Haji Khalid
7. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
8. Mhe. Hija Hassan Hija
9. Mhe. Suleiman Hemed
10. Mhe. Abdalla Mohamed Ali

11. Mhe. Omar Ali Shehe
12. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
13. Mhe. Panya Ali Abdalla
14. Mhe. Salmin Awadh Salmin
15. Mhe. Asha Bakari Makame
16. Mhe. Nassor Salum Ali
17. Mhe. Subeit Khamis Faki
18. Mhe. Fatma Mbarouk Said
19. Mhe. Mgeni Hassan Juma
20. Mhe. Hassan Hamad Omar
21. Mhe. Mussa Ali Hassan

Mhe. Spika, wajumbe wote hawa 21 waliochangia ukitizama wote walielekeza maoni yao kwenye suala zima la mgao ima la asilimia ya hoja yetu hii na kwa sababu hoja yenyewe haikuwa na mafungu mengi. Kwa hivyo Waheshimiwa wote ukitizama michango yao yote ipo ya aina moja, hivyo sitorudia tena kuelezea mheshimiwa huyu kasema hivi au hili, kwa sababu wote walikuwa na malengo mamoja Mhe. Spika.

Mhe. Spika, niishukuru kamati kwa ushauri wake ambao imesaidia sana kuhakikisha kwamba mswada leo kuweza kufika hapa na maoni yake yalikuwa ni sawa sawa na maoni ya serikali.

Vile vile nizidi kuishukuru kamati kwa maelekezo yake kwa nia ya kuzidisha ari ya kuimarisha serikali za mitaa, lengo lake kubwa ni kwamba walitaka tuitizame sana suala zima la mgao kwenye eneo la serikali za mitaa na serikali imefanya hivyo.

Vile vile napenda kuihakikishia kamati kwamba serikali imo mbioni katika kuhakikisha kwamba mswada wa sheria wa marekebisho ya sheria ya serikali za mitaa unaletwa hapa Baraza la Wawakilishi, upo katika hatua za mwisho mwisho, kwa hivyo naamini muda si mrefu wizara husika Mhe. Spika, itawasilisha sheria hiyo kwenye Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kuhusu ruzuku za vyama. Kuna Waheshimiwa Wajumbe walioeleza kwamba ruzuku hizi zinatolewa kwa upendeleo, kwa msingi kwamba kuna baadhi ya vyama vinapewa na baadhi ya vyama havipewi.

Mhe. Spika, nia si upendeleo wala hakuna nia yoyote ya kwamba ruzuku hii itolewe kwa upendeleo. Ruzuku hii inatolewa kwa vigezo, unapotimiza vigezo basi ndio ruzuku unaipata na hii inatokana na maamuzi ya wananchi wenyewe; wananchi ndio wanaoamua chama gain sasa kipate ruzuku hii, maana ni wananchi ndio wanaochagua vile vyama ambavyo vinakubalika vikatimiza masharti haya. Kwa hivyo hatuwezi kusema ni upendeo ni maamuzi ya wananchi na sisi kama serikali, kama Wajumbe wa Baraza hili tukufu hatuna budi kuuheshimu uamuzi huo wa wananchi.

Kuna waliosema kura mgawano huu uende kwa asilimia na kuna waliozungumzia mgawano huu uende kwa kiti. Mhe. Spika, kwa kifupi kwa nini serikali ilikubali mgawano huu uende kwa kiti.

Kwa sababu kiti ndicho kinachoshinda na kwa sababu utaratibu wetu tuliojiwekea ni wa *simple majority*, ina maana yeyote yule ambaye atashinda ndio inayomuwezesha kushinda na ndio anayepata kazi ya kusimamia shughuli, anayeshindwa kwa wakati huo siye anayekiendesha kiti, anayechukua jukumu la uongozi ni yule ambaye ameshinda. Kwa msingi huo ruzuku hii inatolewa ili isaidie shughuli za harakati za kusaidia wananchi.

Hivyo msingi wetu wa kusimama kwenye kiti ni kwamba kwa sababu kura idadi yoyote utakayoipata mwisho wa siku huyo atakayekuzidi ndio yeye atashika nafasi. Kwa hivyo anayeshika nafasi ndiye huyo atakayepata nafasi ya kuongoza katika eneo hilo na kwa msingi huo basi maana yake ni vyema tukasimamia suala la kiti badala ya asilimia ya kura.

Kwa sababu tukijiwekea asilimia ya kura Mhe. Spika, kutakuwa na wengi ambao wanaojitokeza kugombania kwenye ngazi mbali mbali, tokea kwenye udiwani, kwenye jimbo, Urais, hawa wote itabidi nao wapate. Tukiweka utaratibu huo lile tatizo ambalo tulilokuwa nalo la uwezo wa kumudu fedha ya kufanya shughuli hiyo itashindikana.

Kwa hivyo pesa ziliopo ni kidogo zinahitaji kufanyiwa kipaumbele na kipaumbele kikubwa ni kwenda kwa ajili ya kiti ambacho ndicho chenye dhamana ya kuongoza katika eneo hilo. Kwa hivyo nafikiri jambo la msingi hapa ni tuachane na tofauti zetu za kisiasa, tuweke maslahi makubwa ya nchi yetu mbele kwa nia ya kuimarisha umoja wetu na kujenga nchi yetu.

Kwa upande wa kiti cha Urais. Kiti cha Urais hakina sura ya chama, mwisho wa siku utakaposhinda Urais ni wa wananchi wote na unatakiwa utoe huduma kwa wote. Kwa hivyo chama cho chote kitakachoshinda Urais, maana yake kinaongoza wananchi wote na si wananchi wa chama fulani.

Kwa msingi huo inakuwa ni vizuri kukipa nafasi yake kiti hiki na uheshima ya Urais ili kiweze kufanya wajibu wake mzuri. Kama tulivyosema kwamba nafasi ya chama kinachotoa Rais ndicho ilani yake inatekelezwa. Kwa hivyo kuna wajibu vile vile wa kusimamia utekelezaji wa ilani. Kwa hivyo kuna majukumu ya kipekee kwenye nafasi hii. Hivyo nafikiri ushauri wa Waheshimiwa wale walioutoa na mapendekezo ya serikali na kamati kwamba basi twende kwa mujibu wa kiti cha Urais, nafikiri itatusaidia zaidi na tutajiwekea mazingira mazuri zaidi, kwa sababu kama walivyosema wengi hii nafasi leo anapata huyu, kesho anapata huyu na haikuekewa chama maalum lakini msingi wUrais ili kiweze kufanya wajibu wake mzuri. Kama tulivyosema kwamba nafasi ya chama kinachotoa Rais ndicho ilani yake inatekelezwa. Kwa hivyo kuna wajibu vile vile wa kusimamia utekelezaji wa ilani. Kwa hivyo kuna majukumu ya kipekee kwenye nafasi hii. Hivyo nafikiri ushauri wa Waheshimiwa wale walioutoa na mapendekezo ya serikali na kamati kwamba basi twende kwa mujibu wa kiti cha Urais, ninafikiri itatusaidia zaidi na tutajiwekea mazingira mazuri zaidi, kwa sababu kama walivyosema wengi hii nafasi leo anapata huyu, kesho anapata huyu na haikuekewa chama maalum lakini msingi wake ni yeyote atayefikisha lengo hilo ili aweze kupata fursa hiyo.

Mhe. Spika, hoja nyengine inahusu asilimia. Kuna baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi ambao walisema suala la kusema si zaidi ya asilimia mia moja ni bora tuwe na kiwango maalum. Hoja hapa Mhe. Spika, ni hali halisi ya uchumi wetu na ndio maana hapo mwanzo tulishindwa kuitekeleza vilivyo sheria hii kwa sababu ya uwezo.

Kwa hivyo tuliposema si zaidi ya asilimia moja msingi wetu ni kwamba itatuwezesha kuitekeleza asilimia hii, tukiweka *block rate* vile vile kutatokea mkwamo fulani, matokeo yake utekelezaji itashindikana. Kwa hivyo mimi ninafikiri Waheshimiwa tuendelee kukubaliana kwamba si zaidi ya asilimia moja na kwa sababu viongozi waliomo ndani ya serikali, wote wanatokana na vyama na kama wanatokana na vyama wataangalia tu ku-*maximize* kwa vyovyote vile ili kila ikiwezekana kuweka kiwango kikubwa kiwekwe kiwango kikubwa ambacho kitakachoweza kutekelezwa kutokana na hali halisi ya uwezo wa nchi wakati huo ili suala hili liweze kuwezekana.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba dhamira ya awamu ya saba ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni kuhakikisha kwamba sasa basi ruzuku hizi zinapatikana kwa vyama vya siasa kwa mujibu wa sheria yenyewe ilivyoekwa. Katika mwaka huu mara tutakapoitisha bajeti hii, ninawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe fedha zake zimetengwa ili vyama hivyo vipate ruzuku zao.

Kwa hivyo hakuna utata kwa kutekeleza sheria hii kama marekebisho haya yatapita, kwa sababu marekebisho haya msingi wake ni kuweza kutekeleza na msingi wake ni kwamba kiwango hicho cha fedha basi tayari kimetayarishwa kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa vyama vyetu vya siasa. Kwa hivyo nnachowaomba hapa Waheshimiwa tuwezesheni tuweze kutekeleza matakwa haya ya kisheria ili vyama vyetu viweze kupata ruzuku hii viisaidie katika shughuli zetu za kisiasa. Mhe. Spika, kuna swali pia liliulizwa hapa vyama vitapata mara mbili? Maana kuna vyama vina-*qualified* kupata ruzuku kwa mujibu wa sheria ile iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano na kuna vyama vile vile vita-*qualified* kupata ruzuku kwa mujibu wa sheria hii tunayopitisha Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, wale ambao kwa mujibu wa sheria waliokuwa wakipata ruzuku, utaratibu wake kwa upande wa Jamhuri ya Muungano unabakia pale pale. Kwa hivyo, ile ya upande wa Jamhuri ya Muungano itabakia na itaendelea kuwepo na wale ambao wana haki hiyo kupata wataendelea kupata, kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Mhe. Spika, tunayozungumzia kwa sheria yetu hii ni kwa sababu ya upande wetu wa Zanzibar, kwa maana ya Rais wa Zanzibar, Baraza la Wawakilishi na Madiwani. Kwa hivyo, haya ni ya upande wetu wa Zanzibar. Tunatengeneza hivi ili kuwawezesha vyama kwa upande wa Zanzibar, kufanya nao wajibu wao unaotakiwa kisiasa kama ambavyo sheria imeelekeza. Kwa hivyo, kila mwenye haki atapata kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria kama ilivyowekwa.

Kuhusu vyama vyote vipate Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba vyama vitakavyoweza kutimiza vigezo ndio vitapata, hatuchagui hapa. Leo kweli CCM na CUF wamo ndani humu wameweza kutimiza masharti watapata, na kesho chama chengine chochote kile kitakachoweza kutimiza masharti watapata. Cha msingi ni kwenda kwa wananchi na kuwahamasisha waviunge mkono ili wawezeshwe kutimiza masharti haya. Hapa tusitafute njia ya mkato, kila chama kiende kikalime kwa wananchi, kijieleze kwa wananchi, kipate ridhaa ya wananchi na kipate maamuzi ya wananchi ili wapate haki hiyo. Tungekuwa tuna fedha nyingi za kutosha basi tungeamua vyengine, lakini fedha zenyewe ni kidogo na wananchi wa nchi hii wanataka hizi fedha zitumike kwa msingi maalum kutokana na utaratibu wa sheria iliyopo. Kwa hivyo, vyama vitapata hapo ambapo vitakapoweza kutimiza vigezo, haitakuwa kila mmoja apate.

Ukitimiza vigezo fedha hizi ni za umma, wenyewe wananchi wameweka utaratibu wao wa kukuchagua na ukiweza kufanya hivyo maana yake uta-*qualify* kupata ruzuku hiyo.

Kuhusu kiti cha Urais kupata asilimia 25 ama 20. Mhe. Spika, serikali ilikuja na mapendekezo ya asilimia 20 ili kuweka uwiano mzuri wa kisiasa na kupunguza malalamiko ili kuimarisha umoja wetu. Lakini hoja hii ambayo Wawakilishi wametoa ya kwamba twende kwenye asilimia 25 kama ilivyokuwa awali. Kwa upande wetu serikali sisi hatuna matatizo nayo, vile ambavyo Wawakilishi wataona inafaa kwa msingi huo, sisi hatuna tatizo. Lakini ushauri wetu na Kamati ulikuwa ni asilimia 20, lakini madhali Waheshimiwa Wawakilishi wanaomba twende kwenye asilimia 25 hatuna tatizo kwenye suala hilo.

Mhe. Spika, kuhusu mgao wa udiwani sasa, ukishaamua kukipa kiti cha Urais asilimia 25, maana yake tayari umeipunguzia mgao wa udiwani kwa asilimia 30 na maana yake msingi huo unaifanya iwe asilimia 25. Kwa sababu maoni ya humu ndani hakuna hata mmoja aliyegusa suala la mgao kwenye upande wa uwakilishi, wamekubaliana mia kwa mia na suala la asilimia 50. Kwa hivyo, ukizipunguza zile asilimia 25 basi huendi kuzigusa za mgao wa uwakilishi, unazigusa za mgao wa udiwani ndizo zilizozungumzwa. Kwa msingi huo basi utakuwa umepunguza ile asilimia 30 ya udiwani, tukishakubaliana hivyo, tukubali tu kwamba na sasa asilimia ya udiwani itakuja asilimia 25, tukikubaliana hilo basi serikali haina matatizo kwenye suala hilo.

Kuhusu ukaguzi wa fedha za ruzuku. Mhe. Spika, fedha zote za ruzuku ni fedha za umma zinazotoka katika mfuko mkuu wa serikali. Sheria ya fedha na sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, inaeleza moja kwa moja kwamba fedha hizi za serikali zinapotumika popote kule ni fedha za umma, kwa hiyo wao moja kwa moja wana haki ya kufanya ukaguzi. Kwa hivyo, hakuna kipingamizi chochote kile fedha hizi zisikaguliwe, utaratibu wa kukaguliwa zitakaguliwa kama fedha nyengine zozote za umma zinavyokaguliwa. Kwa hivyo, ikiwemo kwenye sheria isiwemo kwenye sheria utaratibu uko *very clear* kwenye sheria nyengine, kwa hivyo moja kwa moja wanafanya wajibu wao. Kwa hivyo, kwenye hili sioni tatizo lolote lile.

Mhe. Spika, kuhusu dira ya matumizi ya fedha. Dira ya mtumizi ya fedha katika sheria yenyewe tayari imeshaelekeza. Ukisoma sheria ile kifungu cha 5(1) kinaeleza vizuri kuhusu matumizi ya fedha zenyewe kuanzia 5(1) (a) mpaka (d), imeweka utaratibu wa matumzi hayo ya fedha. Kwa hivyo, pale maana yake dira ipo, ukiisoma utaiona pale. Nafikiri kwenye suala la dira utaratibu upo wa matumizi, suala la ukaguzi utaratibu wa kisheria upo. Kwa hivyo, hapa tunachotakiwa kukifanya ni kupitisha mgao na asilimia yenyewe ili tuweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, wengine walilalamikia kwamba fedha huko nyuma zilichelewa kutolewa, tokea mwaka 1997 basi kulipwe *arrears.* Tatizo letu ni kwamba hakukuwa na fedha ndio sheria isitekelezwe, ndio ikabidi tubuni mbinu nyengine ya kutekeleza sheria yenyewe. Sasa hizo fedha za *arrears* Mhe. Spika, zitakuwa hazipo, cha kufanya hapa tujikune tunakojipata, uwezo wetu tulionao ni huu, kwa hivyo msingi sasa wa kutekelezwa ni kutokana na uwezo wetu. Naelewa kwamba kweli vyama vyetu vilikosa fursa hiyo, lakini inabidi tuvumiliane ndio njia na hali halisi iliyojitokeza.

Kwa msingi huo basi Mhe. Spika, napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba mara tu watakapopitisha sheria hii, basi tatizo la fedha sasa kwa ruzuku za vyama litakuwa limeondoka na utekelezaji utakwenda vizuri.

Mhe. Spika, naamini kwamba baada ya maelezo yangu haya mambo yote yatakuwa yamejijibu kijumla jumla, kutokana na hali halisi, na kama kutakuwa na suali lolote Mhe. Spika, basi Waheshimiwa Wajumbe wanayo nafasi ya kutuuliza zaidi. Lakini ningependa tuipitishe sheria hii ili tuweze kutekeleza ipasavyo.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja, nashukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru, kwa ufafanuzi wa hoja mbali mbali ambazo Wajumbe walizitoa. Basi Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya mswada huu wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya kutunga sheria, ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ya Mwaka 2012

SEHEMU YA KWANZA

Masharti ya Awali

Kifungu cha 1 Jina fupi na Kuanza Kutumika pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 2 Kusomeka.

Kifungu cha 3 Tafsiri.

SEHEMU YA PILI

Marekebisho

Kifungu cha 4 Marekebisho ya Kifungu cha 3.

Kifungu cha 5 Marekebisho ya Kifungu cha 4 pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Kwenye mswada kama ulivyo hapa kuna hiyo asilimia 25, 50, 25. marekebisho yalikuwa ya kwenye Kamati ambayo yaliifanya asilimia 20, 50,30. Sasa hapa inabidi tujue ni marekebisho yapi, kwa sababu kuna marekebisho mengine yamekuja hapa kwa mujibu wa maelezo yaliyotoka hapa na pale.

Labda niende kama huu mswada ulivyo humu, ili tuone kama ndivyo hivyo au vyenginevyo, kwa sababu kuna maoni mawili. Kuna maoni ya Kamati na kuna maoni ya Wajumbe humu ndani. Kwa hivyo, sasa niende kwenye huu mswada kama ulivyo kabla hata ya hayo marekebisho.

Kifungu cha 5 ambacho kinarekebisha kifungu cha 4, kinakubaliwa.?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndiyoo.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na mabadiliko yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ya Mwaka 2012, usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake, katika kusomwa kwa mara ya tatu wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa leo mmemaliza kazi, baada ya mashirikiano makubwa mliyotoa kwa kuchangia mswada huu kuanzia asubuhi na hivi sasa kwenye saa 12:15 sasa kazi yenu mmeimaliza kwa leo. Sina budi nikushukuruni kwa kazi nzuri mliyoifanya na kwa kuwa *order paper* haioneshi kama kuna kazi nyengine kwa leo, basi tukubaliane tukapumzike. Kwa maana hiyo sasa naakhirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 17/01/2013 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 12:15 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 17/01/2013 saa 3:00 za asubuhi)